KUDHANIA

Kuwa na wakati huu wa ushirika pamoja na ninyi watu, mbali sana na ile kaskazini iliyoganda ambako ndiyo kwanza nimetoka huko. Nilimwambia mchungaji wenu, huko kwenye chumba chake cha kusomea alasiri ya leo, "Huu utakuwa mmoja wa mikutano mikubwa sana niliyopata kuona, la sivyo nilikosa kuona mapenzi ya Bwana." Sijapata kupigwa vita vikali na Shetani kama alivyofanya nikija hapa. Wakati Ndugu Williams aliponialika wakati fulani uliopita, kwa namna fulani nilisitasita kidogo. Nikasema, "Nitakujulisha baadaye kidogo, kwa kuwa ninaamini katika kuomba kwa ajili ya mambo kabla ha—hatujatoa uamuzi wetu. Na iwe ni chaguo la Mungu."

2 Nami nilidumu kujisikia nikiongozwa kuja, kwa kuwa ulikuwa ni wakati... Daima ninauthamini Ushirika wa Wafanyabiashara wa Full Gospel. Halafu basi... Na huu ulikuwa ni wa ziada kidogo, kwa maana ningeweza kukutana na makanisa mbalimbali, ndugu mbalimbali wa madhehebu mbalimbali. Ninapenda kufanya jambo hilo, na kwa namna fulani kufanya ushirika wa pamoja katika makanisa mbalimbali, wa—wa makanisa yote ya Mungu. Kwa hiyo basi wakati...

3 Nilisema, "Nitakuwa na hakika sasa ya kwamba ni Bwana anayeniita." Nikasema, "Nitampa Ndugu Williams wakati mwingi wa kumpata mtu mwingine, unajua, kwenda kule. Kuwa—kuwa na hakika, ya kwamba, kama angali ananingojea, basi ninajua ni Bwana, na kama ndugu wote wakisema wanataka nije huku." Nikasema, "Baba wa Mbinguni, nitachukulia tu ya—ya kwamba Wewe unataka niende Phoenix."

4 Vema, basi, nilingojea siku kadhaa. Nikawazia, "Sasa, afadhali nimfahamishe mara moja, kwa maana yeye ni... Inawabidi kuutangaza katika—katika *Sauti* ya Wafanyabiashara."

5 Na kwa hiyo baada ya kungojea siku chache, ndipo nikampigia simu. Akasema, "Loo, Ndugu Branham, ndugu wote wanataka uje huku." Kwa hiyo nikasema... Nilisikia tu ule muashirio mdogo ninapaswa kwenda, kwa hiyo hii ingekuwa ni fursa nzuri sana.

6 Vema, nilidhani ningekuja ma—mapema kidogo. Pia nilitaka kwenda Mexico na kujinunulia sanduku la nguo nililokuwa nikihitaji sana. Hilo, mtu fulani alinipa pesa wakati wa Krismasi, kulinunua, nami ningeweza kulipata kwa nusu ya bei ambayo ningelililipata hapa, na ni zuri maradufu, nikivuka mpaka. Nikawaza, "Vema, nitashuka niende huko Texas, kwa hiyo nitajitengea kama siku tatu hivi za ziada niweze kulitafuta

madukani na kupata zuri, hivyo basi nipumzike kidogo nikiwa safarini." Nami nilikuwa nianze Alhamisi.

7 Nasi tulijiandaa kabisa kuanza, ndipo ikaja dhoruba kali ya theluji kote nchini, na hata wakafunga barabara kuu, kila mahali. Na Kusini kulikuwa hakupitiki, kabisa. Wala wasingeturuhusu kupitia sehemu za kaskazini, huko 66.

8 Nilingojea siku mbili, na hatimaye wakafungua barabara, kasema, "Mnaweza kubahatisha." Kwa hiyo nikashika njia.

9 Niliwazia, "Vema, itakuwa hali nzuri ya hewa." Aha! Sidhani nilipata kuwa katika dhoruba kali zaidi ya theluji, maishani mwangu mwote; na barafu na msongamano wa magari, na kote barabarani, na kila kitu.

10 Hatimaye, mmoja wa vijana wa kurekodi hapa, Ndugu Maguire, gari lake lilichurupuka, alipokuwa akija huku. Tulikuwa tukiendelea. Na kwa hiyo tulikuwa tuna ninii mbaya sana . . . Nafikiri liliharibika tu. Sidhani lilimwasi. Liliharibika tu, unaona. Na kwa hiyo akachukua jenereta ya zamani, wala kitu hicho kisingeanza vizuri. Ndipo akajaribu tena, wala isingeanza vizuri. Akaiweka kwenye duka lingine; isingewaka vizuri. Akajaribu tatu, tukaendelea hadi kama saa tano usiku mmoja, na bado kitu hicho . . .

11 Kesho yake asubuhi, tukaanza. Nyekundu ingeninii . . . Aliingia huku kisiri. Sasa, yuko mahali fulani akinisikiliza. Sijapata kamwe kuzungumza jambo hilo hata kwa baba mkwe wake na hao wengine. Lakini alinigusa begani, alipokuwa akitoka kwenye mgahawa, kasema, "Ndugu Branham, hebu mwombe Mungu tu, nayo itafanya kazi vizuri."

Nikasema, "Kweli unaamini jambo hilo?"

Akasema, "Ninaamini."

Nayo ikafanya kazi vizuri. Tukashuka tukaja.

12 Kwa hiyo nilipofika Phoenix, nikawaza, "Sasa shida yangu imekwisha." Na kama sikuamka asubuhi ya leo nikiwa na homa ya mafua, kuumwa na kichwa na kujisikia vibaya.

Vema, nikasema, "Shetani, ni vita."

13 Kwa hiyo mimi hapa. Kwa hiyo tuko hapa kufurahia ushirika huu. Nami niliweza kukutana na mchungaji alasiri ya leo, kwenye chumba chake cha kusomea hapa juu, nasi tulikuwa na wakati mzuri sana. Kanisa zuri dogo jinsi hiyo. Nami nawaletea salamu kutoka katika nyumba yote ya Mungu, huko katika mashariki ya kati, ninakotoka. Na kwa hiyo tunajua ya kwamba mnaendelea vizuri sana hapa nje. Tunasikia kutoka kwenu.

14 Pia nafurahi kumwona Ndugu Norman ameketi hapa usiku wa leo, kutoka Tucson. Nami nina watu fulani . . . Ninaangalia kwenye kusanyiko hili dogo hapa, na kuona watu kutoka huko Ohio, ndugu na Dada Dauch wameketi hapa. Na ninaamini

hawa ni watu kutoka Iowa, wameketi moja kwa moja nyuma yetu hapa, na—na watu mbalimbali. Wametoka tu mashariki na magharibi, sivyo, kila mahali, wakitiririka pamoja? Kwa hiyo tunafurahi kuwa hapa.

15 Na sasa tunatazamia siku za usiku tuliopangiwa kuzungumza kwenye makanisa mbalimbali. Nafikiri, kesho usiku, tutakuwa huko Tempe, ilikuwa hivyo? [Ndugu mmoja anasema, "Naam, huko Tempe."—Mh.] Tempe. Halafu basi, usiku ufuatao, nafikiri, kwa . . . ["Ndugu Outlaw."] Kwa Ndugu Outlaw. Hiyo ni ninii . . . ["Ya 20 na Roosevelt."] Barabara ya 20 na ya Roosevelt. Halafu, mbalimbali. Na ninii . . .

16 Kama ninyi ndugu mko hapa, ambapo ilinibidi kukosa siku hizo mbili usiku, ninasikitika juu ya jambo hilo. Lakini Bwana atatupa baraka maalum kwenye asubuhi hizo za Jumapili ambapo tutazifidia. Kwa hiyo kwa namna fulani ni ratiba kamili iliyojaa, lakini kwa neema ya Mungu tuta—tutafaulu.

17 Halafu tunatarajia wakati mzuri sana katika mkutano huu unaokuja, huu, mkutano wa Wafanyabiashara. Nina furaha sana kwa ajili ya fursa hiyo, labda nitaweza kukutana na ndugu hao wote, na kuwapa mkono. Na ni—ni jambo zuri, kukutana na marafiki. Nasi tu—tu- . . . Hakuna kitu kizuri kama marafiki.

18 Nitanukuu jambo fulani nililomnukulia mchungaji alasiri ya leo. Oswald J. Smith, yeye ni mtu mashuhuri mwenye moyo wa kimishenari. Alikuwa akizungumza, wakati fulani uliopita, huko Louisville, Kentucky, na rafiki yangu, Dkt. Wallace Cobbles. Naye akamwambia Ndugu Cobbles, akasema, "Ndugu Cobbles, ni—ninaamini ya kwamba wakati mtu anapofunga ndoa mara ya kwanza," akasema, "na mke wake ni kijana na ni mzuri wa sura na kila kitu," kasema, "unajua, kama ikitokea kwamba aharibike, atoroke nyumbani, kama tunavyosema, akimbie zake, awe mzinzi, ama chochote kile, mwajua, atoke nje na kufanya mambo mabaya," kasema, "inakubidi kumwacha, ama chochote kile," kasema, "ni jambo baya, bali sivyo." Kasema, "Unaweza . . . Wewe ni kijana, na unaweza kujitafutia, labda, na umpate mwingine atakayefaa." Kasema, "Ndipo baada ya kuishi naye kwa muda mrefu vya kutosha, mpaka watoto waje," kasema, "ni vigumu sana, anafanya hivyo basi, unajua." Kasema, "Unaanza kutambua ya kwamba kweli unamhitaji." Kasema, "Unapofikia kwenye umri wa miaka hamsini hivi," kasema, "ndipo ni vigumu sana kwako kumwacha." Kasema, "Ndipo wakati unapofikia kwenye umri wa miaka sabini, hakika huwezi kumwacha."

19 Ikatukia kwamba niliwazia, kwa namna fulani nikaweka tafsiri ndogo ya kiroho kwa jambo hilo. Nilipokuwa mhudumu kijana, kila mtu aliyefanya kosa, alitengwa kabisa. Hata asingeweza kushiriki katika mbio. Hivyo tu. Kama hakuwa Mbaptisti, alitengwa kabisa, hivyo tu. Unaona? Ilimbidi tu

kuona mambo niliyoyaona mimi, la sivyo mtu huyo alikuwa amekosea kabisa.

20 Halafu basi wakati nilipokuwa na umri mkubwa kidogo, nilianza kutambua ya kwamba, unajua, blanketi kwa namna fulani lilitanda kidogo. Niliona ambapo ilimbidi, yale yaliyombidi kupitia; kazi ngumu sana, mchungaji wa kanisa, na uchungu wa moyoni unaoambatana na hayo. Nilitambua ya kwamba blanketi hili hutanda kidogo juu yake, pia, mwajua, kwa namna fulani kumkinga na baridi. Na sasa tunaposhuka kuja kwenye mahali kama nilipo mimi sasa, na—na—nawaambia; tunahitajiana sana mmoja kwa mwingine, ni vigumu kabisa kuachana. Ni hilo tu.

21 Na tunapoona siku zikiwa mbaya, na jinsi mambo yalivyo, mbona, nafikiri ni vizuri kwamba tukutane na kushirikiana pamoja. Nami ninatamani sana kukutana na ndugu, na kuzungumza nao, na kadhalika. Makanisa yote mbalimbali, na—na udugu, na—napenda jambo hilo. Mnaona, ni kitu fulani kuhusiana na jambo hilo, ambacho ni halisi.

22 Nami ninafikiri, si kulitangazia kundi hili la watu, la Wafanyabiashara wa Full Gospel, bali ninafikiri ya kwamba hiyo ni fursa kuu ambayo Mungu ametupa sisi sote, ambapo tunaweza kukusanyika katika hilo, na tunaweza kuwa na ushirika. Hawaweki mpaka wowote kuhusu madhehebu yoyote, na kadhalika, nasi tunaweza kuketi pamoja katika ulimwengu wa Roho katika Kristo. Sasa, ninatambua ya kwamba halitakuwa kamilifu. Watafanya makosa mengi. Ninaona yao, nao wanaona yangu. Nanyi mnaona yangu; ninaoana yenu. Na, bali inatubidi ku—inatubidi kuishi pamoja, na inatubidi kutambua. Lakini nafikiri, hata hivyo, kama jambo zima likichunguzwa, kwa upande wangu, ni watu walio bora kabisa. Unaona? Hiyo ni kweli. Ni hili.

23 Nimechagua kuwa pamoja na Full Gospel, miaka kadhaa iliyopita, nami nina furaha zaidi kila siku kuhusu jambo hilo. Nami ni—nina furaha kuwa mmoja wao. Na nikiwa na tukio hili zuri sana la kumpokea Kristo kama Mwokozi wangu, na, kwa kuitikia basi, kumfanya anijaze na Roho Wake Mtakatifu, na akiishi moyoni mwangu, kila siku, kama shahidi kwangu, ya kwamba nimepita toka mautini kuingia Uzimani. Nikiujaribu mmea wangu wa wokovu wangu, kila siku, ninapofanya hesabu. Kuona tu jinsi ambavyo Roho ndani yangu, anahisije? Anashirikianaje na mambo ya ulimwengu? Ama, je! hivi ameelekea Mbinguni hata ulimwengu unaonekana usiovutia, na ovyo ovyo, na mchafu?

24 Nilikuwa nikipitia hapa mtaani. Nilikuja hapa mara ya kwanza, miaka thelathini na mitano iliyopita, mwaka huu, 1926, katika Ford ya kale ya muundo wa T. Nami niliishi huko kwenye mtaa wa Kumi na Sita na Henshaw. Ninaona hata

wamebadilisha jina hilo. Ni Buckeye sasa huko nje. Kwa hiyo kila kitu kinabadilika. Bali ninapatambua mahali hapo pa kale. Mwajua, nilipanda farasi karibu na hapa nikaenda huko chini bondeni, Mto wa Chumvi, na kupitia kule. Vema, walikuwa na punda wadogo ng'ambo ya pili ya mlima ule pale, punda wadogo wa mwitu, mnaona, na maskini watafuta madini wa kale wangekuja. Jamani! Wangali wana watafuta madini wanaokuja, bali wako katika Makadilaki, kwa hiyo ingali ni vile vile. Kwa hiyo ku—kumebadilika sana.

25 Lakini ninaona ya kwamba Injili haibadiliki; ingali inaleta ridhaa ile ile. Nawe ukirudi, miaka baada ya miaka, unakuta kwamba ni vile vile. Ni tukio lile lile walilopata Pentekoste. Baada ya miaka elfu mbili, halijabadilika hata kidogo. Tunapata jambo lile lile, mnaona, jambo lile lile tu lililofanya.

26 Nilipokuwa nikiangalia barabara hizo nzuri sana, na kuona mahali hapo na taa, na—na sehemu hizo pamewashwa taa, niliwaza, "Miaka mia tatu iliyopita..." Nilipokuwa nikizungumza na mwanangu, tukija huku. "Bonde hili lilikuwa lina amani na utulivu. Labda wakati mwingine mbwa mwitu angelia, ama—ama kelele fulani, punda mwitu mdogo angelia, ama—ama miaka mia tatu iliyopita. Na tunapoangalia jinsi ambavyo imekuwa, sijui kama mnasema ni kuongoka ama ni kupotoshwa, kufikia lilivyo sasa.

27 Ingekuwa ni mwongofu kama barabara hizi zilikuwa zikitembelewa huku na huko, na watu, wakiwa wameinua mikono yao juu kwa Mungu, wakimsifu Mungu kwa ajili ya bonde zuri, na mahali pazuri pa kuishi, na hali nzuri ya hewa; na wakimsifu Mungu katika makanisa, na ndugu walikuwa ni ndugu, na dada, na kadhalika, koloni kuu tu la uchumi wa Mungu; pangekuwa ni mahali pazuri sana.

28 Lakini badala ya jambo hilo, kukiwa na vilabu vya pombe, baa za pombe rahisi, umalaya, kuvuta sigara, kucheza karata, matusi, kutukana. Ninawazia tu siku moja ya kwamba Mungu atafagilia mbali kitu hicho chote. Hiyo ni kweli. Na wale wanaomchagua Yeye wataishi tena hapa katika wakati usio na mwisho, ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu utakaokuja.

29 Na ni kusudi langu, na kile kilichonileta hapa Phoenix usiku wa leo, ni kujaribu kushiriki, kwanza, kulitia kanisa nguvu, kuwaombea wagonjwa kama yeyote akija kuombewa. Hatukusudii kusambaza kadi zozote za maombi, ama kadhalika. Tunakuja. Tungefanya tu kila tuwezacho kuwasaidia watu. Kama mtu anataka kuombewa, jambo pekee utakalofanya ni kuomba, nasi tutawaombea, chochote tunachoweza kufanya. Nilikuta kwamba nyumbani, majuma machache yaliyopita, kufanya jambo hilo, ni zaidi sana ya jambo lingine lolote, mnaona.

30 Nami ninakumbuka nilipokuja kwa mara ya kwanza hapa Phoenix. Tulisimama pale kwenye kanisa la Ndugu Outlaw, ndiye wa kwanza aliyenialika Phoenix. Na halafu kulikuwa na kanisa dogo la Kimeksiko, lililoitwa Garcia, Ndugu Garcia, maskini kanisa dogo lilililozungumza Kihispaniola mahali fulani kule chini. Na ni wakati mzuri jinsi gani tuliokuwa nao kule, na watu wakisimama kwenye mistari ya maombi, na wakiponywa, kuomba tu na kuwawekea mikono.

31 Huduma imepanda juu zaidi. Hakika, imepanda. Karama zimeongezeka. Lakini kwa namna moja au nyingine, laiti ningalikuwa kama nilivyokuwa huko nyuma mara ya kwanza, unaona. Ninii tu. . . Unaona? Naam. Nafikiri, zaidi hapa. Tunasahau tu baadhi ya mambo waliyopata kujifunza, nafikiri ingalikuwa ni bora zaidi. Mnaona?

32 Vema, nafikiri njia ya kumwendea Mungu ni kupitia njia ya unyenyekevu na kutumika. Nafikiri ya kwamba hakuna jambo lingine lililo bora zaidi ulimwenguni, kutuinua juu kwa Kristo, kuliko hilo. Unapata kuona uigaji wa kimwili, na kadhalika, inakudhoofisha na kuweka kitu fulani ndani yako. Na—natamani isingalifanya hivyo, unaona. Tunaninii tu. . . Kama ulijifanya tu. . . Kwa namna fulani inakuinua. Nafikiri inakuweka katika hali ngumu sana, wakati hupaswi kuwa kule. Inakupasa kuweka mambo yote mbali, na kuendelea.

33 Na kwa hiyo basi ninatumaini ya kwamba, katika jambo hili, litaimarisha shirika zetu pamoja, mmoja kwa mwingine. Tunaomba ya kwamba Mungu atawaponya wagonjwa watakaoombewa. Na zaidi ya yote, amwokoe kila mtu anayeweza kuokolewa. Sijui wako wapi, hao ni akina nani. Kwa hiyo ninaninii tu—ninavyohubiri tu, na chochote kinachoingia, hapo ndipo ninapojaribu kuwahudumia. Na kutumainia ya kwamba siku moja katika huo Umilele mkuu, na bonde la amani, labda si Maricopa, bali bonde fulani lenye amani mahali fulani, tutaishi pamoja, majirani kote katika nyakati zisizo na mwisho. Hiyo ndiyo sababu tupo hapa.

34 Sasa, wengi wanasimama. Nami. . . Ninyi ni wazuri sana, ningeweza kuzungumza usiku kucha. Na—na kwa hiyo ninajua tuna ibada kadhaa, wala sitaki kuchukua wakati mwingi kupita kiasi katika kila mahali.

35 Lakini kama tutainamisha tu vichwa vyetu sasa kwa uchaji kabla hatujafungua Neno la Mungu, na tuombe.

36 Baba yetu wa Mbinguni wa neema, kwa kweli ni majaliwa mazuri usiku wa leo kuwa hai, kuwa na nafasi ya kushuhudia tena mbele ya Kanisa la Mungu aliye hai. Na kama nilivyokuwa nikizungumza na watu hawa muda mfupi uliopita, na kuwazia juu ya jiji hili kubwa mno, linalopendeza, hata hivyo limelemewa na dhambi kama miji mingine yote, nilikuwa nikifikiri kama vile mwanangu alivyosema, "Kuna faida gani basi, baba?"

37 Nikasema, “Mwanangu, kote katika jiji hili kumetawanyika kanisa la Mungu aliye hai. Kundi hilo ndilo tunaloliinua juu mbele za Mungu. Ni hao—hao watakatifu.”

38 Kama ambavyo hapana shaka Paulo aliuangalia Roma, kukiweko na maelfu mengi ya wakazi wake, na mahali mbalimbali alikokwenda, angeona jiji hilo limeigeukia ibada ya sanamu. Lakini kulikuwako na lulu katika jiji hilo, aliyopaswa kushughulikia. Wanastarehe huko ng’ambo, wakingojea ufufuo wa kiama katika siku ya mwisho, ambao tunaamini umekaribia.

39 Tunaliombea kila kanisa Phoenix. Kila moja ya hayo, Baba, tunaomba ya kwamba utamwaga Roho Wako juu ya hao wote. Jalia kuwe na taa kama hizo zikiiangazia Injili, mpaka zingeweza kufifisha taa za vilabu hivi vya usiku na vilabu vya pombe haramu. Tujalie, Bwana. Jalia mioyo ya watu ikuonee kiu sana katika wakati huu wa kuzuriwa, na naomba Wewe utuzuru kwa uhakika, Bwana. Tuzuru kwa Roho Wako, na ummimine juu yetu katika vipimo vikubwa, Bwana.

40 Bariki mkutano unaokuja. Ninaomba, Baba, ya kwamba kutakuwa na wafanyabiashara wengi, na wengine, watakaoongozwa kwenye ujuzi huu mkuu wa kumjua Kristo kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Tujalie, Bwana.

41 Bariki kanisa hili tulimo ndani yake hapa usiku wa leo, maskini mchungaji wake mzuri sana, utu wa—wake wote, Bwana. Linasimama hapa kama mfano. Ni taa kwa ajili ya mji huu, ili watu wapate kuiona njia ya kweli. Ninaomba ya kwamba utawafanya washiriki wake wakolee chumvi sana ili kila mmoja katika eneo hili, na kote jijini, atatamani sana kuwa kama wao.

42 Sasa, ninajua ya kwamba unayasimamisha makanisa haya hapa kwa kusudi fulani. Yanasimama kama shahidi dhidi ya maovu. Na kuna ushuhuda ndani yao ya kwamba Mungu ni mwenye haki na ni wa kweli. Ninaomba ya kwamba ungewabariki, Baba, sana.

43 Sasa, kwa ajili ya sehemu hii ya ibada inayokuja usiku wa leo, hapana shaka kwamba umemwaga baraka Zako juu yao. Tunaomba ya kwamba utatubariki, Bwana, kwa Uwepo Wako mkuu. Nena kupitia sisi, kwa Neno, katika Roho. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

44 Alasiri hii nilipokuwa nimeketi, nikisoma, macho yangu yaliangukia juu ya fungu dogo hapa ambalo huenda nikataka kusoma, na kutumia sehemu yake kwa ajili ya fungu husika, Mungu akipenda. Nami niliandika baadhi ya Maandiko na mihtasari michache, ningetaka kuwazungumzia kidogo juu yake, kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

45 Sasa, ninyi mnaotaka kufungua, hebu na tufungue Hesabu, mlango wa 14, na kuanzia kifungu cha 41. Hesabu 14:41, nasi tutasoma, kinapoanza.

Musa akawaambia, Kwa nini ninyi sasa kuyahalifu maagizo *ya* BWANA*? maana halitafanikiwa jambo hilo.*

Msikwee, kwa kuwa BWANA *hamo kati yenu; msipigwe na kuangushwa mbele ya* adui *wenu.*

Kwa kuwa Waamaleki na Wakanaani wako mbele yenu, nanyi mtaanguka kwa upanga, kwa sababu mmerudi nyuma msimwandame BWANA*, kwa sababu hiyo* BWANA *hatakuwa pamoja nanyi.*

Lakini walithubutu kukwea mlimani hata kileleni, ila sanduku la agano la BWANA *halikutoka humo maragoni, wala Musa hakutoka.*

Ndipo Waamaleki, na Wakanaani waliokaa mlimani. . .huko mlimani, wakatelemka, wakawapiga na wakawaangusha, *hata kufikilia Horma.*

46 Bwana na aongeze baraka Zake kwenye kusomwa kwa Neno Lake. Ninataka kuchukua somo kutoka hapo, Bwana akipenda, juu ya somo la: *Kudhania*. Ni ninii . . .

47 Ninapenda tu kusoma Neno, kwa sababu ninajua ya kwamba Hilo ni kweli. Neno ndilo tunalodumu nalo. Haina budi kuwa ni Neno la Mungu daima, la sivyo tu—tutapitia njia mbaya.

48 Imeandikwa katika Yohana Mtakatifu, nafikiri, kama mlango wa 15, "Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu." Unaona? Neno linakaa ndani yenu. Unaona? "Basi ombeni mtakalo, nalo litatimizwa." Kwa kuwa, si wewe. Ni Neno lililo ndani yako. Nalo Neno ni Mungu, unaona, Mungu ndani yenu. Mungu ni Neno. "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Naye Neno alikuwako kwa Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu."

49 Sasa, katika kurudi kwa Roho Mtakatifu, akileta Neno ndani yetu, nalo linakaa mle ndani, basi si wewe unayenena, ni Neno Lenyewe likitoka. Kwa hiyo Hilo, Neno, litafanya hiyo kazi.

50 *Kudhania*, nilichukua kamusi na kuangalia neno *kudhania* linamaanisha nini hasa. Webster inasema linamaanisha "kujasiria bila mamlaka halisi." *Kudhania* chochote, ni "kuthubutu bila mamlaka halisi, ama kuchukulia. Kujasiria bila mamlaka halisi, ama kuchukulia. Kufanya jambo fulani kabla hujapewa mamlaka ya kulifanya; bila ya mamlaka halisi ya kulifanya."

51 Sasa, ndio kwanza tupite likizo mbili zilizo kubwa, ambazo tunazijua hapa Marekani kuwa ni wakati wa Krismasi na ya Mwaka Mpya. Kwa kweli sio Krismasi. Ni siku ambayo tulitenga. Hakika, tunatambua si siku ya kuzaliwa kwa Bwana. Asingeweza kuzaliwa tarehe 25 Desemba, kwa maana ni—ni baridi sana kule juu, wachungaji wasingeweza kuwa kilimani, na kadhalika. Na kama ulipata kuwa huko Uyahudi kwenye wakati huo wa mwaka, ungejua haikuwa—haikuwa kwenye majira ya

baridi kali. Lakini inadhaniwa kwamba labda ilikuwa ni kwenye Aprili ama Mei, wakati wana-kondoo wanapozaliwa. Na kama vile Yeye anavyokuja kwa maumbile yote, kama tu vile wana-kondoo wa kawaida wanavyozaliwa; Yeye alikuwa ni Mwana-Kondoo wa Mungu, Naye alizaliwa kwenye wakati huo. Lakini sidhani Yeye anajali ni siku gani tunayotenga, kwa maana siku yenyewe imepotea. Lakini ni katika kumbukumbu la siku ya kuzaliwa Kwake.

52 Badala ya sisi kuifanya kumbukumbu na siku ya kumwabudu Mungu, kwa kumtuma Kwake Mwanawe kwetu, tuna sherehe. Unaona? Tunasherehekea Krismasi. Wala si sherehe. Ungeweza kusherehekea siku ya kuzaliwa kwa Washington ama siku ya kuzaliwa kwa Lincoln. Ama siku ya kuzaliwa kwa mtu fulani mwingine mashuhuri, huenda ukaisherehekea. Lakini Krismasi inapaswa kuwa ni siku ya kuabudu. Tumeibadilisha na kuifanya moja ya siku kubwa sana za kibiashara. Yote imeandaliwa kwa kupeana zawadi mmoja kwa mwingine, na kuudhika kama hatufanyi jambo hilo, na kuzilipa. Na yote imebadilishwa.

53 Halafu majuma machache yaliyopita, wakati mimi na mke wangu tulipokuwa madukani katika kijiji chetu kidogo huko nyumbani, tulisikia bila kukusudia mazungumzo ya wasichana wawili wakizungumza. Na mmoja wao akasema, “Vema, ulimnunulia nini mama kwa ajili ya Krismasi?”

54 “Loo,” akasema, “mpenzi, nisingeweza kuwazia juu ya kitu kingine chochote kumnunulia. Lakini kile angalifurahia zaidi kilikuwa ni pakiti ya. . .ama katoni ya sigara na *ndicho nilichowazia*, kwa ajili ya mama.” Kisha akasema, “Nilimnunulia baba kisaga cha wiski.” Kisha kasema, “Unajua wakati . . . ”

55 Naye akasema, “Vema, ninafurahi ulifanya hivyo, mpenzi, kwa sababu nilimnunulia kibao kipya cha kuchezea karata, unaona.”

56 Mnaona, hiyo ndiyo Krismasi. Mnaona? Ulimwengu unawezaje kusimama muda mrefu zaidi, sherehe? Halafu ninadhani wanadhani ya kwamba hivyo ndivyo inavyofaa kufanywa. Unaona? Hivyo ndivyo wanavyotaka kufanya. Lakini wanadhania tu jambo hilo. Unaona?

57 Na hii hapa ya Mwaka Mpya inakuja. Baada ya Mwaka Mpya kuja, mbona, kwa kawaida watu wote wana karamu kuu ya Mwaka Mpya. Na halafu katika karamu hii ya Mwaka Mpya, wote wanaingia katika ulevi mkubwa mno kwenye usiku wa manane. Na nawazia wanaua dhambi zao, kuzisahau zote, yale waliyofanya katika mwaka huo. Wanalewa sana hata wanasahau yahusuyo dhambi zao zote. Nami nafikiri wanadhani hivyo ndivyo unavyoondoa dhambi. Lakini wanakosea. Hilo

linasababisha tu dhambi zaidi. Huwezi kutatua jambo lolote kwa kufanya kosa lingine. Kwa hiyo ni kudhania tu, kuzamisha.

58 Sijui yale watu wanayofikiria, ya kwamba, wakati, na anasa ya kunywa pombe, ambayo wanaita anasa. Wakati wiski inapoingia katika mfumo, inachemsha damu hivi kwamba inavuruga akili, ubongo, nawe unakuwa tupu. Ubongo wako umechafuliwa sana mpaka, kwa joto la pombe hii katika mkondo wa damu, ndivyo wanavyosema madaktari, hivi kwamba kwa namna fulani inaufanya ubongo wako kuwa mtupu.

59 Mbona, kama kulikuwa na ugonjwa fulani mwilini mwako ambao ungeliufanya ubongo wako kuwa mtupu, ungetafuta kila ofisi ya daktari mjini, kupata kitu cha kuuondoa. Na hata hivyo, watu wanasherehekea siku ya kuzaliwa kwa Kristo, na kujaribu kunyamazisha majonzi yao, kwa kufanya bongo lao tupu. Hivi hutambui, rafiki yangu, ya kwamba, watu, inakubidi kukabiliana na jambo hilo kwenye Siku ya Hukumu? Huwezi kuepuka hilo. Lakini wanadhani hiyo ndiyo desturi ya kawaida hapa katika taifa hili, ni kufanya ubongo wako mtupu kwenye usiku wa mkesha wa Krismasi, ama mkesha wa Mwaka Mpya, kufanya bongo lako tupu kwa kunywa pombe.

60 Wanaiita, "Ma—maskini burudani ndogo safi. Anasa ndogo ambayo watu wanapaswa kuwa nayo, kujiburudisha." Vema, kama hiyo ndiyo raha yote ambayo mtu aliwahi kupata maishani, ingekuwa ni raha ya jinsi gani? Kufanya ubongo wako mtupu sana hivi kwamba hata hujui yale unayofanya, kisha unaiita raha.

61 Sasa, ningeweza kuona watu wa ulimwengu wakifanya hivyo. Lakini inapofikia kanisa kufanya jambo hilo, watu wanaojiita Wakristo, basi inaonyesha ya kwamba kumekuwako na kupotoka mahali fulani, maana hivyo sivyo unavyosahau dhambi. Ziko kwenye Kitabu cha Mungu. Na jinsi tu zinavyoweza kuondolewa, ni kuwekwa katika Bahari ya Usahaulifu, Damu ya Yesu Kristo, halafu zisikumbukwe dhidi yako tena. Hiyo ndiyo njia ya pekee. Lakini wanadhani ya kwamba njia nzuri ni kulifanya kwa njia ya kawaida, jinsi watu wanavyofanya jambo hilo.

62 Pia tuna wahubiri wa madhehebu, madhehebu makubwa kote nchini, na wahudumu hawa wanahubiri fundisho la dhehebu lao, wakidhani ya kwamba wanafanya yaliyo sawa kabisa. Wengi wao, haidhuru jambo ni kinyume jinsi gani na Maandiko, wanadhani wanafanya vema wanapohubiri fundisho hilo, hata liwe ni la jinsi gani. Wanadhani ya kwamba hilo ndilo tu Mungu analohitaji: kanuni fulani ya imani, ama uanachama fulani. Wanadhani ya kwamba hayo ndiyo yote tu Mungu anayohitaji. Wanadhani ya kwamba wanawapeleka watu Mbinguni kwa kujiunga tu na kanisa fulani na kuhubiri kanuni ya imani. Wanadhani ya kwamba hilo ni sawa, hilo tu ndilo

unalopaswa kufanya. Hilo ni kosa la jinsi gani! Hilo ni kosa baya sana, kudhania tu katika hilo.

63 Kuna kanuni moja tu ya imani katika Biblia: hiyo ni Kristo. Unaona? Inatupasa tu ku—kumjua Yeye, ni kujua, ni kupata Uzima. Nje ya hilo, hakuna njia ya kuelekea Uzimani, nje ya kumjua Kristo kwa tukio lako mwenyewe pamoja Naye, wala si kwa kujiunga na kanisa, wala kukariri kanuni ya imani. Na wakati tu tunapolileta kwenye hali hiyo duni, hiyo ndiyo sababu tuna karamu za Mwaka Mpya za ulevi kwa Wakristo, wanavyojiita. Hiyo ndiyo sababu tuna sherehe za Krismasi na za Mwaka Mpya, na siku zingine takatifu, na kadhalika.

64 Hiyo ndiyo sababu watu hufanya hivyo, ni kwa sababu hivyo ndivyo tu wanavyojua kufanya. Vema, hakika, kama kuna kitu kinachowafanya watu watake kufanya kitu siku hiyo, kunapaswa kuwe na kitu halisi cha kufanywa. Kuna jambo fulani mahali fulani ambalo ndilo jambo sahihi linalopaswa kufanywa, kama hilo ni jambo baya la kufanya. Kwa sababu, kunapaswa kuwe na jambo la kweli kwa kila kosa, la sivyo lingekuwa ni kweli. Kwa hiyo lazima kuwe na kweli na uongo, kukanusha na kuitikia.

65 Lazima kuwe na dola halisi ambayo dola ya bandia imenakiliwa kutokana na hiyo, la sivyo dola ya bandia ingekuwa ndiyo dola halisi. Na tunapoona dhe—dhe—dhehebu, ama ku—kundi la watu wanaoona njaa kwa ajili ya jambo fulani, nao wanaingia kanisani, na—na kujiunga na kanisa, wanaonyesha ya kwamba kuna kitu fulani wanachoonea njaa.

66 Nafsi ya mwanadamu hulilia kitu fulani. Inajua ya kwamba kuna kitu fulani kilichoileta hapa. Wao. . .Inajua ya kwamba kuna kitu fulani ambacho—ambacho ni zaidi ya mahali hapa. Wanajua ya kwamba wametoka kwenye usiku, nao wanarudi kwenye usiku. Nao wanataka kujua walikotoka, na mahali wanakoelekea. Sasa, kama njaa hiyo imo mle ndani, huwezi kuipata kwa kuiharibu akili yako.

67 Unajua, nilisikia mtu fulani aliyekuwa mkutanoni hapa, wakati fulani uliopita. Mtu fulani alisema, "Hebu achia akili yako iwe tupu tu sasa. Angalia tu moja kwa moja juu angani. Achia akili yako iwe tupu. Utapata tukio." Na hapana shaka utapata. Hiyo ni kweli. Lakini, unapata tukio, ila ni tukio gani? Unaona, unapofanya jambo hilo, unamfungulia tu Shetani nafsi yako. Atakupa kitu fulani. Hiyo ni kweli.

68 Lakini, nafikiri, mtu anapomjia Kristo anapaswa kuja na akili yake yote waliyo nayo, na wakinukuu niani mwao, wanapomjia Yeye, kila ahadi katika Maandiko. Weka akili yako macho, unapomjia Kristo. Usiache iwe tupu. Ibilisi atakufanya ufanye jambo lolote. Unaona? Watakupa mhemuko. Anaweza kufanya hivyo, pia. Lakini unataka tukio, jambo ambalo Biblia inafundisha, jambo ambalo ni halisi.

69 Halafu wanaondoka, wakidhania, “Vema, mtetemeko mdogo wa neva. Niliona nuru mbele yangu,” ama—ama kitu kama hicho. “Nilimpata.” Wala hawaishi tofauti kamwe. Wanatoka tu na kuendelea.

70 Wengi wao wanakuja na kusema, “Naam, ninakariri kanuni *hii* ya imani. Ninaamini ya kwamba niko sawa, sasa.” Sasa, unadhani uko sawa. Unafikiri tu uko sawa.

71 Sasa, wanapofanya jambo hili, ndipo watu wanakuja na kujiunga na kanisa hili, wakidhani ya kwamba wanafanya vema. Na wengi wao wanaombwa tu kuchukua ka—kanuni ya imani, kuishi kwayo. Wananyunyiziwa maji kidogo, na kuwafanya wafuasi wa kanisa, nao wako sawa, basi. Hao watu wanatoka, watu waaminifu, wazuri, wakidhani ya kwamba wanaelekea Mbinguni.

72 Sasa hapo ndipo shida inapoingilia. Watu wanaowazia vema wanaamini ya kwamba kama wakiingizwa katika hali fulani, ama mahali fulani, ama wakitoa ahadi fulani, ama kitu kama hicho, kwamba hayo tu ndiyo Mungu anayohitaji. Kutimiza amri, ama kuishi kwa zile amri kumi, ama kitu kama hicho, kufanya matendo mema, kazi za jamii, kumpa jirani kitu fulani. Wanadhani ya kwamba hiyo ndiyo dini, na hilo tu ndilo wanalopaswa kuwa nalo. Lakini hilo ni kosa kabisa.

73 Sasa tunaishi tumechelewa kuliko tunavyowazia. Mwaka baada ya mwaka, nikija Phoenix na mahali pengine, sijui kama tutakuwa hapa mwaka ujao. Nashangaa basi, ninapoondoka, “Je! nili. . .Nilikuwa mwaminifu? Niliweka kila kitu wazi nilivyojua kukiweka? Bwana, nilifuata maagizo Yako? Nilisema jambo moja kinyume cha Neno Lako, ama niliweka kila neno sawasawa kwenye Neno Lako? Kwa sababu, watu wawa hawa watasimama pamoja nami kwenye ile Hukumu, na itanibidi kutoa hesabu kwa yale nimesema nilipokuwa mahali hapa, mahali lilipo.”

74 Lakini watu, baada ya wahudumu hawa, ninaamini, kudhania, baada ya kupata elimu nyingi na digrii na kadhalika, na kujifunza kanuni ya imani ya kanisa fulani, na kurudi na kuchukua kazi ya uchungaji, na, ninaamini, kwa uaminifu na usafi wa moyo, kwa uaminifu tu kama mtu yeyote angeweza kuwa. Lakini uaminifu sio unaolifanya liwe kweli. Hilo, hilo kwa jumla si Kweli. Nimesimama wakati mimi . . .

75 Hapa si muda mrefu uliopita huko India, na kuwaona wakiwa na sanamu yenye rubi masikioni, yenye thamani ya maelfu ya dola, na uso wa kuchukiza sana ndani yake, na macho makubwa mno. Na kuwaona makuhani wakimimina maji matakatifu juu ya mtu fulani, huku mwili wake umejaa ndoana zikiwa na matone madogo ya maji yakining’inia kutoka kwake. Na—na nikawaona wakipitia kwenye handaki la moto, kama urefu wa yadi thelathini, labda upana wa futi kumi, na

kina cha futi kadhaa, miali tu myeupe ya moto, na kumwona mtu huyo akiwa na mateso haya yote. Na labda midomo yake, kama alikuwa amedanganya ama kufanya udanganyifu fulani, akifanya vitubio, anatoa ulimi wake na kuushonea puani mwake, na kuchoma mdomo wake wa juu kwa visu vidogo, vinatokea kwenye paji la uso wake hapa, na kutokeza namna *hiyo*. Kila aina ya vitu vya kutisha sana! Ndipo makuhani wanammwagia maji matakatifu, pia, nao wanachinja mbuzi hapo, kutoa dhabihu ya damu. Kutembea kupitia kwenye moto huo, wakidhani ya kwamba wanafanya mapenzi ya Mungu, nao ni waaminifu. Wao ni waaminifu.

76 Huko chini Afrika, unawaona wakiwachukua watoto wadogo, wadogo tu, wanene, watoto wachanga weusi, jamaa wadogo sana, na kuchukua. . . Mchawi angechukua visu na kuwakata, na kusugua huo wino wa forsadi nyusoni mwao, na kuwaumbua, na kuwahasi wasichana wadogo, na kadhalika, kuwafanya mabikira. Na kila namna ya mambo kama hayo, akiwa mwaminifu kabisa. Hakika, wanafanya hivyo. Wanasujudia vinyago, na hata wanatoa uhai wao kwa uaminifu sana. Lakini uaminifu haukidhi matakwa. Wanadhani hiyo ni sawa. Wanafikiri tu hayo ni sawa.

77 Nanyi, sisi tunawadharau, na tunafikiri wanapaswa kufundishwa vinginevyo. Lakini sisi hapa Marekani ni wabaya vivyo hivyo, na, kusema kweli, ni wabaya zaidi. Ni kweli. Tunadhania. Tunaona ni jambo la kawaida. Tunathubutu kila mahali bila mamlaka halisi ya kufanya jambo hilo. Hakuna ruhusa katika Biblia kwa Mkristo kunywa pombe, kucheza karata, kudanganya, kufanya karamu za ulevi.

78 Watu wanajiunga na makanisa haya na kuendelea vivyo hivyo. Wanajiunga na makanisa haya. Wanawake wanakata nywele zao, wanavaa kaptura, wanavuta sigara, hakika, wanaendelea moja kwa moja. Wanafikiri hayo ni sawa. Wanadhani ni sawa. Bali si sawa. Si sawa. Kwa maili milioni moja, si sawa. Neno la Mungu haliungi jambo hilo mkono. Ni kinyume chake, bali wao wanadhani ni sawa.

79 Mahali fulani hapa kwenye Pwani ya Magharibi. Sasa, hili si huko kwa Wapresbiteri sasa. Hili ni kwa Wapentekoste, na kanisa kubwa zuri, dhehebu zuri sana, bali wameenda mbali sana na Neno. Bibi huyu alikuwa na nywele ndefu. Alikuwa amezitengeneza kwa kitu kidogo cha duara nyuma ya kichwa chake. Na, wao, wangemwendea, waseme, “Aisee, gurudumu lako limetoboka, huku nyuma.” Wao. . . Na hao wote wakamdhihaki. Hata mchungaji alimwambia anapaswa kukata nywele zake kwa sababu zilikuwa ni tofauti.

Aliniuliza. Akasema, “Ndugu Branham, na hilo je?”

Nikasema, “Alikwambia jambo la makosa.”

Dada zetu wa Kipentekoste wanafanya jambo lile lile, kama walimwengu.

80 Mtu fulani alisema, hivi majuzi, kasema, “Ndugu Branham, watu wanakuthamini wewe kama nabii. Kwa nini sana sana huwafundishi watu hao jinsi ya kupata karama za kiroho? Uachane na vile hao wanawake wanavyovaa nguo na jinsi hao wanaume wanavyotenda. Achana nao. Si kazi yako kuyasema hayo. Wafundishe mambo makuu, ya kiroho, yenye kilindi.”

81 Nikasema, “Ninawezaje kuwafundisha aljebra, wakati hawajui ABC?” Unawezaje kuwapa elimu ya chuoni; hata hawajatoka kwenye shule ya chekechea? Hata hamna adabu ya kawaida kujisafisha na kutenda kama Wakristo, na kuvaa kama Wakristo, na kuishi kama Wakristo, na halafu kuzungumza juu ya karama za kiroho. Tokeni kwenye shule ya chekechea. Wanadhani hayo ni sawa, bali ni makosa. Hampaswi kufanya jambo hilo. Mama zenu hawakufanya jambo hilo, hilo lilikuwa katika miaka ya Kipentekoste. Bali wanalifanya.

82 Na ninyi wanaume, jinsi mnavyoishi, mnawaacha wake zenu kufanya hivyo? Mngali mko katika shule ya chekechea. Mnaona? Hiyo ni kweli. Mnadhani ni sawa, bali si sawa. Mnasema, “Vema, mke atafanya *hivi* na kufanya *vile*.” Wewe ndiwe kichwa cha nyumba. Mungu alisema hivyo. Naam.

83 Mnadhani tu ni sawa kwa sababu hao wengine wanafanya hivyo. Sijali yale hao wengine wanayofanya. Ni vile Neno la Mungu linavyosema. Huo ndio Ukweli.

84 Wanadhani tu. Mnaona? Mnasema, “Vema, ninakisia ni sawa, m—mchungaji.”

85 Sijali mchungaji anasema nini. Neno ni kweli. Neno ndilo lililo kweli. Mnaona? Msidhanie. Mtaingia katika matatizo. Fanyeni tu vile Neno linavyosema mfanye. Naam, bwana.

86 Watu, wana—wanaendelea kufanya jambo hilo vivyo hivyo, bali wanadhani ni sawa wakati si sawa.

87 Watu wanasema, “Vema, Yeye ni mwema sana. Yeye, Yeye ni mzuri sana asingeweza kufanya jambo hilo. Mungu ni mwema sana.”

Ninaamini hilo. Ninaamini Mungu ni mwema.

88 Mvulana mmoja tineja alisema, si muda mrefu uliopita, mjini kwetu, jiji letu. Yeye alisema, “Unajua nini?” Alisema, “Mungu ni mwema sana, Ndugu Branham.” Akasema, “Unajua, Mungu ni mwema sana, Yeye huniacha tu nifanye jambo lolote.” Akasema, “Yeye hajali. Hajali, maana Yeye ni mwema sana kwangu.” Upuuzi.

89 Mungu ni Mungu mwema. Tunasikia mengi sana kuhusu Yeye kuwa ni Mungu mwema, nami ninaamini ni Mungu mwema. Hiyo ni kweli. Yeye ni Mungu mwema. Lakini kama Yeye ni Mungu mwema, hana budi kuwa ni Mungu mwenye haki.

Yeye hawezi kutupa amri kufanya jambo fulani au jingine, nasi tusilitii na tutarajie kuepukana na Hukumu. Yeye pia ni Mungu wa hasira, Mungu wa hukumu. Hilo ndilo linalomfanya kuwa Mungu mwema, kwa sababu Yeye hutimiza Neno Lake. Hulilinda.

90 Kwa hiyo hatuwezi kutarajia kufanya makosa, mambo haya tunayoyafanya, na tukwepe. La. Tunaninii tu. . . .Yeye si ninii sana . . . Sivyo alivyo.

91 Yeye yu mwema. Hiyo ni kweli. Sitaki mnielewe vibaya. Lakini, Mungu ni Mungu mwema. Hiyo ni kweli kabisa.

92 Lakini, kumbukeni, jinsi tu anavyoweza kuwa mwema ni kuwa mwenye haki. Na endapo Yeye ni mwenye haki, hana budi kutimiza amri Zake Mwenyewe. Na kama Yeye hutimiza amri Zake, ni vibaya kwa Wakristo kukubaliana na ulimwengu. Ni kosa. Hatupaswi kufanya hivyo. Inatupasa kuwa watu tofauti.

93 Nasi tunajasiria tu, kudhania jambo bila mamlaka halisi. Neno la Mungu hutupa mamlaka, na hayo ndiyo mamlaka tunayopaswa kusimamia, ni yale Mungu aliyosema.

94 Hapa Israeli walidhani walikuwa wako sawa. Alikuwa ni Mungu mwema, pale mahali ambapo nimesoma hivi punde katika Hesabu. Alikuwa ni Mungu mwema. Alikuwa ameshuka akaenda Misri, na kuwatoa utumwani. Hakika. Alikuwa ni Mungu mwema. "Mbona, hata alitunyeshea ile—ile mana kutoka mbinguni." Mungu mwema, hakika. Ilikuwa ni vizuri sana.

95 Lakini basi ilipofikia wakati ambao Neno Lake lilikuwa litimizwe, ilipofikia Kadeshi-barnea, nao wapelelezi wakarudi wakiwa na ushahidi wa nchi ya huko ng'ambo, basi wao walidhani ya kwamba ingekuwa ni sawa kama wangevuka hilo. Mungu aliwakasirikia.

96 Ndipo Musa akasema, "Msiende kule juu pamoja na Waamaleki, kwa kuwa hamjatimiza yale Mungu aliyotwambia kufanya." Unaona?

97 Amri ilikuwa, "Nimewapa nchi hiyo. Nendeni, mkaitwae."

98 Nao wakarudi wakiwa na ushuhuda wake, lakini waliutilia shaka. Walitaka kurudi nyuma, na hasa warudi Misri, kuliko kwenda na kuiteka, kwa maana waliogopa.

99 Watu wengi sana wanaogopa leo, kwamba mtu fulani, jirani yako, atasema jambo fulani dhidi yako.

100 Mara nyingi mchungaji anaogopa kusema jambo fulani, kwamba, kuhusu Injili. "Ninahofu itamuudhi mtu fulani." Wanapaswa kuudhika. Anapaswa kuudhika.

101 Wakati mwingine wa—wa—wanawake wanahofu, wanasema, "Ndugu Branham . . . "

102 Ni kama tu maskini mtu huyu, mwanamke huyu alisema, "Ninahofu kuachilia . . . Kama sikukata nywele zangu, nanii wangu—mume wangu na hao wanawake wengine . . . "

103 Vema, ndugu, usiyadhanie mambo hayo. Chukua Neno la Mungu kuyahusu. Unajua una nafsi ambayo inapaswa kuokolewa? Je! unatambua mauti hayabadilishi nafsi hiyo? Mauti hayabadilishi jambo lolote ila makazi yake, vyovyote ilivyo wakati inapokuacha.

104 Tunaenda kwenye nyumba ya mazishi. Tunawasikitikia wa—watu waliokufa. Mara nyingine tunataka kuwazia mambo mazuri sana tuwezayo juu yao. Hilo ni sawa.

105 Lakini Yesu alitilia mkazo akasema, "Mtu asipozaliwa mara ya pili, hataingia kamwe." Kwa hiyo hakuna mstari nusu.

106 Unadhani alienda Mbinguni. Lakini, kulingana na Neno, hakuenda. Unaona, unadhani tu alienda. "Vema, alikuwa ni mfuasi mzuri wa kanisa. Alifanya mema kwa ajili ya majirani." Hilo ni jambo zuri. Tunaamini jambo hilo. Hilo ni jema. Hakuna la kusema dhidi ya sehemu hiyo.

107 Lakini je! ulitambua kile kilichowazuia watu kuingia katika ile nchi ya ahadi? Walikuwa waaminio wakwamia mpakani. Walienda umbali huo, bali wasingeenda mbele zaidi.

108 Hivyo ndivyo wanaume na wanawake, watu wanavyofanya siku hizi. Wataenda umbali fulani katika Mungu. Watasema, "Naam, nita—nitaamini. Nita—nitabatizwa. Nitafanya *hivi*, *vile*, ama *vinginevyo*, sheria zozote kanisa linazoweka." Lakini inapofikia kujisalimisha kila kitu kwa Kristo, maisha yako na kila kitu, hapo ndipo mstari ulipo.

109 Hilo ndilo linalowafanya watu kusema, "Vema, ninawaangalia hao wengine." Na hapa kwenu ninyi Wakristo wenye umri mkubwa zaidi, kwa walio wadogo. Wasichana wanawaangalia wanawake wenye umri mkubwa zaidi, vijana wanaume wanawaangalia wanaume wenye umri mkubwa zaidi, na kuona mienendo yenu, kuona yale mnayofanya. Nao wanadhani kwamba wao wako sawa, ni kwa sababu mnafanya jinsi mnavyofanya.

110 Sasa, kama kanisa la Kipentekoste kweli lingeishi kwa kanuni zake, kama lingeishi yale linayodai kuwa nayo, basi ulimwengu ungelilionea kiu. Lakini wanapoona kanisa la Kipentekoste likikwama, likiwa na mambo mengi vile vile, karibu, kama ulimwengu uliyo nayo, ndipo wanadhani wao ni wenye kukubalika tu kadiri mlivyo ninyi. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Wana haki ya kuwazia hivyo. Unaona? Lakini inatubidi kuondoka kwenye jambo hilo. Hatuwezi kulidhania. Tunapaswa kujiweka sawa na Neno. Kutumia . . .

111 Sasa karibu ni jambo lisilowezekana kuwafanya watu kuomba, kufunga, kumwita Bwana. Inaonekana kana kwamba

kanisa limesinzia sana, ni vivu katika siku hizi za mwisho, ni jambo la kusikitisha sana. Nami ninachukia kuja na kuendelea tu kuwachochea, na kuhubiri, na kusema mambo haya. Lakini, ndugu, dada, hiyo ni kweli. Kamwe siwezi kujizuia. Ni Injili, na haina budi kuhubiriwa. Haina budi kuhubiriwa kama ushahidi. Ni kweli.

112 Kwa hiyo ninafikiri tunadhania tu kupita kiasi. Tunadhania, kwa sababu tulikuwa na tukio fulani. "Miaka mitano iliyopita, Ndugu Branham, nilikuwa nikitembea barabarani, siku moja. Na Roho Mtakatifu alinibariki sana, nami nikatimua mbio barabarani. Ni—nikawazia, 'Bwana, huna budi kunipeleka mahali fulani, maana nitafanya yasiyofaa barabarani.'"

113 Labda ulitoka ukaenda kanisani, nawe ukapata tukio. Ukanena kwa lugha, na kuwazia, "Vema, hilo ni sawa. Ninaweza kuendelea sasa, na niko sawa, ninaona hao wengine wakifanya jambo *hili*." Unadhania tu jambo hilo.

114 Israeli walikuwa na matukio hayo. Israeli walikuwa wametoka Misri. Israeli walikuwa wameona ishara, na miujiza, na maajabu njia nzima safarini mwao. Walikuwa wamevuka Bahari ya Shamu, kana kwamba ni katika nchi kavu. Walikuwa wameona mana ikishuka kutoka mbinguni, kila usiku. Walikuwa wakishuhudia baraka za Mungu maishani mwao. Lakini baadaye wakapotoka, kutotii moja ya amri za Mungu, na ni jambo gani lililotukia? Baraka zilikatika kwao. Nao wakadhani ya kwamba kwa sababu Mungu alikuwa mwema sana, Yeye angeendelea tu, awe mwema, aendelee tu. Bali Mungu hawezi kufanya hivyo.

115 Nafikiri tumefikia mahali hapo. Tumekuja kwenye Kadeshi-barnea, ambapo sisi . . . wakati Mungu ametoa wito kwa ka—kanisa kusimama, na kuyarudia maisha ya maombi, kurudi kwenye kujitakasa, kurudi mahali ambapo tunajiweka wakfu mbali na mambo ya ulimwengu, na mbali na tofauti zetu ndogo ndogo miongoni mwetu; na—na—na kumrudia Mungu, na upendano wa ndugu, na unyenyekevu, kuzirudia nguvu za Mungu tena. Unaona? Tunaninii tu . . .

116 Sisi, tunadhania tu ya kwamba tunaendelea vizuri, kwa sababu Mungu anatubariki. Kwamba—kwamba, Yeye labda alikuwa akiwabariki Israeli siku ile ile waliyokataa kukwea kwenda kule na kuitwaa ile nchi ya ahadi. Siku ile ile waliyokataa kuamini, wale wapelelezi, mana ilianguka vile vile tu usiku huo. Lakini walikuwa kabisa nje ya mapenzi ya Bwana. Wasingeweza kushinda vita vingine mpaka waliporudi na—na kuweka mambo sawa na Mungu. Sasa ni ninii . . . Nafikiri wakati umewadia kwa Kanisa kumrudia Mungu tena. Kurudi na kuanza kama vile linavyopaswa kwenda, kusudi tupate kuendelea katika safari ye—yetu.

117 Hata hivyo, walijua ya kwamba Mungu alikuwa ni Mungu mwema. Alikuwa amejaa rehema. Alikuwa amewapa neema. Alikuwa amewaonyesha utukufu Wake. Jinsi ambavyo hapakuwapo. . .Hata viatu vyao havikuwa vikichakaa. Nguo zao hazikuwa zikichakaa. Na mana ilikuwa ikishuka kutoka mbinguni, kila usiku. Waliendelea kuona miujiza na ishara, za Uwepo wa Mungu akiwa pamoja nao. Hata hivyo, walidhani ya kwamba kwa sababu Mungu alikuwa amefanya mambo hayo, ya kwamba wangeweza wapande waende kule na kuutwaa mlima huo.

118 Hili hapa, wakati, kama tunataka karama za kiroho kanisani, kama tunataka nguvu za Mungu, na nguvu halisi za Mungu. Sasa, ninakuambia, ndugu, dada, ni rahisi sana kwa mtu kudanganywa na jambo hilo, mihemuko na kadhalika. Ibilisi anaweza kuiga karibu kila mhemuko alio nao Mungu. Unaona?

119 Lakini, unaona, kanisa letu halienendi jinsi linavyopaswa kwenda. Tunajua kuna kasoro. Mnaona? Na tunajua basi, ya kwamba Mungu hatakuwa pamoja nasi mpaka tutakaponinii, chochote kile, kujiweka sawa. Kwa hiyo ni wakati wa kujichunguza, tuone mambo tunayopaswa kufanya, na ni mambo gani tusiyopaswa kufanya, halafu tujiandae na kusonga mbele. Ni sawa, baraka.

120 Samsoni, vema, Samsoni alikuwa ni mtu mashuhuri. Alizaliwa Mnazarayo kwa Bwana. Alikuwa na vishungi vyake saba vya nywele vikining'inia mabegani mwake. Alithibitisha kwa ishara yake ya kwamba yeye alikuwa ni M—M—Mnazarayo kwa Bwana. Na Mungu alikuwa ni mwema, ingawa aliwatoroka wazazi wake, akashuka, na akaanza kubembana na mwanamke wa Kifilisti. Na hiyo ilikuwa ni kinyume cha mila, ama kinyume cha Israeli, kujipumbaza wakati wowote na Mfilisti. Lakini huyu hapa, akishuka kwenda kule. Mungu aliendelea tu kumrehemu; mambo yalikuwa sawa. Halafu akaninii . . .

121 Mwanamke huyo alijaribu kumbembeleza atoe siri yake. Badala ya kujitokeza mara moja na kumwambia asifanye jambo kama hilo, ya kwamba yeye alikuwa ni Mnazarayo kwa Bwana na asingemwambia, yeye alimwambia, kasema, "Ifunge mikono yangu." Akamdanganya. Mnaona? Naye Mungu akasamehe uongo wake. Ndipo akazikata zile kamba, na akaendelea zaidi na zaidi jinsi hiyo. Mpaka, hatimaye, wakati mmoja ambapo alidhani ya kwamba angeweza kufanya tu jambo lolote alilotaka kufanya, na awe yuko sawa.

122 Hiyo ndiyo shida, kudhani ya kwamba tunaweza kufanya jambo lolote na kuepuka. "Sisi ni Wapentekoste, mnaona, tunaweza kufanya jambo lolote na tubarikiwe." Hamwezi kufanya hivyo. Hamwezi kufanya hivyo.

123 Hatuwezi tu kuendelea kwa sababu sisi ni dhehebu kubwa. Tunamshukuru Bwana kwa ajili ya jambo hilo, kwa ajili

ya dhehebu kubwa. Hilo linathaminiwa. Lakini hatuwezi tu kuendelea, tuseme, "Tuna wafuasi wengi zaidi kuliko jamaa huyo mwingine, na kwa hiyo yeye hayuko kwenye shindano la mbio, nasi tunaweza tu kuendelea. Ninawaambia, tutaacha kufanya jambo *hili*, na kuacha kufanya jambo *lile*. Ninafikiri, vema, ninafikiri *hili* ni la mtindo wa kale. Sidhani inatupasa kufanya mikutano hiyo ya maombi, na mambo haya yote yanayoendelea. Nafikiri haitupasi kufanya hivyo." Unadhania tu.

124 Ninawaambia tena, badala ya kuhubiri, kuwapeleka wanafunzi wetu wengi huku, na kuwafanya washindiliwe theolojia tupu na mambo kama hayo, nafikiri ingefaa kuwapeleka kwenye chumba cha juu kama walivyokuwa wakifanya muda mrefu uliopita, wapate tukio.

125 Hudson Taylor alisema wakati mmoja, yule mmishenari mashuhuri wa India. Mvulana mmoja wa Kihindi aliongoka, naye akajazwa na Roho wa Mungu. Akasema uso wake ulikuwa uking'aa kama nu—nuru. Ndipo aliingia, kasema, "Bw. Taylor, sasa ninaamini nitaenda shuleni, na nichukue miaka yangu minne niliyokosa chuoni." Akasema, "Ndipo nafikiri nitasoma, na kupata Shahada yangu ya Sanaa, na katika miaka michache nitaweza ku—kutoka niende nikaihubiri Injili."

126 Bw. Taylor, akiwa Mkristo mashuhuri jinsi alivyokuwa, alisema, "Mwanangu, nenda na kile ulicho nacho sasa." Jambo ndilo hilo. Kasema, "Anza kutoa Mwanga wakati mshumaa umewashwa, si wakati umetumika nusu." Hiyo ni kweli. Tangaza yale unayojua. Usipokuwa na tukio, huwezi kutangaza chochote.

127 Lakini tunachohitaji ni—ni "kumrudia Mungu." Hiyo ni kweli. Mnaona, inabidi turudi kwenye lile tukio tena, kwenye kitu kinachotusafisha, ndani na nje. Kama ndani kukiwa sawa, nje kutajitegemea. Itachukua. . .Kutakaa sawa kwenyewe. A-ha. Naam, bwana.

128 Samsoni alisema, "Vema, nitainuka tu, na kujitikisa, kama tu vile nimefanya daima. Na halafu nikifanya hivyo, Mungu atakuwa yupo hapo. Ninadhani tu Yeye yuko." Lakini alikuta kwamba alikuwa ameondoka.

129 Mnajua nini? Ninaamini ya kwamba kanisa linapaswa kurudi kwenye utakatifu tena, linapaswa kuirudia njia sahihi ya kuishi. Unaona? Tunadhani basi, kwa sababu tunapokea Roho, kwa sababu tulicheza katika Roho, kwa sababu kwamba tumefanya mambo haya ambayo tumefanya, na Mungu ametubariki, na tumeona mikutano ya uponyaji, na tunaona miamsho, na kadhalika, tunawazia tu ya kwamba hilo ni sawa.

130 "Sasa, tunapofanya hivyo, tutajipanga, tutatulia, kwa sababu tuna jengo kubwa, tuna dhehebu zuri, tuna haya yote. Tuna tabaka la juu sana la *hili*, kanisa lililo bora sana jijini hapa,

na mambo haya yote, mpaka tunaweza kuingiza ulimwengu ndani na kusema, ‘Mnaona piano yetu, kinanda chetu, na *ninii* chetu, ni kizuri tu kama chenu. Na mabenchi ye—yetu ni, viti vya kanisa ni vizuri kama vyenu. Mhubiri wetu ana elimu ya juu sana kama wenu.’ Tunadhania ya kwamba Mungu angali yu pamoja nasi.” Wakati Yeye hayuko. Unaona? Inawabidi kukumbuka jambo hilo.

131 Tunapoanza kuona miujiza na ishara na maajabu ya Mungu, tunaona nguvu za Mungu zikishuka, halafu tunaona watu wakiishi tofauti, wakiyasafisha maisha yao. Hasira za msumeno, hasira kali, kugombana na kuzozana, na kupigana wenyewe kwa wenyewe, “wafuasi wako kwenye vurugu.” Eti hilo ni sawa, kila namna ya dhambi miongoni mwetu, kutokuamini.

132 Mtu fulani anahubiri Neno la Mungu, na kusema, “Mungu alisema huna budi kuzaliwa mara ya pili. Kama huwezi, hata huwezi kuingia.”

“Sikubaliani na jambo hilo.”

133 Nawe unasema ati una Roho Mtakatifu? Roho Mtakatifu hatakana Neno Lake Mwenyewe. Inambidi kudumu na Neno hilo, maana Yeye Ndiye aliyelinena. Kama nikisema neno, halafu nikane niliyosema, basi neno langu halifai kitu. Roho Mtakatifu hana budi kufuata aliyosema. Na Neno hili lililoandikwa *Hapa* ni Neno la Roho Mtakatifu. Ninaliamini. Hilo ni kweli. Sasa tunaona ya kwamba Mungu . . .

134 Tunahitaji, tunahitaji utakatifu zaidi. Tunahitaji kusafishwa, makanisa yetu.

135 Samsoni, aliwazia, “Vema, nita—nitaninii tu . . . ” Alishuka akaenda kule chini na kuishi na kahaba huyu, na kila kitu. “Hatimaye akaniambia nifanye *hivi*, na hatimaye nikaliepuka, halafu *haya* yote. Na, loo, kweli ni—nilimwambia ukweli, kwamba yote yanamaanisha hivi. Ilikuwa *hivi*, nami—nami nafikiri itakuwa ni sawa. Nadhani Yeye yuko pamoja nami.” Lakini wakati alipoamka na kujitikisa, alikuta kwamba nguvu zake zilikuwa zimemwacha.

136 Nafikiri leo, ndugu, tunapoangalia kila mahali kwenye makanisa yetu jinsi yanavyoendelea, ni wakati wa kujitikisa. Kuna kasoro fulani. Tunadhania ya kwamba tunaendelea vema. Tunadhani ya kwamba tunafanya vema.

137 Kama nilivyokuwa nikizungumza, si muda mrefu uliopita, na baadhi ya wafanyabiashara, ndugu zetu, nilisema katika mkutano fulani tuliokuwamo, huko kwenye nchi za ng’ambo. Na hao ndugu walikuwa kule, nao walikuwa na mkutano. Nao walikuwa wakishuhudia jinsi Bwana alivyokuwa amewabariki. Nao ati walikuwa na biashara ndogo pembeni, basi wakamtolea Kristo maisha yao, nao walikuwa na mlolongo wa makadilaki sasa.

138 Kwa hiyo nikawaambia hao ndugu, nikasema, “Msiseme hivyo. Hilo ni kinyume. Hivyo sivyo wale Wapentekoste wa kwanza walivyofanya. Walitoa waliyokuwa nayo na kuwapa maskini. Hao watu ni wafanyabiashara. Wana viwanda, na chochote kile. Inakupasa kuwapa kitu ambacho hawajui lolote kukihusu.”

139 Hiyo ndiyo shida ya kanisa. Tunapata taa zinazong’aa na kila kitu, na ninii. . .karibu makelele matupu kanisani. Tunajaribu kujilinganisha na ulimwengu. Kamwe huwezi kufanya jambo hilo. Inatupasa kuualika u—ulimwengu kwenye maeneo ya kanisa, si kwenda nje kwenye maeneo yao. Hatuwezi kujilinganisha nao kule. Lakini tuna kitu ambacho hawana. Hicho ndicho tunachotaka. Jambo ndilo hilo. Naam, bwana. Kitu tunachotaka kuwaonyesha ni Kristo maishani mwetu, nguvu za Roho Mtakatifu, mnaona, kuwaonyesha kitu ambacho hawana. Acheni waje kwenye maeneo yetu. Wakimtaka Kristo, waje kwenye eneo hili. Lakini msifanye kama wao na kutenda kama wao. Hilo ni kosa.

140 Hapo ndipo Samsoni alipofanya kosa. Alitoka Palestina, akashuka kwenye nchi ya Kifilisti. Aliondoka na ninii mba-. . . aliondoka kwenye maeneo yake. Naye hatimaye, wakati mmoja, akidhani ya kwamba Mungu alikuwa pamoja naye, na Mungu alikuwa amemwacha.

141 Akani, kisa, alichukua kabari hiyo ndogo na joho lile la Babeli, lo, aliwazia, alidhani halitaonekana kamwe. “Vema, ni kitu gani hicho? Maskini vazi dogo zee tu. Nitalishindilia *hapa* chini, na labda familia yangu italifurahia hilo kwa muda mrefu. Nina kabari. Kama wakati wowote tukiingia katika shida, basi nina ka—kabari ya dhahabu. Hakuna mtu atakayeiona. Nitakifunika kitu hiki pamoja na kukiweka chini ya koti langu na nisonge mbele.” Alidhani kwamba ilikuwa ni sawa, kudhania.

142 Lakini amri ya Mungu ilikuwa, “Msichukue kitu kutoka kwenye mji huo uliolaaniwa. Msiwe popote pale na kitu chochote kilicholaaniwa.”

143 Basi tunawezaje kuvuta sigara? Wanawake wanawezaje kukata nywele zao? Mungu anasema ya kwamba, wanapofanya hivyo, ni kosa? Mnawezaje kuvaa suruali hizi chafu za kitu wanachovaa? Wakati, Mungu alisema, “Mwanamke anayevaa vazi linalompasa mwanamume, ni chukizo machoni Pake.” Mungu habadiliki. Tunawezaje kufanya jambo hilo? Na ni kudhania tu kwamba ni sawa. Si sawa. Si sawa. Wanawake wetu wa Kipentekoste wanaofanya jambo kama hilo, afadhali muache na mjichunguze, mjitikise, mwangalie nyuma. Msiyadhanie mambo hayo, kwa maana mmekosea, mmekosea kabisa.

144 Wamisri, walipomfuata Musa pamoja na Israeli, walimwona Musa akiivuka hiyo bahari moja kwa moja, akivuka kule, kila

Mwisraeli. Walikuwa wametahiriwa na kuwekwa wakfu kwa Bwana. Wao, amri za Mungu zilikuwa pamoja nao. Ishara za Mungu zilikuwa zikiwafuata. Walitembea wakavuka bahari moja kwa moja. Hakukuwako na kosa. Wamisri walisimama wakawaangalia wakivuka.

"Vema," walisema, "Nadhani, kama wao wanaweza kufanya hivyo, sisi pia tunaweza."

145 Sasa, tunaangalia nyuma na kuona kanisa la Kipentekoste hapo mwanzo. Tunawazia juu ya Pentekoste, miaka thelathini, arobaini iliyopita. Tunawazia juu ya baraza la Pentekoste la baada ya Nikea. Tunawazia juu yao katika nyakati za mwanzoni za Irenio, Mtakatifu Martin, Columba, Justin, Polycarp, watu hao wote wacha Mungu. Nasi tunahisi kwamba, tukiwaona, ya kwamba tuna baraka ile ile waliyokuwa nayo, kwa hiyo tunaweza kuhisi ya kwamba tunaweza kwendelea moja kwa moja tu kama walivyofanya. Tunaona ya kwamba tunaweza kufanya mambo yale yale waliyofanya. Lakini hatuwezi kuyafanya chini ya hali hizi za mambo, chini ya hali hizi ambazo kanisa liko ndani yake sasa.

146 Angalia yale hao wanaume waliyofanya. Angalia yale hayo makanisa yaliyofanya. Ilikuwa ni kujitolea kwa jinsi gani! Yale yaliyowabidi kuacha! Jinsi walivyoyahesabu maisha yao kwamba hata si kitu kwao. Walidumu kulala kifudifudi, usiku na mchana, wakimwomba Bwana. Walienda kila mahali walipoweza, wakitafuta kila—kila ufa na kona wangeweza kuingia, wakishuhudia Ufalme wa Mungu, kwa watu.

147 Na, leo, tunamtarajia tu mchungaji kulileta kwenye mkoba wake, ama mwinjilisti, na, "Mungu abarikiwe! Mimi ni mfuasi wa kanisa." Jambo ndilo hilo. Mnaona? "Mimi ni mfuasi kule. Mimi ni ninii tu... Ninaamini katika kanisa hili. Hili, kanisa hili ni sawa." Hakika. Jengo linaweza kuwa ni sawa. Huenda kusiweko na jambo lolote baya, hakuna mchwa wala chochote kile ndani yake.

148 Lakini na hilo jengo je! hilo jengo lingine? Limepatwa na mchwa wa aina gani? Mnaona? Hilo ndilo jambo linaloweza kutuletea shida. Unaona? Mchwa watakula hadi ndani ya nafsi. Loo, jinsi itupasavyo kuchunguza na kuliona, kwanza, badala ya kudhani kwamba tuko sawa. Ndiyo. Naam.

149 Hao Wamisri wasiotahiriwa, waliwazia, "Tutapitia tu moja kwa moja baharini kama walivyofanya," nao wakayapoteza maisha yao.

150 Akani aliwazia, "Kabari hii ndogo na safi, haitaleta tofauti yoyote." "Hao wanawake wengine wanakata nywele zao. Nitafanya jambo lile lile. Haitaleta tofauti yoyote." Lakini ilifanya nini? Haikuleta furaha kwa familia yake. Ilisababisha mauti kwa kila mmoja wao.

151 Na wakati tunapopatana kwenye amri yoyote ya Mungu, kuwafurahisha watu, tunaua kitu kile papo hapo. Kabari moja ndogo na safi, vazi moja la Babeli, lilisimamisha jeshi lililokuwa likipiga hatua taratibu. Ndugu, jambo moja tunaloruhusu kanisa kufanya, ambalo ni kosa, jambo moja ambalo hatutalikemea, na kuwafanya watu walinyoshe, litazuia mwendo wa kanisa.

152 Wanadhani mnaendelea. Huenda ikawa tunaendelea, kwa jina. Huenda tunaendelea, kwa idadi. Hilo silo linalojalisha. Hilo silo linalojalisha.

153 Ni Mungu pamoja nasi, Mungu ndani yetu, Mungu akitenda kazi kupitia kwetu, Neno Lake likiwa hai ndani yetu.

154 Usidhani ya kwamba unajua jambo hilo. Angalia jinsi linavyokufanya uishi, msimamo unaochukua kuhusu dhambi, jinsi ambavyo kila kitu. Mbona, unawazia juu ya Mungu mtakatifu. Je! ulipata kuwazia ya kwamba Huyo, utasimama Mbele Zake na kutoa hesabu kwa ajili ya Neno hili, na kwa ajili ya Kristo? Wakati, Mungu ni mtakatifu sana, akikaa huko katika Umilele, wakati majua milioni kumi yangekuwa madoa meusi mbele Zake. Mtakatifu sana, hivi kwamba, hata Malaika wanaonekana wachafu, mbele Zake. Malaika mbele Zake, wao ni wachafu.

155 Unatarajia wewe na mimi, pamoja na Neno Lake na Damu ya Mwanawe kutusafisha na dhambi, na kukiuka amri Zake moja kwa moja na kuingia moja kwa moja ulimwenguni, na kutarajia kusimama pale bila hatia, wakati ulijua vizuri kuliko kufanya hivyo?

156 Kanisa bora ujiweke sawa. Usininii, hebu na tusidhanie jambo hili, kwa sababu tu idadi kubwa kuliko tulivyokuwa, na tuko katika hali nzuri kifedha kuliko tulivyokuwa. Tuna majengo mazuri kuliko tuliyokuwa nayo. Tungevalia nguo nzuri kuliko tulizokuwa tukivaa. Tunatumia. . . Tuna magari mazuri zaidi kuliko tuliyokuwa nayo. Lakini, loo, ndugu, nashangaa kuhusu Kristo, Yuko pamoja nasi kiasi gani. Mnaona? Jambo ndilo hilo. Tunadhania tu. Naam, bwana.

157 Wasiotahiriwa wasingeweza kufanya jambo hilo. Hiyo ni kweli. Walikufa maji baharini.

158 Katika siku za Nuhu, wakati Nuhu alipokuwa akijenga mashua ile kubwa mno iliyokuwa itakabili dhoruba, vema, hapana shaka ila wafuasi wengi wa kanisa la siku hiyo walisema, "Ati, yule mlokole! Vipi kama kweli ikitukia? Vipi kama ikitukia? Vipi kama dhoruba ikitokea? Tutaingia kwenye mtumbwi *wetu* na kuelea. Mtumbwi wetu ni mzuri tu kama wao. Mtumbwi wetu utaelea kama wao, kama umeundwa na Mungu ama haujaundwa Naye."

159 Hiyo ndiyo sababu. . .?. . .watu wanafanya kama siku hizo. Wanasema, "Mimi ni mfuasi wa kanisa *hili*. Nilijiunga *hapa*. Hilo ni zuri tu kama lingine lile."

160 Vema, ndugu, kama sisi hatuko kwenye Neno, wala Neno halimo ndani yetu, tunadhania tu tuko sawa. Kumbukeni, wakati gharika ilipokuja, mtumbwi ulioundwa na Mungu ndio tu ulioelea. Walidhani wangekuwa sawa. Lakini kudhani ya kwamba wewe uko sawa, na kuwa sawa, ni tofauti. Unaona?

161 Mnasema, "Ndugu Branham, wewe ni kama unatufungia hapa nje kwenye tawi fulani mahali fulani. Sivyo?"

162 La. Ninataka tu kuwaonyesha kile kilicho mbele zenu. Unaona? Ndipo tutakuja kwenye kuokoa katika dakika moja. Naam.

163 Unasema, "Mbona, Nuhu. . ." Mtu fulani angesema, "Vema, hapa, nina. . .Vema, ninamjua John Doe, hapa chini pembeni. Mbona, yeye ana mtumbwi ambao tunaweza kuabiria mto wowote nao."

164 Lakini, unaona, haukuwa umeundwa na Mungu. Haukuwa umejengwa na mbao za mshita, na—na—na jinsi Mungu alivyouunda.

165 Unasema, "Nina kanisa, Ndugu Branham. Loo, sisi, sisi ni wafuasi wa dhehebu kubwa sana lililo ndani ya mji huu. Sisi, sisi ndio kanisa lililo kubwa sana hapa, na tuna kundi lililovalia vizuri sana la watu. Meya huja kanisani mwetu, na watu mashuhuri huja kanisani mwetu. Mbona, sisi, yote haya tunayo. Unaona?"

166 Lakini isipokuwa hilo liwe limeundwa na Mungu, halitasimama. Hakuna dhehebu, isipokuwa limeanga. . . limeundwa na uundaji wa Mungu hapa, ambalo halitasimama. Unaona? Hiyo ni kweli. Linapaswa kuja jinsi Mungu alivyosema liundwe. Haliwezi kuja kwa njia nyingine yoyote; si kwa kanuni ya imani, si kwa kujiunga, si kwa *hili*, wala si kwa mhemuko. Linapaswa kuja kwa njia ya msalaba. Linapaswa kuja kwa njia ya Damu. Linapaswa kuja na kujazwa na Roho Mtakatifu. Linapaswa kuwa ni la nyenzo za Roho Mtakatifu, na nyenzo za Roho Mtakatifu hufanya watu wa Roho Mtakatifu.

167 Mtumbwi wa mvinje huunda mtumbwi wa mvinje. Mpopla huunda mtumbwi wa mpopla. Mnaona ninalomaanisha? Na nyenzo za kilimwengu huunda kanisa la kilimwengu. Nyenzo za Roho Mtakatifu hufanya Kanisa la Roho Mtakatifu.

168 "Kanisa hili la Roho Mtakatifu ni nini, Ndugu Branham? Linatenda nini? Hutenda kazi namna gani?" Tutaona katika muda mfupi tu. Unaona? Vema.

169 Limeundwa, kama ilivyo sasa, wana—wanajaribu kuamini. Wengi sana, leo, wengi sana kote katika nyakati, wamezungumza juu ya jambo hilo, kuna njia nyingi sana mbalimbali,

kuwaambia, watu wengi sana wa njia mbalimbali. Ni mchafuko. Unaenda *hapa* . . .

170 Mama yangu mkongwe ambaye ndiyo kwanza aage dunia, miezi michache iliyopita, wakati alipokuwa amelala pale kitandani, alisema, "Billy, ninaondoka."

Nikasema, "Mama, usizungumze namna hiyo."

171 Akasema, "Ninaondoka." Kasema, "Ninataka kwenda kuwaona watoto wangu wengine. Ninataka kumwona baba. Ninaondoka." Naye akaangalia huko ng'ambo.

172 Nilikuwa nimesimama pale, kifungua mimba chake. Hapa alisimama dada yangu, kitinda mimba. Na sote tulikuwa watoto kumi; wavulana tisa na msichana mmoja.

173 Aliangalia, naye akasema, "Mwanangu wa kwanza na wa mwisho." Akasema, "Dolores, wewe ndiwe msichana wangu wa pekee. Ulikuwa mwema kwangu." Kasema, "Umekuja na kunisaidia kuosha nguo zangu. Ume—umenipenda na kunitunza."

174 Akasema, "Billy, umehakikisha ya kwamba sikupata njaa. Umelipa bili zangu. Umenipa mahali pa kuishi." Kisha kasema, "Umekuwa kiongozi wangu wa kiroho."

175 Nami nikasema, "Mama, miaka michache iliyopita, nilipokuja kwa Kristo, kama mvulana mdogo, baada ya kuitwa kama mtoto," nikasema, "kwanza, nikiwa Mwairishi, nilifikiri nitaenda huko kwenye kanisa la Kiairishi. Nao wakasema, 'Sisi ndio kanisa, haidhuru kitu kingine chochote kinasema nini. Sisi ndio kanisa.' Kisha wakasema, 'Hapa ndipo utakuja, inakupasa uje kwenye hili. Hili ndilo kanisa la pekee.'"

176 Ndipo nikasema, "Halafu niliwaza nitaenda kule na kulitembelea la Kilutheri. La Kilutheri likasema, 'Sisi, sisi ndio kanisa. Sisi ndio. Sisi ndio hilo.' Mwi-. . . Kanisa ni kundi la watu, kundi la watu lililoitwa. Nikawaza, 'Vema, sasa, ni lipi kati yao lililo ule Mwili? Ni lipi kati yao ambalo kweli ndilo Kanisa? Moja linasema liko *hivi*, na lingine linasema liko *vile*.' Nikaenda kwa Wamethodisti, wao wako *hivi*. Wabaptisti *hivi*."

177 Nikasema, "Nilikuta kwamba kuna kama makanisa mia tisa mbalimbali, unaona, kila moja likivuta upande *huu* na upande *ule*. Kama tu. . . " Nikasema, "Nisingeweza kuweka msingi wa imani juu ya hilo. Nisingeweza kufanya hivyo, mama. Kwa hiyo, sikuchukua yoyote ya hayo."

178 "Lakini nilirudi nyuma, na nikaona muundo ulivyokuwa, yale Mungu aliyoamuru; maagizo, hasa, maagizo yaliyofaa kutekelezwa. Nami nikayafundisha jinsi hasa mitume walivyofundisha, nami nikapata matokeo yale yale." Nikasema, "Sasa, jambo ndilo Hilo. Unaona? Ndilo hilo. Nilichukua Neno la Mungu na nikaliweka tu namna hiyo."

Naye akasema, "Billy, ninategemea jambo hilo."

179 Na wakati maskini mama huyo asingeweza kuzungumza tena, nikasema, "Mama." Ninataka kuiweka nafsi yake kwa Mungu. Niliiweka, ya baba yangu. Nami ninataka kuiweka nafsi yake kwa Mungu, naye alikuwa amelala pale. Asingeweza kuzungumza tena. Nikasema, "Mama, ningali nimesimama hapa bado. Unajua jambo hilo? Kama unaweza, pepesa macho yako." Naye angepepesa macho yake. Nikasema, "Ninataka kukuuliza jambo fulani sasa, mama. Uko umbali wa dakika chache tu sasa." Nikasema, "Ninataka kusimama hapa nione Yesu akija kuichukua nafsi yako." Nikasema, "Ndipo nitaikabidhi Kwake." Nikasema, "Ninataka kukuuliza jambo fulani, mama," nikasema.

180 Sasa, nilimbatiza mama yangu yapata miaka thelathini iliyopita. Naye alijazwa na Roho Mtakatifu. Na—naye alikuwa ni Mkristo, mtakatifu halisi wa Mungu.

181 Nami nikasema, "Mama, je! Yesu anamaanisha, papa hapa wakati labda una dakika tano zaidi za kuishi. Je! Yesu, ni mtamu tu kwako kama ile siku uliyompokea Roho Mtakatifu?" Nikasema, "Mama, ninataka kusema jambo hili kwa ajili yangu, ili kwamba niweze kuwaambia wengine. Je! Yeye ni mzuri jinsi ile ile sasa hivi? Wewe ni mama yangu. Usingeniambia jambo lolote la uongo. Ninataka kujua jinsi unavyojisikia sasa hivi. Je! Yeye ni mtamu tu kama alivyokuwa wakati ulipompokea huko nyuma, miaka thelathini iliyopita? Kama ndivyo, huwezi kuzungumza, lakini pepesa macho yako upesi sana." Naye angepepesa macho yake upesi sana, na machozi yakatiririka mashavuni mwake. Loo, ndugu! Naam.

182 Jambo ndilo hilo. Hudhanii basi. Unajua mahali unaposimama. Hiyo ni kweli. Loo, usidhani juu ya jambo hilo. Kuna njia nyingi sana tofauti. Usidhanie kabisa. Lakini Mungu ametoa thibitisho la ahadi Yake. Mnaona? Haitupasi kudhania hilo. Mungu amelithibitisha.

183 Sasa, katika Kumbukumbu la Torati 18:22, unaweza kupata, 18:15 hadi 22, utaona. Biblia ilisema ya kwamba, "Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii mithili yangu," Musa akizungumza. "Naye, watu. . .Mtu asiyemsikiliza Nabii huyu, atakatiliwa mbali na watu."

184 Kisha anaendelea na akasema, "Kukiwako na nabii miongoni mwenu, ama mtu anayedai kwamba ni nabii, na yale asemayo hayatimii, basi msimwogope. Sio kweli. Lakini kama Bwana amenena naye, Yeye atalitimiza." Mnaona? Hivyo ndivyo mtakavyojua jambo hilo. Mungu alitupa sisi maagizo jinsi ya kujua, ambapo haitubidi kudhania jambo lolote, lolote lile. Haikubidi kuwazia tu. Unaweza kupata tukio la kujua jambo hilo. Naam, bwana.

185 Katika Yohana 14:12, yule Nabii ambaye Mungu alimwinua, ambaye alikuwa ni Yesu Kristo, Mwanawe. Nabii yuyo huyo,

katika Yohana Mtakatifu 14:12, alisema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.” Ndugu, hakuna kudhania juu ya jambo hilo, hata kidogo. Alisema kwamba mtazifanya. Katika Marko, mlango wa 16, kutoka kifungu cha 15 hadi cha 18, Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.”

186 Huna haja ya kudhania, “Je! ninajiona mimi niko sahihi? Je! ni—ni—ninaweza kuwazia niko sahihi?”

187 Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Hukisii chochote kuhusu jambo hilo.

188 Yohana Mbatizaji, haikumlazimu kudhania, kusema, “Nadhani labda yule ndiye Kristo. Sina hakika. Sasa, huenda yule anayesimama pale Ndiye. Ninadhani labda ndiye.” Hakusema hivyo. Yeye alisema, “Tazameni, yule pale Mwana-Kondoo wa Mungu amesimama.” Hakuwa akidhani Ndiye. Alijua Ndiye. Kwa nini?

189 Mungu alikuwa amemwambia, huko nyikani, “Sasa, hutadanganyika kwa jambo hili, Yohana. Hili ni jambo muhimu. Hutaki mambo yako yavurugwe.”

190 Hivyo ndivyo ilivyo leo. Mungu anataka Kanisa Lake lijue Kweli. Hatutaki kuchanganyikiwa katika jambo hili. Ndugu, hupati jaribio lingine. Afadhali uwe sawa, wakati meli inapoingia nyumbani mwako, wakati mauti yanaelea chumbani. Inakupasa kuwa na hakika ya jambo hili. Usibahatishe juu yake. Usifanye jambo hilo. Ni makosa. Hakikisha uko sawa.

191 Yeye alimwambia Yohana, “Mtu utakayemwona akishukiwa na Roho, Huyo Ndiye atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa Moto. Unaona? Huyo Ndiye. Huyo atakuwa Ndiye.”

192 Yohana hakusema, “Ninalidhania.” Alisema, “Yule pale.” Ee, Mungu. Jambo ndilo hilo. Mjue Yeye. Hakudhania jambo lolote. Alijua huyo alikuwa ni Mwana wa Mungu. Alijua Huyo alikuwa Ndiye Mwana-Kondoo aliyekuwa akiichukua dhambi ya ulimwengu, kwa kuwa lilifunuliwa kwake.

193 Wala wewe hutajua vizuri zaidi mpaka litakapofunuliwa kwako. Na Mungu anawezaje kukufunulia jambo ambalo ni kinyume na Neno Lake? Jinsi tu Roho Mtakatifu atakavyoweza kujifunua Mwenywe kwako ni wakati anapotimiza ahadi Yake kwako. “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Jina Langu, watatoa pepo. Watasema kwa lugha mpya. Watashika nyoka, ama kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru. Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya. Hivyo watu wote watatambua, ya kwamba ninyi ni wanafunzi Wangu, mkipendana ninyi kwa nyinyi.”

194 Hizi ndizo amri. Haya ndiyo mambo ya kuangaliwa. Matunda ya Roho: upendo, furaha, amani, uvumilivu, imani, wema, upole, utu wema, subira. Hilo ndilo tunda la Roho. Hayo

ndiyo mambo, ushahidi. Hilo ndilo thibitisho. Hivyo ndivyo Mungu anavyothibitisha jambo hilo. Analithibitisha kwako.

195 Tofauti ilikuwa ni nini katika Moabu, huko mlimani, akiwa na madhabahu saba na kondoo waume saba; na Israeli huko chini bondeni, wakiwa na madhabahu saba na kondoo waume saba? Wote wawili wakitimiza amri za Mungu. Wote wawili wakijaribu kufanya hivyo. Lakini Mungu aliwathibitisha Israeli.

196 Kaini alifanya nini, wakati alipotengeneza madhabahu nzuri vile vile, ama nzuri kuliko ya Habili? Alitoa matunda. Alitoa fungu lake la kumi. Alileta mapato yake katika nyumba ya Bwana. Alipiga magoti madhabahuni. Alisujudia. Aliomba. Aliabudu, kwa uaminifu tu kama mtu yeyote yule. Lakini Mungu alimthibitisha Habili kwa kuteketeza dhabihu yake.

197 Juu ya Mlima Kameli, ile siku kuu wakati makuhani mia nne wa kikafiri walipokuwa wamekusanyika huko nje, ya nyumba ya mke wa mfalme nchini, walipokusanyika kule kutoa dhabihu yao. Waliita, siku nzima, wala hapakuwapo na sauti yoyote wala moto. Lakini wakati Eliya alipomweka huyo fahali hapo juu, na kummwagia mitungi saba ya maji juu yake, Mungu alithibitisha ya kwamba hiyo ilikuwa ni kweli.

198 Kama ukisema wewe ni mwaminio, Mungu huthibitisha jambo hilo. Haikubidi kudhania jambo lolote. Ni Mungu, kuteketeza. Haikubidi kudhania. Hiyo ni kweli. Madhabahu ya shaba yaliiteketeza dhabihu. Kama dhabihu iliwekwa madhabahuni, nayo haikuteketezwa, Mungu aliikataa. Mnaona? Ni kuteketezwa. Nawe ni dhabihu ya Mungu. Jiweke juu ya madhabahu, useme, "Mungu, yaondoe tu yote ndani yangu. Nifanye tupu, upate kunijaza, ukanitumie." Hiyo ni kweli. Usidhanie jambo hilo. Liamini. Naam, bwana. Kama huliamini, wewe, Mungu hataipokea dhabihu yako.

199 Yeye angeweza kusema, Yohana alisema, "*Huyu* ndiye. Yeye, Yeye ni wa kweli. Ninajua kwamba ni Yeye."

200 Nathanaeli alirudi kwenye Kumbukumbu la Torati 18. Nanyi mnaona, Kumbukumbu la Torati 18:15, kama mkitaka kuandika. Haikumbidi kudhania. Wakati Filipo alipoenda huko na kumpata, alisema, "Njoo, uone. Tumemwona Masihi."

201 Sasa, unaona, Filipo alikuwa na hakika. Alijua kile alichokuwa akizungumzia. Alisema, "Tumemwona Masihi." Sio "Njoo, hebu na twende hapa tuone. Hebu—hebu tushauriane, tuone kama huyu angeweza kuwa ndiye Masihi. Hebu mimi na wewe tuchukue vitabu vyetu tushuke twende tukaone." Haikuwa ni kushauriana naye. Hakuwa akidhani ilikuwa ni Masihi. Alijua Ndiye. Alijua Ndiye.

202 Kwa hiyo, Nathanaeli, akiwa ni mwanazuoni mzuri, wakati alipoenda pale mbele ya Yesu, na Yesu akasema, "Tazama

Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake," kudhania kwake kulikwisha.

Kasema, "Rabi, ulinijua lini?"

203 Akasema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya ule mti." Hakuna kudhania tena. Kitu gani? Alijua ya kwamba Mungu alikuwa amesema jambo hilo.

204 Mungu alikuwa amesema, "Kama akitokea nabii, mmoja miongoni mwenu, na yale asemayo hayatimii, basi msimsikie. Lakini yakitimia, nimemtuma." Haya basi. Haikumbidi kudhania. Alijua huyo alikuwa ni Masihi.

205 Mwangalie yule mwanamke pale kisimani, wakati Yesu alipokuwa huko nje kwenye kisima kule Samaria, wakati Yeye, yule mwanamke alikuwa amesimama pale kisimani. Akasema . . . Mnajua hadithi hiyo, kuhusu, "Nipe maji ninywe." Naye akasema, "Kisima ni kirefu nawe huna kitu cha kuchotea," na kadhalika, ninii . . . wakati mazungumzo yakiendelea.

206 Na hatimaye akamwambia, kasema, "Nenda kamlete mumeo uje naye hapa."

207 Naye akasema, "Sina mume." Akasema, "Bwana, naona ya kuwa u nabii," baada ya kumwambia. Kasema, "Sina mume," akasema.

208 Ndipo basi akasema, "Umesema vema, kwa maana umekuwa na watano, naye unayeishi naye sasa siye mume wako."

Akasema, "Bwana, naona ya kuwa u nabii. Tunajua."

209 Si, "Tunadhani, tunadhani kuwa labda . . . Sisi, tunadhani, labda, ya kwamba huenda Masihi akafanya jambo hili. Tunadhani."

210 "Tunajua ya kwamba Masihi ajapo . . . " Haleluya! Jambo ndilo hilo. "Tunajua. Hatudhanii lolote. Tunajua vile hasa Maandiko yasemavyo."

211 Ndugu, Maandiko yalisema hatuna budi kuzaliwa mara ya pili. Inatubidi kujitenga na uchafu wote wa ulimwengu na kuwa watakatifu. Hatuna—hatuna budi kufanya hivyo. Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema. Wanawake wetu hawapaswi kutenda kama ulimwengu unavyotenda. Wanaume wetu hawapaswi kutenda kama ulimwengu. Haitupasi kusimama mahali fulani, kuambiana mizaha michafu mmoja kwa mwingine. Haitupasi kutoka kwenda hapa nje na kuvuta sigara, kunywa pombe, tupate kudumisha kazi yetu.

212 Vema, kama ilinibidi ku—kula biskuti ya magadi, na kunywa maji ya matawi ya miti, afadhali nife kwa njaa mtaani, kuliko kung'ang'ania kazi ambako ilinibidi kunywa mwozo wa ibilisi na kuvuta sigara, chochote kile, kupendelewa. La, bwana.

213 Afadhali nijitenge na kundi la watu wanaojiita Wakristo watakaoniita wa mtindo wa kale, kama nilikuwa mwanamke,

maana ingenibidi kuwa—kuwa na nywele ndefu na nguo nzuri. Afadhali nijitenge na niwe mlokole, kuliko kushirikiana na watu kama hao ambao wangecheka na kufanyia mzaha mambo kama hayo. Lo, ni chukizo mbele za Mungu! Ni kweli.

214 Lakini, hata hivyo, tunajaribu kusema, "Jambo ndilo hilo tu." Tunadhani hilo ni sawa. "Hao wengine wanafanya hivyo." Lo, hilo halileti ninii yoyote. . . Yuda alimsaliti Kristo. Je! hiyo ni ishara ya kwamba inakubidi kumsaliti? La, bwana. Hatutaki kufanya hivyo.

215 Unataka kuninii, unataka kudumu na Neno la Mungu. Usidhanie jambo lolote. Chukua yale Neno la Mungu lisemayo. Naam, bwana.

216 Vipi kama wanafunzi, sasa, kwenye Siku ya Pentekoste. . . (Tunafunga.) Vipi kama wanafunzi walisema, "Tulipanda tukaenda huko," nao wa—walikuwa huko kwa muda wa siku tisa? Kwenye siku ya tisa, vipi kama Petro alikuja, akasema, "Ndugu zangu, mnajua Bwana wetu hawezi kusema uongo. Hasha. Hawezi kusema uongo."

Mathayo angesema, "Hiyo, hiyo ni kweli, Simoni. Yeye, Yeye hawezi kusema uongo."

Unaonaje, Marko?"

"Loo, hiyo ni kweli. Yeye hawezi kusema uongo."

217 "Alitwambia kama tungekuja hapa kwenye mji wa Yerusalemu na kungojea, Yeye angetuma ahadi ya Baba juu yetu. Tunaamini jambo hilo. Sivyo, ndugu zangu?"

"Loo, hakika."

218 "Sasa hebu niwaambieni jambo. Tumekuwa hapa siku tisa. Nadhani tumeipokea tayari." Loo, hilo linawafanya Wabaptisti wazuri, na Wamethodisti, na Wapresbiteri. Mnaona? "Nadhani tumeipata, ndugu. Hebu tutoke nje na kuanza mkutano."

219 Wasingeipata kamwe. Lakini hawakukisia lolote. Kwa nini? Walijua ya kwamba huku katika Maandiko. . . Nitawapa Maandiko machache katika dakika moja, mara nikiyafungua.

220 Katika Isaya 28:11, Yeye alisema, "Amri juu ya amri; kanuni juu ya kanuni juu ya kanuni; hapa kidogo na pale kidogo." "Shikilia yaliyo mema." "Kwa kuwa kwa midomo ya watu wageni na kwa lugha nyingine nitasema na watu hawa. Hii ndiyo raha."

221 Yoeli 2:28 ilisema, "Itakuwa katika siku za mwisho, nitaimwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili. Wana wenu na binti zenu watatabiri." Haleluya! Walingojea mpaka Maandiko yakadhihirishwa kwao. Hawakukisia lolote. Walingojea mpaka ikaisha. Walingojea mpaka wakaipata.

222 Kanisa la Kipentekoste, wanawake wao wangali wanakata nywele zao, wanaume wao wangali wanavuta sigara, na mambo

tunayofanya, na mambo kama hayo, na—na kuwaacha watu wetu kuendelea namna hiyo. Tunadhania jambo fulani. Hebu na turudi, ndugu. Hebu turudi hapa kwa dakika moja tu. Tunajitanguliza. Hatuwezi kuwa Wapentekoste na kufanya namna hiyo. La, bwana.

223 Hebu na turudi nyuma mpaka Moto wa Mungu uteketezao utakaposhuka, na kuipokea dhabihu, ulifanye Kanisa lijazwe kabisa na Roho wa Mungu, na nguvu za Kipentekoste za mtindo wa kale zianze kujidhihirisha zenyewe kanisani tena. Hakika. Hakika.

224 Tunadhania tu jambo hilo. Unaona? Tunalichukua tu, "Vema, naam, bwana, ninaamini. Nilinena kwa lugha siku moja. Ninaamini niliipokea, Ndugu Branham. Ni—ninaamini hilo ni kweli." Na unatenda jinsi unavyotenda? Unafanya mambo unayofanya? Kushirikiana na ulimwengu? Kuangalia televisheni Jumatano usiku badala ya kwenda kwenye mkutano wa maombi? Mambo haya yote, unayapenda, "Tunampenda Sucy," na hayo mambo mengine yote, kuliko unavyoipenda Biblia? Unatangulia kusoma magazeti? Ati Wapentekoste wanatangulia kuyasoma magazeti? Maana, wanawake hao wengine wanatenda hivyo, wewe unapaswa kutenda hivyo, pia? Kufanya aina hizi zote za mambo, hivyo basi unadhania tu.

225 "Yeye aipendaye dunia, ama mambo yaliyo katika dunia, kupenda Mungu hata hakumo ndani yake." Hilo ni sawa. Ni kweli.

226 Inafikia mahali ambapo yote ni maonyesho. Yote ni maonyesho tu, badala ya utakatifu wa mtindo wa kale, badala ya kumrudia Mungu. Mnaona picha za siku hizi za matangazo, na wainjilisti wakitoka, na nywele nzuri sana, za kipilipili. Ningependa kuwa na kama hizo. Hiyo ni kweli. Lakini mnawaona. Watapiga picha zao, hata hivyo, wanashikilia—wanaelekeza kichwa chao upande mmoja, wapate kuonyesha hizo nywele nzuri sana, za kipilipili, kutangaza kule nje, na upuuzi kama huo.

227 Hebu niwaambie, ndugu. Si ajabu Roho wa Mungu ameondoka kwenye kitu hicho. Si ajabu tumerudi tukiwa baridi tu kama Wamethodisti ama Wabaptisti. Inatubidi kutoka kwenye jambo hili, ndugu, dada, la sivyo Mungu atatuangamiza. Hiyo ni kweli kabisa. Inatubidi turudi kwenye nguvu za Mungu, kwenye mikutano ya kale ya maombi na kutikiswa kwa Roho Mtakatifu, mpaka wanaume na wanawake waishi wakiwa watakatifu na waliotakaswa. Naam, bwana. Tutoe ulimwengu, na Hollywood yote, na nguo na kadhalika, kutoka kwenye kitu hicho. Jamani! Hiyo ni kweli, ndugu. Naam. Loo, jinsi dhambi ilivyo danganyifu sana! Jinsi ambavyo inanyemelea ndani kwa urahisi namna hiyo, na kuchukua vitu hivyo. Inakushika tu, na kukushikilia, na kuondoka nayo. Naam, bwana.

228 Wasomi, ninyi makanisa mara nyingi mkimpigia kura mchungaji wenu, ama vyovyote mnavyolifanya jambo hilo. Wanafanya hivyo kama makanisa ya Kibaptisti, na kadhalika, na Wapresbiteri, na Wamethodisti, na Wapentekoste, pia, hakika. Mnamtaka mchungaji wenu, mnajaribu kupata jamaa mashuhuri, msomi, ili mpate kumwambia jirani yenu hapa, "Unaona, jamaa yetu ana . . . Mchungaji we—wetu ana elimu ya chuoni." Mnaona? Sisi, ninyi, mtamchagua mtu kama huyo.

229 Kama nikitaka mtu wa kuwafundisha watoto wangu, kuwaacha chini ya mafunzo yake, na mambo kama hayo, na ndugu yangu, mama yangu, na mtu ambaye ninatarajia kukutana naye huko kwenye nchi nyingine, afadhali nimpate mtu ambaye hakujua ABC zake, inapofikia kwenye msimamo wa elimu. Afadhali angalimjua Kristo, hiyo ni kweli, kama Mwokozi. Naam, bwana. Kama angeweza kuhubiri, ama kusimama na kutoa mate na kila kitu, haingeleta tofauti yoyote kwangu. Kama alivaa ovaroli mimbarani, inaleta tofauti gani? Shida yake ni kwamba, tumekuwa wapenda nguo na mitindo kupita kiasi. Na Wapentekoste, tunaninii tu . . .

230 Ni sisi sote tu. Tuta—tutaangamizwa tu kama hatutafanya jambo lolote kuhusu jambo hili. Tunahitaji mikutano ya maombi. Tunahitaji kurudi kwenye nguvu za Mungu. Naam, bwana. Na ukisema tu jambo dogo kulihusu, "Loo, jamani, masalale!" Watu wanafikiri tu hilo ni baya sana. "Loo, jamani! Nisingemtaka kanisani mwangu, akisema mambo kama hayo." Aha! Unaona? Jambo ndilo hilo. Kuna shida gani?

231 Inaonyesha kuna jambo fulani baya humo ndani. *Hili* ni Neno la Mungu. *Hili* ni agizo Lake. Tunadhani ya kwamba tuko sawa, bali sijui, sijui yale Mungu anayosema juu ya jambo hilo. Naam, bwana. Naam, bwana. Naam, bwana. Hilo—hilo ni jambo baya sana kusema hivyo, lakini ni kweli. Naam, bwana.

232 Siku ya Pentekoste, walingojea mpaka wakapata mamlaka ya Kimaandiko. Hiyo ni kweli, kabla hawajadai chochote, walijua walikuwa nayo. Hawakusema—kusema, "Vema, ni—nilisikia mhemuko mdogo." Waliihisi, wakaiona, chochote kile. Walijua walikuwa nayo. Waliiona ikitenda kazi ndani yao, ikitenda kazi ndani yao, ikizungumza kupitia kwao, kila kitu. Ilikuwa pale. Haikuwabidi kudhania chochote. Ilikuwa pale, ikijielezea.

233 Na mtu, anapozaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu, ni jambo lile lile leo. Hudhanii.

234 "Ni—ninaamini tunampokea Roho Mtakatifu tunapoamini." La. Hamkumpokea. Hamumpo- . . . Wengine, mngeweza kumpokea. Lakini kwa sababu tu ati uliamini, kama Mungu hakukujaza na Roho Mtakatifu, basi Yeye hajakuthibitisha bado. Hujampata. Unaona? Hiyo ni kweli.

235 Usidhanie unaye. Kuwa na hakika na kitu hicho. Hutaki kubahatisha juu ya jambo hilo, la, maana utapotea. Usibahatishe tu. Kaa tu, nenda, kaa mpaka jambo hilo limetimizwa kwako. Leo tunachukua jambo hilo kwa kanuni ya imani ama kwa namna fulani ya mhemuko.

236 Nilimsikia mtu mmoja; kama nilivyokuwa nikisema hapo mwanzo wa ujumbe wangu. Hapa nyuma, siku chache zilizopita, nilikuwa mahali fulani, na baadhi yao walisema, "Sasa, inakubidi kuvaa joho la Eliya." Jamani, kuna majoho mengi zaidi mbalimbali, na—na kugusa, na kushika, na mihemuko, niliyopata kusikia maishani mwangu. Kasema, "Sasa, acha iwe tupu. Jifanye tupu. Rudisha kichwa chako nyuma." Watu wazuri, waaminifu. "Jifanye tupu. Usiwazie lolote. A—a—acha tu bongo lako liwe tupu kabisa sasa. Sasa sema, 'Ninamwamini Mungu. Loo, ninaamini utanipa jo—joho la Eliya.'"

237 Sitaki joho la Eliya. Ninataka Roho Mtakatifu. Ninataka kuja juu ya msingi wa Neno hili. Ninataka kuja nikiwa na maarifa. Unaona? Nami ninamjia Mungu, nikiamini Hilo. Siwezi kufunikwa na joho la Eliya. Ninataka kufunikwa na joho la haki ya Yesu Kristo, nivikwe haki Yake. Hakika. Hilo ndilo joho tunalotaka. Naam, bwana.

238 Sema basi, "Tunaye!" Sisi!" Nao watu wanaenda, wakiamini jambo hilo. Wanasema, "Vema, sasa nadhani ya kwamba ninaye. Nilikuwa na hisi ya ajabu, unaona. Ama, kwe—kweli nilimpata. Mimi, misisimko baridi ilipitia kote mwilini mwangu." Naam.

239 Baadhi yao walisema, "Vema, hata ilinifanya nilie." Nililia, kwenye mazishi ya mama yangu, lakini, hata hivyo, hilo halikuwa na uhusiano wowote na Huyo, Roho Mtakatifu.

240 Roho Mtakatifu ni nguvu za Mungu unazotumiwa, ndani ya moyo, kama shahidi wa Roho. Unazaliwa mara ya pili. Maisha yako yanasafishwa. Ulimwengu umekufa, na uvundo wake wote. Ni kama kitunguu saumu huko Misri, unaona, uko mbali sana nacho. Wewe ni kiumbe kipya katika Kristo Yesu. Mambo ya kale yamepita. Unakuwa mpya, kabisa, kiumbe kipya, umezaliwa kwa Roho. Naam, bwana. Viungo vyako vyote vya mwili wako vinamtii Roho Wake, nawe unatembea katika Roho Mtakatifu, wala huisikilizi sauti ya ulimwengu. Macho yako yameelekezwa kwenye mambo ya Mbinguni. Hapo, hapo—hapo ni wakati ambapo wewe kweli umeninii . . . Mungu anathibitisha ja—jambo hilo.

241 Lakini mradi tu ungali una ulimwengu, na unataka kusema, "Vema, wao wanafanya *hivi*, nao wanafanya *vile*. Ninadhani ya kwamba wamempata." Wao, huenda wanaye. Sijui wana kitu gani, bali silo Hili ninalozungumzia. Hiyo ni kweli kabisa. Maana, silo. Naam, bwana. Hilo—hilo ndilo jambo moja la kweli, maana linafaa. Naam, bwana.

242 Halafu je! unaweza kuwazia mtu aliye na Roho Mtakatifu na anakana sehemu ya Neno la Mungu, akichukua nusu Yake, akisema sehemu hiyo nyingine si nzuri? Unaona? “Kwa hiyo ninaamini mtu anapaswa kuishi, maisha mazuri sana. Lakini tunapofikia wakati wa kufikiria juu ya uponyaji wa Kiungu na jambo hili lote namna hiyo, na kuacha, na, loo, inatupasa kuwa *hivi*, *vile*, siamini jambo hilo.” A-ha.

243 Biblia ilisema hilo lingetukia. “Wenye mfano wa utauwa, bali wakikana nguvu zake.” Wanakana nusu ya Neno Lake na nguvu Zake zote. Hiyo ni kweli. Naam, bwana. Hiyo ni kweli. Halafu wanadhani ya kwamba wanaye. “Ni sawa.” Mnaona? Naam, bwana.

244 Mama mmoja, baadhi ya akina mama, walikutana na mmoja wa dada zetu akishuka kuja huku, naye alikuwa amepata ajali ndogo barabarani, ama aliharibu, alilipua plagi katika gari lake, ama kitu kama hicho. Na wanawake fulani, walimchukua, kutoka kwenye kanisa fulani. Na wakamwambia mahali alikotoka. Wakasema, “Loo, Bwana alituongoza hapa.” Kasema, “Umekosea. Pentekoste imekosea, unaona. Kwa hiyo sisi . . . ” Loo, laiti ningalikuwa pale! Nusu uchi!

245 Acha kudhania. Ngojea mpaka hasira yote imeondoka, ishara za Biblia za wokovu wako zinatenda kazi ndani yako.

246 Musa alidhania, bila ya wito halisi, ya kwamba Mungu hakika angewafunulia watu hao. Alikuwa akitoka kwenda kuiteka Misri kule chini. Alidhani ni wakati wa kufanya jambo hilo. Lakini alishindwa, na alishindwa vibaya, na akajisalimisha, akaacha wazo hilo lote, mpaka siku moja Mungu akakutana naye.

247 Wakati alipokutana na Mungu kwenye kijiti kilichowaka moto, a-ha, aliingia katika kijiti hicho, kijiti hicho kikamwingia. Ndipo palikuwa na tofauti. Hakudhania, “Sasa, sijui. Ninaamini nitamwua tu huyu Mmisri, nimfiche hapa chini katika mchanga, na—na hilo litatosha.” Hiyo ilikuwa ni kabari nyingine ya Akani, mnaona. Mnaona?

248 Lakini wakati Mungu alipozungumza naye, katika kijiti kilichowaka moto, na kweli akamwona Mungu, akawa na hakika na Mungu, na akajua ya kwamba Mungu alikuwako, na akamsikia akisema, “Hakika nitakuwa pamoja nawe,” huo ni—huo ni wito wa kibinafsi.

249 Mara nyingi watu wanaondoka na kusema, “Ninaamini niliitwa kuihubiri Injili.” Unaona? Mtu hapaswi kuhubiri Injili mpaka . . .

250 Sijali ana elimu nzuri namna gani, jinsi anavyoijua Biblia vizuri. Ibilisi anaijua vizuri kuliko yeyote wetu, hiyo ni kweli, bali hawezi kuiishia. Jambo ndilo hilo. Hawezi kuiishi. Unaona? Hapo tu ndipo unapompiku. Unaona? Huenda akaijua vizuri kama wewe unavyoijua, bali hawezi kuiishi kama vile wewe

unavyoweza. Kristo alikufa, upate kuiishi, unaona, wala kamwe hakumfia. Kwa hiyo sasa, mnaona, ninii . . .

251 Hakuna mhudumu aliye na haki zozote, haidhuru yeye ni mwerevu jinsi gani, anajua theolojia kiasi gani, na jinsi gani anavyoijua Biblia vizuri, hapaswi kupanda mimbarani, kuhubiri Injili, mpaka kwanza amekutana na Mungu. Si kudhania, ya kwamba, "Inanibidi kutoka niende. Nitapata ruzuku bora zaidi, na ninatumaini haitanibidi kufanya kazi mno." Umekosea hapo, ndugu, kama kweli wewe ni mhubiri. Naam. "Lakini nitaninii . . . Na watu watakuwa *hivi*. Nami nitapendwa na watu miongoni mwa ji—jirani mahali nilipo, na mambo kama hayo. Nami ninafikiri ndilo jambo zuri la kufanya." Hilo silo.

252 Wito wa Mungu ni jambo ambalo hudhanii. Ni jambo, tukio halisi, jambo fulani ambalo umezungumza uso kwa uso na Mungu, nawe unajua umeagizwa kwenda kufanya jambo hilo. "Hakika nitakuwa pamoja nawe." Hudhanii lolote. Unaamini jambo hilo tu. Naam. Usilidhanie.

253 Usidhanie kamwe, "Ninapiga mbio vema." Ngojea tukio binafsi, la Kikristo. Usidai una Roho Mtakatifu wakati unapojiona mwenyewe unachezacheza katika ulimwengu. Usifanye hivyo. Usifanye. Wewe, ingekuwa ni bora zaidi kwako kama ungesahau tu jambo hilo, unaona, kama ulisahau.

254 "Vema," unasema, "Ndugu Branham, ni—nilipata misisimko mwilini siku moja." Hilo—hilo—hilo—hilo huenda likawa ni sawa, pia. Unaona? Lakini unasema, "Vema, ni—nilicheza katika Roho. Huenda nilinena kwa lugha. Hu—hu—huenda nilifanya mambo haya." Hilo ni jambo zuri. Naam, bwana. Hilo ni sawa. Lakini kama maisha hayo hayajanyoka, kama ninyi wanaume mngali mnavuta sigara, mnafanya mizaha, mnakunywa pombe, mnadanganya, kuhadaa, si mwaminifu kwa jirani yako, hata si mwaminifu kwa familia yako, unaona, na unadai kuwa na Roho Mtakatifu, usitoe ushuhuda huo tena, ndugu.

255 Na ninyi wanawake ambao hamna adabu ya kawaida ya kuachilia nywele zenu zikue, kama vile Mungu alivyowaambia mfanye. Hiyo ni kweli. Biblia ilisema ya kwamba mwanamke atakayezikata nywele zake hakiheshimu kichwa chake, na, nanii wake, hamheshimu mume wake. Na ninyi ambao mtavaa mavazi haya machafu mafupi kama walimwengu wengine wanavyovaa, Biblia ilisema ya kwamba yeye ambaye . . . "Mwanamke atakayevaa vazi limpasalo mwanamume ni chukizo," mchafu mbele za Mungu. Halafu ati unadai kwamba una Roho Mtakatifu? Unadhani unaye. Lakini unapompata, Yeye hukusafisha, hiyo ni kweli, anakufanya tofauti.

256 Ninyi ambao mnadai mna Roho Mtakatifu, na ninyi mlio na nywele ndefu, na mnaovaa mavazi nadhifu, kila kitu namna hiyo. Na mtakaa nyumbani Jumatano usiku na kuangalia kipindi fulani, kipindi cha televisheni, badala ya kwenda kanisani

kwenye mkutano wa maombi, mnadhania mna Roho Mtakatifu. Kwa kuwa Roho Mtakatifu anapokuwa humo ndani, upendo wa Mungu unakubidiisha sana, mpaka huwezi kukaa mbali na watu. Unaona? Ninyi ambao inawabidi kulazimishwa kwenda kwenye maombi!

257 Vipi kama mke wangu, kama nilimwambia mke wangu... Na kama nikioa, nilikuwa nimeoa, nilimwambia mke wangu ya kwamba ni—nilimpenda, na hilo lilikuwa ni uongo? Na wakati ikifikia kwenye shindano la kuamua kweli, sisi, ni—ni upendo wa bandia. Mimi ni nanii tu... Mimi ni... Si kweli kabisa. Unaona?

258 Ni kama tu vile ungalijitia meno ya bandia, kama huna meno. Hilo, hilo ni sawa. Inakubidi uwe na kitu cha kutafunia, kwa hiyo unatia meno ya bandia. Hayo meno ni sawa, kibadala, mpaka u—utakapopata mengine. Lakini, hayo, hayo meno hayajaunganishwa na wewe. Hayajaunganishwa pale. Hayo ni sawa. Ni kibadala, bali hayajaunganishwa na wewe. Hayatakuja katika ufufuo, maana hayajaunganishwa pamoja na wewe. Hiyo ni kweli.

259 Kama ulikatwa mkono, uweke mkono wa bandia, ni kibadala cha kitu fulani. Unavaa glavu, na kwa hiyo—hiyo ni sawa. Ni sawa kabisa, unaona, kufanya hivyo, bali mkono huo wa bandia kamwe hautafufuliwa. Hakuna kitu cha kujitengenezea kitakachofufuliwa kamwe.

260 Wala na Mkristo wa bandia kamwe hatafufuka katika ufufuo. Hujaunganishwa na Kristo.

261 Na kama kweli humpendi mke wako kuliko mwanamke mwingine yeyote ulimwenguni, yeye si ninii, bado kuna kasoro fulani. Kama humpendi mume wako, kama unamchezea wala huishi maisha mazuri, kuna kasoro. Hiyo ni kweli. Hatakuwako. Hawatakuwako basi, katika ufufu-... Huenda ulikuwa umeolewa naye. Unaishi maisha mazuri kwake. Hilo ni jambo zuri. Ni—ninathamini jambo hilo. Unapaswa kufanya hivyo kama mama, kwa ajili ya watoto wako. Na ninyi wanaume kwa ajili ya wake zenu, hiyo ni kweli, mnapaswa kufanya hivyo, kuwa mwenye heshima. Lakini katika ufufuo, huyo hatakuwa ndiye.

262 Wewe, vile vile tu katika Kristo sasa, huna budi kuunganishwa, sehemu ya Kristo.

263 Si kitu fulani cha bandia, cha kuiga, "Ninaenda kanisani na kukariri Sifa na Imani ya Mitume, na kadhalika, nami ninaamini ninapiga mbio vizuri tu kama hao wengine." Ndugu, unadhania. Usichukue jambo hilo vivi hivi tu. Unatembea mahali ambapo kweli huna mamlaka ya kudai kuwa na Roho Mtakatifu. Huna mamlaka halisi.

264 Tulisema nini huku nyuma, Webster ilisema nini? Webster ilisema, "kuthubutu bila mamlaka halisi."

265 Unathubutu, ukisema, "Mimi ni mpentekoste," wakati huna tukio, na hujakuwa ukiishi yale maisha ya Kipentekoste. Unaona? Naam, bwana. Ati nini? Bila ya mamlaka halisi. Ama, kulichukua vivi hivi, "Nilinena kwa lugha, kwa hiyo nadhani nimempata."

266 Ninaamini katika kunena kwa lugha, pia. Lakini kama maisha hayakufuati, basi halikuwa linafaa kitu. Unaona? Hakika. Nimeona wachawi wakinena kwa lugha, na walozi wakiifasiri. Mnaona? Ninajua jambo hilo. Na nimeona watakatifu wakinena kwa lugha. Zilifasiriwa, pia. Lakini, unaona, inabidi iwe ni maisha. "Kwa matunda yao mtawatambua," kwamba ni maisha ya aina gani.

267 Tena angalia Ujumbe wetu wa Kipentekoste leo katika kuhubiri, na watu wetu wakiachilia daima. Hata mambo madogo ya kawaida, hata hawawezi kufikia kwenye msingi wa adabu ya kawaida. Basi tutadai vipi kwamba tuna Roho Mtakatifu? Wakati umewadia, ndugu. Si ajabu ulimwengu unasema hamna kile mnachodai kuwa nacho. Tunakidhania. Tunachukua jina la "pentekoste" bila kuishi Maisha ya pentekoste. Maisha ya pentekoste ni maisha yaliyowekwa wakfu yaliyojazwa na Roho Mtakatifu, yaliyokolea na maaminifu, mpaka hakuna mtu anayeweza kukuelekezea kidole. Hiyo ndiyo Pentekoste halisi. Loo, hivi sisi . . . Ati nini? Kwa nini ungetaka kuwa na kibadala? Kwa nini ibilisi akufanyie ujanja kwa kitu kama hicho?

268 Nilikuwa nikisoma hapa si muda mrefu uliopita, jinsi ambavyo ibilisi anaweza kumdanganya mtu kirahisi kwa kitu hicho. Nilikuwa nikisoma maisha ya Mtakatifu Martin. Wengi wenu mmeisoma hiyo, bila shaka, katika wa Nikea, Wazee wa Baada ya Baraza la Nikea, hasa, jinsi kwamba ambavyo Shetani alimjia, akiwa halisi sana, kwamba alimjia huyu Martin. Alikuwa amevaa taji nzuri kichwani mwake, inayopendeza macho, nywele zilizometameta, viatu vya dhahabu. Martin, alimshangaa sana, wakati alipoona ono la huyo amesimama pale. Akasema, "Hivi hunijui mimi, Martin? Mimi ni Kristo."

269 Martin alikuwa ni mtu aliyejazwa na Roho Mtakatifu, naye alikuwa amefanya yaliyo mema kweli. Mnaona? Hebu silikilizeni tu jambo hili.

Naye akasema, "Nikubali, Martin. Kwa nini unasimama, unasitasita?"

270 Martin akaangalia nyuma akasema—akasema, [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.], "Bwana wangu harudi amevaa taji kichwani Mwake. Watakatifu Wake watamvika taji." Mnaona? Maandiko; dumuni Nayo. Naam. Yeye alikuwa kwenye Neno.

271 Usiku mmoja, shuleni; mmoja wa wanafunzi wake, mhudumu, alikuwa na shule, nyumba ya watawa. Wengi wa ninii . . . Ambapo, wanawaita sasa wanafunzi na shule za Biblia. Lakini mmoja wa hao wanafunzi alianza kupata hali ya

kujigamba. Akasema, "Mimi ni mmoja wa manabii wa Agano la Kale. Ninyi nyote nisikilizeni."

272 Tuna jambo hilo siku hizi. "Nisikilizeni mimi." Nabii halisi kamwe hasemi kitu kama hicho, marafiki. Neno lake la mwisho, ndiye mtu wa mwisho kusema jambo hilo. Mnaona?

273 "Ninyi nyote nisikilizeni. Bwana amenipa mamlaka." Aliendelea kufanya hivyo. Ndugu halisi hawakumsikiliza kamwe, wala na askofu. Aliendelea tu, na hatimaye akasema, "Kwa sababu ninyi nyote hamjaniamini, ninatabiri. Usiku wa leo, Bwana Mungu atashuka na kunipa joho jeupe, kuketi miongoni mwenu. Mimi ni mmoja wa manabii wa Agano la Kale."

274 Hilo linasikika kwa namna fulani ni la kawaida siku hizi? Lichunguzeni sasa, endeleeni tu. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaona? Mtu fulani alisema, si muda mrefu uliopita, yaliandikwa kwenye gazeti, "Mungu alishuka, akamchukua akampeleka mbele ya Mungu Baba, na akawagusa Malaika wenye manyoya kwenye mabawa yao." Whiu! Vema.

275 Ndipo hii, usiku huo yapata usiku wa manane, kweli kulikuwa na nuru iliyokuja mahali pake. Na siku hizo walikuwa na nuru za tochi tu, nuru halisi, wakasikia watu wakinong'onezewa. Mara moja akatokea akiwa na joho jeupe. Kila mtu aliligusa, hawakuwa wameona kitu kama hicho. Kila mtu akamkaribia. Askofu akamkaribia, akaliangalia. Si hata ni kitambaa cha aina gani; lilikuwa ni zuri. Halikuwa joho jeupe. Lilikuwa—lilikuwa ni joho la zambarau, laini hasa na zuri, hawakupata kuona kitu kama hicho kilichofumwa katika wakati wote.

276 Hivi Wapentekoste si wangemeza jambo hilo? A-ha! Jamani, hilo lingekuwa ndilo lenyewe. Naam, bwana.

277 Kwa hiyo huyo mzee askofu alikuwa ni mtu mwerevu sana, hata hivyo. Ninii yake. . . Kulikuwa na shida gani kwao, kanisa kule nyuma? Walidumu na Neno. Hawakudhania lolote, haidhuru ilikuwa mhemuko wa namna gani.

278 Mungu aibariki mioyo yenu, ndugu. Dumuni na Neno hilo. Haidhuru mchungaji wenu, haidhuru John Doe, ama mtu mwingine yeyote anasema nini, ama kanisa, ama dhehebu linasema *hivi*, *vile* ama *vinginevyo*, "Yote ni sawa. Fanyeni vizuri mwezavyo." Usiamini jambo hilo. Dumu tu na hilo Neno.

279 Kwa hiyo joho hili halikuwa la maumbile haya ya kawaida. Naye akasema, "Sasa mnaona, tangu sasa na kuendelea, nimeketi miongoni mwenu, katika joho hili zuri lililotumwa kutoka Mbinguni."

280 Whiu! Hilo si lingaliuvunja mkutano wa Kipentekoste, ndugu? [Ndugu mmoja anasema, "Lingeuvunja."—Mh.] Si wangefanya hivyo? A-ha! Mnaona? Kuyapofusha macho,

kupokea tu kitu fulani, loo, ni rahisi sana kudanganywa. Mnaona? Hiyo ni kweli. Msipokee jambo hilo.

281 Kasema, “Bwana alinipa hili. Na sasa inawabidi ninyi nyote kujua ya kwamba mimi ni nabii. Mimi ni mmoja wa manabii wa Agano la Kale. Sasa ninyi nyote sikilizeni yale ninayowaambia.” Mnaona? “Nitatoa amri hapa tangu sasa na kuendelea.”

282 Lakini kwa namna fulani, yule askofu mzee, halikumwingia. Kamwe hakukuwapo na. . .Jambo fulani halikuwa sahihi. Mnaona? Halikuonekana sawa kabisa, kwa kuwa moyo wa mvulana huyo haukuwa sahihi. Mnaona?

283 Hivyo sivyo manabii wanavyotenda. Wao hawathibitishwi na yale wanayosema, yale wao. . .namna hiyo, yale wanayokiri. Ni ishara zinazowafuata.

284 Mkristo, vivyo hivyo, na kadhalika. Kama tukisema sisi ni Wakristo, na tungali katika ulimwengu, basi kuna kasoro. Mnaona? Kuna kasoro fulani. Haininii, haisikiki sawa, haionekani sawa. Haidhuru unasema ni sawa kiasi gani, bado si sawa. Inapaswa kuja kwa Neno, kurudi kwenye Neno.

285 Kwa hiyo yeye alisema, yule askofu mzee alisema, “Tutatumia usiku uliosalia katika kuimba nyimbo na—na kuomba.” Kila kitu kiliendelea. Yule askofu mzee aliomba usiku kucha. Hao wengine walimwimbia Bwana nyimbo.

286 Kesho yake asubuhi. Walijua ya kwamba Martin alikuwa nabii wa Mungu aliyethibitishwa. Haikumbidi kumwambia mtu yeyote ya kwamba kazi zake zilithibitisha jambo hilo. Kwa hiyo akasema, “Kuna jambo moja zaidi ninalotaka ufanye, mwanangu.” Kasema, “Ninataka uende usimame mbele ya Martin.”

Akasema, “Loo, nimeonywa nisisimame mbele ya Martin.”

287 Haya basi. Haya basi. Mnaona? Yeye aliye na dhahabu nzuri haogopi kuipeleka kwenye mtambo wa kuhakiki. Yeye anayeishi maisha yasiyo na lawama hajali yale ulimwengu unayomwita, “mtakatifu anayejifingirisha.” Hiyo ni kweli. Kama mwanamume akiishi maisha yasiyo na lawama, wakati mwanamke anapoishi maisha yasiyo na lawama, anaweza kusikia namna yoyote ya neno likihubiriwa kutoka katika Neno la Mungu, ama mwanamume, yeyote wao. Halimsumbui. Hakika halimsumbui. Haimbidi kwenda, kuhofu jiwe la kumhakiki, kama una dhahabu halisi. Haikubidi kuogopa kuhusu hilo. Itastahimili jaribio.

288 Na kwa hiyo walisema, “Utaenda hata hivyo,” kwa kuwa wanajua ya kwamba Martin alikuwa amethibitishwa kuwa ni nabii wa Bwana. Kwa hiyo, Mungu alikuwa pamoja naye katika mambo aliyokuwa amefanya, na kuthibitisha kwamba ni kweli. Kwa hiyo wakaanza kumbeba, kumpeleka, kwa vyovyote vile, na ndipo joho hilo likatoweka. [Ndugu Branham anadata kidole

chake—Mh.] Mnaona ni rahisi jinsi gani, kudhania? Mvulana huyo mwaminifu, akidhani alikuwa amesikia sauti! Ingekuwa ni rahisi jinsi gani kwa askofu huyo, na yeyote wao, kushawishiwa na jambo hilo, bali hao ndugu walilishikilia Neno.

289 Wakati baraza hilo la Nikea lilipokuja pale, walianza ubishi. Wengi wenu ninyi wahudumu mnajua ninalozungumzia. Wale waliokuwa kwenye shule halisi, kama vile Mtakatifu Patrick na hao wengine ambao walienda huko, na watu mbalimbali, hao na akina Ireneo na watu mbalimbali, walidumu katika Neno. Hao wengine walichukua mafundisho ya sharti na wakaanguka, na ndiyo hiyo hapo hata leo. Lakini waaminio halisi walidumu na Neno. Mungu abarikiwe! Ninajua.

290 Hebu tusidhanie chochote. Dumuni na hilo Neno. Naye Mungu anawajibika kufanya . . .

291 Neno hilo ni Mbegu, na hilo Neno litazaa kila kitu lilichoahidi kuzaa. Litazaa. Litaondoa ulimwengu kutoka kwako. Litakutakasa. Litakufanya uishi maisha ya tofauti. Litakufanya ufanye mambo ambayo ulidhani usingeweza kufanya, kwa maana ni Neno ndani yako.

292 Usidhanie umempata. Angalia maisha yako, na ujipime uone maisha yako yakoje. Angalia jinsi unavyoishi. Angalia kama uko katika Imani. Angalia uone kama kila kitu kinaenda barabara kabisa. Angalia kama ulimwengu ungali una upendo, sana, hivi kwamba utakuita uyaache mambo ambayo kweli ni ya Mungu, kuipenda dunia. Kama ndivyo ilivyo, ndugu, jichunguze papa hapa. Simama papa hapa, useme, "Shetani, rudisha kitu hicho kichafu. Sitakipokea."

293 "Vema, huko kwenye kanisa la *Nanii*, wanafanya hivyo. Ndugu *Nanii* huwaruhusu watu wake.

294 "Sijali yale Ndugu *Nanii* afanyayo. Neno linasema lisifanywe. Hilo latosha." Hiyo ni kweli.

295 "Vema, wao, wao ndio dhehebu kubwa mno nchini. Wote wanafanya hivyo. Wanasema ni sawa." Ndiyo. Naam, huenda wakasema ni sawa.

296 Lakini Mungu anaposema, unaona, Neno la Mungu lilisema. Shetani alisema, "Imeandikwa . . . " Naye Yesu akasema, "Pia imeandikwa . . . " Mnaona? Hilo hapo. Mnaona? Imeandikwa.

297 Hatuna budi kutii Neno la Mungu. Usidhanie lolote. Usilichukue vivi hivi tu. Usithubutu wakati huna mamlaka ya kuthubutu. Jambo la kufanya ni kukaa pale na kungojea, kama ni siku kumi, siku ishirini, miaka kumi, ama chochote kile, mpaka utakapokuwa na hakika kabisa, nalo Neno linajishuhudia ya kwamba ni kweli. Ndipo wewe uko sawa. Maisha hayo yatanyooka, na yaje moja kwa moja kwake, yaje moja kwa moja mahali pake. Hakika yatakuja.

298 Na, kanisa, daima nimeshangaa. Ningependa kuingia kanisani...natumaini kuliona kabla sijafa. (Ninafunga.) Niingie kwenye kanisa wakati mmoja, na kutembea kule na kuona tu, loo, jinsi ambavyo dhambi hata haingekaa kwenye kanisa hilo. Mshiriki yeyote ingemlazimu kuitubia kabla hata hawajafika pale. Roho Mtakatifu angeiita papo hapo tu, namna hiyo. Unaona? Kama tu, niwaone wanawake wameketi pale, wakionekana kama mama wa heshima. Niwaone wanaume kama wanaume, wanaume waadilifu kweli, wanaume waliojazwa na Roho Mtakatifu, waliojazwa na Roho. Hebu dhambi moja tu iwe kanisani, mahali popote, Roho Mtakatifu anaiita moja kwa moja. Kama vile Anania, Safira, kuwa nayo papo hapo mbele yenu. Mnaona? Loo, hilo ndilo kanisa ningetaka kuona. Laiti ningaliliona.

299 Nimepigana kote nchini, marafiki. Nimepigana. Nimewagongagonga. Ni—nimefanya kila kitu, nikawakemea watu, na mara nyingine nikayakaripia madhehebu yao, na kadhalika. Si madhehebu; siyo. Dhehebu ni sawa. Sina chochote dhidi ya hilo. Lakini sikiliza, ndugu, watu wengi sana, unaona, wanategemea dhehebu hilo. Mnaona?

300 Kama ulikuwa ukishuka kwenda mtoni kuelekea kwenye maporomoko, nami nikaona ulikuwa kwenye mtumbwi mdogo, na mtumbwi huo ulikuwa unaenda kuzama. Nami nikikupigia kelele, si kwamba sikupendi. Ni kwa sababu ninakupenda. Unaona? Utajigonga upasuke kwenye hayo maporomoko.

301 Na kama ukisema, "Vema, sisi ni wa *hili*. Lakini, Ndugu Branham, nakwambia, sisi, mchungaji wetu, yeye ni mtu mzuri." Sitilii hilo shaka hata kidogo. Na mtu huyo ni mwaminifu. Yeye anadhania kwamba yuko sahihi. Ndipo unasema, "Mbona, yeye anasema, 'Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu. Hakuna kitu kama kunena kwa lugha. Hakuna kitu kama mambo haya. Hiyo si kweli.' Kwa nini, anasema hilo ni kosa. Dhehebu lake linafundisha jambo hilo." Vema, mimi sipingi dhehebu lake, lakini kitu hicho kitapasuka.

302 Yesu alisema. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Mnaona? Usidhanie. Uwe na hakika. Ndipo unaye, wakati unapokuwa na hakika. Ni wangapi wangetaka kweli kuwa tu na tukio la aina hiyo, wangetaka kuingia kwenye kanisa kama hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hivi si lingekuwa ni jambo zuri sana? ["Amina."]

Na tuinamishe vichwa vyetu kidogo.

303 Baba yetu wa Mbinguni, katika Uwepo wa utakatifu Wake, tukijua ya kwamba Yeye Ndiye wa kweli na wa haki, jinsi ilivyo vigumu, Bwana, kuja kwa ndugu na dada na kuzungumza mambo yanayoumiza, na kuchimba, na kurarua. Na jinsi ilivyo vigumu kusema mambo hayo, Baba. Na—naomba unirehemu, na

ujue ya kwamba moyo wangu unawaendea watu katika—katika upendo, ya kwamba ni—ninapenda kabisa kuwa nao.

304 Na ni kwa nini inilazimu kusema mambo kama hayo? Kwa sababu, Baba, ninaamini ya kwamba—ya kwamba yanapaswa kusemwa, ya kwamba ni—ni Neno Lako, na linapaswa kufanywa. Na mara nyingi inasaidia ndugu zetu safarini, wakati kusanyiko linapojivuna sana hata wana—wanapuuza amri za mchungaji na kadhalika. Halafu basi, Bwana, Wewe unamtuma, mara nyingine, mtu fulani mwingine, na kufanya vinywa vya mashahidi wawili ama watatu, na kuona ya kwamba—ya kwamba linaaminiwa kweli, na ni kweli kabisa, na watu mbalimbali wakilinukuu. Ndipo watu hao watasimama bila udhuru katika siku hiyo.

305 Baba Mungu, ninajua hakuna mtu hapa ambaye angetaka kupotea kwenye Siku hiyo. Jambo lililo mbali sana na nia yao lingekuwa ni kupotea kwenye ile Siku. Na, Bwana, haidhuru tumefanya nini, Wewe ulisema, "Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi hata kuuona Ufalme wa Mungu." Ndipo kama tumezaliwa mara ya pili, sisi ni wana wa Mungu, na mambo ya ulimwengu yamekufa kwetu. Hatujihusishi nayo tena. Yame—yamekufa.

306 Nami ninakuomba Wewe, Baba, ya kwamba Wewe utakuwa na rehema usiku wa leo na kutujalia ya kwamba kila mshiriki wa kanisa ambaye amehusika katika mambo kama baridi kidogo, na kurudi ulimwenguni, ya kwamba, upesi watakuwa kama yule hua aliyetolewa kwenye safina, aende akatafute nchi kavu, kisha arudi. Asingepata mahali pa kusimama kwa nyayo za miguu yake, juu ya mizoga iliyokufa. Ndipo akabisha dirishani, mpaka baba Nuhu akamwacha apumzike ndani ya safina, mpaka mafuriko yalipopungua. Ee Bwana, jalia mtu huyo amrudie Mungu usiku wa leo.

307 Jalia kanisa lirudi, likiwa zima. Jalia huu uwe ni wakati wa kujichunguza, katika Phoenix. Jalia makanisa yachochewe katika utakatifu, Bwana. Na jalia kuwe na uamsho mkubwa, kuona ya kwamba, ile miamsho mikuu ambayo Wewe unaanzisha, na. . .na nguvu za Mungu zianze kububujika miongoni mwa watu. Na ndipo ulimwengu na kutojali, na maigizo, na—na kujilinganisha kimwili, na—na ulimwengu unajipenyeza kanisani, kama tu vile ilivyokuwa kwenye somo letu usiku wa leo. Walipiga mbio vizuri.

308 Walitoka Misri, chini ya tohara, na katika damu ya mwana-kondoo, na—nao walikuwa wakienenda vizuri. Lakini walipofikia pale kwenye sehemu nyingine ya Neno Lako, na halafu wakalitilia shaka, papo hapo walisimama, nao wakashindwa vita.

309 Na, Baba, tunaomba ya kwamba hilo halitatukia kabisa kwa Kanisa Lako katika siku hizi za mwisho. Mungu, usiruhusu

tushindwe vita. Jalia tuwaweke akina Akani wote nje, na ka—kabari kutoka kwenye kambi, na—na turudi kwenye Neno, na turudi kwenye utakatifu, na turudi kwenye haki, na kumwishia Mungu katika nguvu za Roho Mtakatifu. Tujalie, Bwana.

310 Kwa Yesu Kristo ninaomba ya kwamba utaweka njaa katika mioyo ya watu, kuona kanisa hilo kama lilivyokuwa huko nyuma zamani za kale, wakati hata hawakuwa na vyo—vyombo vya kudumu kanisani. Hata hawakuweka madhabahu ndani yake, kwa sababu makafiri wangejilaza chini mbele ya madhabahu, na kusujudu mbele ya sanamu za vinyago. Nao walihofu kuweka madhabahu kanisani, kwa sababu watu, waongofu wa kawaida, huenda wakajaribu kuabudu madhabahu badala ya Mungu a—aliye hai.

311 Nao wangepiga magoti moja kwa moja hadharani, na kuinua mikono yao juu moja kwa moja kwa Mungu asiyeonekana, kwa maana walipenda yale matokeo ya kububujika kwa Roho. Waliketi kwenye bamba za kale zenye baridi ya—ya mwamba, na—na ardhini, kusikiliza mtu mcha Mungu akieleza Injili na nguvu za Mungu, kisha Roho Mtakatifu anashuka mkutanoni.

312 Ee Mungu, tunawaona wakiingia kwenye matundu ya simba, na katika mashimo ya moto, na—na kila kitu, Baba. Na katika ule ufufuo, sisi tutasimama wapi? Huenda wasihitajike leo kwenda kwenye mashimo na kwenye matundu ya simba, bali Mungu, tunatakiwa kuishi maisha mazuri na matakatifu, na kulingana na utaratibu wa Mungu; kuishi maisha ya utauwa, tukichunguza na kuomba, na—na kungojea, na kuangalia wakati wowote Yeye angekuja: si kuogopa kwamba Yeye anakuja, bali "kupenda kuonekana Kwake." Tujalie, Bwana.

313 Tunapenda kuona hilo Kanisa kubwa limeitwa pamoja, na sehemu hii inayopumzika na kupita hapa Phoenix. Tunaamini ya kwamba una kweli mamia ya washiriki wa Kanisa Lako walio wapitaji hapa Phoenix, wakiungojea ule wakati. Bwana, hawadhanii. Wamejazwa na Roho. Maisha yao yanalingana na kuonyesha kwamba wamejazwa. Hao ni watoto Wako.

314 Na kuna wengine wangetaka kuwa hivyo, Baba. Labda wamedhania tu, nao wanaangalia maisha yao huko nyuma na kuona hayaenendi namna hiyo. Kuna kasoro. Ninaomba, Baba, ya kwamba usiku wa leo utaninii . . . kukiweko na yeyote hapa, ya kwamba huu utakuwa ndio usiku watakaoitwa, kwamba hawataona haya, bali watasimama na kusema, "Nimekosea. Mungu, nisamehe. Na unisaidie, tangu usiku huu na kuendelea, kuja kabisa kwenye Neno, na kuliamini lote, na kujazwa na Roho, na kutakaswa hivi kwamba ushuhuda wangu hautakuwa dhidi yangu kwenye jiji hili." Tujalie, Baba.

315 Sasa wakati tumeinamisha vichwa vyetu, macho yetu yamefumbwa, nitawauliza, kama—kama ndugu yenu, kama msafiri pamoja nanyi, anayeutafuta mji ambao Mwenye

Kuujenga na Kuubuni ni Mungu. Nami nashangaa, baadhi yenu akina dada hapa usiku wa leo, baadhi yenu ndugu, hapana shaka ninyi ni wazuri, waaminifu. Sijataka kuwaudhi. Bali nilitaka kuwaambia lililo Kweli, Neno la Mungu.

316 Nami nimekuwa katika mji wenu na kufanya miamsho. Mmeona ya kwamba—ya kwamba ninamwamini Mungu. Mungu hajibu wenye dhambi. Tunajua jambo hilo. Nasi tu—tunaninii. . . Ninaamini kuwa mimi ni Mkristo. Nami. . . Na—na wachungaji wenu wamewaambia, kote jijini hapa. Nanyi mtakuta kwamba mnakiri ya kwamba mna Roho Mtakatifu, na mtaona ya kwamba mngali mnapatana na ulimwengu, kutangatanga huko nje ulimwenguni. Hutaki jambo hilo, sivyo, dada? Hutaki jambo hilo. Wewe ni mtu mzuri sana kuwa namna hiyo. Usingekosa hilo kwa chochote kile. Na sasa, tangu usiku wa leo na kuendelea, Mungu, . . . Kama kabisa hujapata kusikia hilo hapo awali, Mungu atakuwajibisha kwa hilo. Atakuwajibisha.

317 Ndugu, kama una hatia ya baadhi ya mambo hayo ambayo tumekuwa tukizungumzia, hutaki kuwa hivyo, sivyo, ndugu? Hakika hutaki. Unataka kuwa Mkristo halisi.

318 Mungu anawezaje wakati wowote kutuingiza kwenye aljebra, kama nilivyosema, wakati hatuwezi kuondoka kwenye shule ya chekechea. Unaona? Hu—huenda tukawa na mihemuko. Huenda tukapaza sauti na kumsifu Mungu, na kucheza katika Roho, na yote namna hiyo. Mbona, hilo, hayo yote ni sawa, ndugu, dada. Ninaamini katika hilo, pia. Lakini nimewaona wakicheza ngoma wakizunguka kinyago moja kwa moja vivyo hivyo, wakipaza sauti na kupiga mayowe, na kunena kwa lugha, mnaona.

319 Kwa hiyo maisha ndi—ndiyo muhimu. Mnaona hilo? "Kwa tunda wanajulikana." Nawe unaona kwamba unaninii. . . hayaendani. Je! ungetaka kuwa Mkristo halisi? Na sasa nawatakeni, huku macho yenu yamefumbwa, mkiomba, mkiweza. Ninawatakeni mwe waaminifu sana sasa, sasa hivi tu iweni waaminifu sana.

320 Dhambi haiwezi kufunikwa kwa kunywa pombe, kwa kuitupilia kando, kwa kujiunga na kanisa, kwa kujaribu kufanya vizuri zaidi. Dhambi inaweza tu kuuawa na nguvu za Mungu, Damu ya Yesu Kristo. Je! hivi usingetaka maisha ya namna hiyo? Kama ungetaka, nawe unaninii. . . Unaamini ya kwamba Mungu yuko katika jengo hili. Uwepo Wake usioshindwa uko karibu daima, haidhuru wewe uko wapi.

321 Ono hivi majuzi asubuhi, Yeye aliniambia hivyo. Alisema, "Ninii. . . Usiogope." Alisema, "Simama kwa ujasiri, unaona, maana uwepo usioshindwa wa Kristo uko karibu."

322 Je! ungetaka kuwa Mkristo wa aina hiyo, kama vile u—unavyojua kweli unapaswa kuwa? Wewe, wewe unajaribu kuwa, lakini hujafikia mahali hapo bado. Sasa, maisha

yako mwenyewe yanathibitisha jambo hilo. Unaona? Mwinulie Mungu mkono wako. Sema tu…Mungu akubariki. Hiyo ni mioyo yenye uaminifu, minyofu. "Kweli ninataka kuwa."

323 Sasa, vipi kama unaninii…Kama unajua maishani mwako ya kwamba huambatani na yale Mkristo anayopaswa kufanya. Na halafu basi, hata sasa, katika Uwepo wa Roho Mtakatifu, Shetani anakufanya ushushe mkono wako chini, wala hutalipokea. Sasa, vipi kuhusu hilo? Wakati, unajua, papa hapa kwenye Maandiko, ya kwamba umekosea. Ninasema jambo hilo kwa upendo, heshima. Mnaona?

324 Jinsi hilo lilivyo jambo baya, mnaona, kwamba mngejua hilo. Sisemi ya kwamba ndivyo mlivyo. Lakini, ninasema, kama ungejua jambo hilo, na kujua ya kwamba, maisha yako, uangalie yale unayofanya, na mambo ambayo unayatenda, uone maisha yako hayalingani na Biblia. Nawe unasikia, Injili inahubiriwa. Unaisoma wewe mwenyewe. Unajua ni kosa kufanya mambo hayo, na hata hivyo unayafanya. Unaona? Hilo si ni jambo baya sana?

325 Sasa, angalau mikono ishirini, thelathini iliinuliwa. Je! kuna mmoja aliyeachwa, angetaka…? Sasa, mtu yeyote asiangalie. Hebu mimi tu niangalie. Ninataka kuomba. Wengine waliachwa, naomba uinue mkono wako. Ninakuona wewe kwenye roshani. Ndiyo. Naam, pale. Mungu akubariki. Kuna wengine wengi. Ndiyo. Mungu awe pamoja nawe. Huo ni uaminifu kweli. Mbona tusilitatue usiku wa leo? Kwa nini tusiseme tu, usiku wa leo, "Hebu na tulitatue."

326 Sasa, nimekuja miongoni mwenu, huku Phoenix, mahali hapa panapopendeza, nikiwathamini sana, barua mnazoandika, na kutia moyo na kadhalika, mnavyojitahidi kunitia moyo niendelee. Nanyi huniombea. Hiyo ndiyo sababu ninaninii… Ninataka kuwa mwaminifu kwenu. Unaona? Ndipo Kristo atanifanya niwajibike kwa jambo hili. Na kama siwaambii Kweli yote, basi, uone, itanibidi kuwajibika. Na hiyo ndiyo sababu, ninawatakeni—ninawatakeni mwe Kule, ndugu, dada.

327 Usibahatishe. Kama kuna nafasi iliyo ndogo sana, usibahatishe. Kamwe usicheze nayo. Usiache…Hebu kweli tuwe Wakristo halisi, halisi sana. Hebu tuninii. Unaweza kuwa. Wengine ndivyo walivyo. Unaweza kuwa, pia. Unamjua dada fulani ambaye ungetaka kuwa kama yeye, mwanamume fulani ungetaka kuwa kama yeye, mhudumu fulani ungetaka kuwa kama yeye, mtu fulani. Unataka kuwa hivyo. Unaweza kuwa. Sasa hebu na tuamini kwa moyo wetu wote.

328 Sasa, wakati tukiwa tumeinamisha kichwa chetu, nitamwomba dada yetu kwenye piano pale, ninamuomba, atupe tu sauti ndogo ya wimbo, dada, ninakuomba. Nami nashangaa, ninyi ambao kweli mngetaka kuninii, sasa, kama kweli ninyi ni

waaminifu. Itatendeka sasa hivi kama kweli ninyi ni waaminifu. Lakini inawabidi kuwa waaminifu.

329 Nina ushuhuda. Nimekuwa . . . Tangu mama yangu alipoaga dunia, nimekuwa huko nyikani, nikilala ndani ya pango, nikifunga na kuomba. Ono lilinijia. Na hilo lilikuwa ni moja ya yale mambo, ule unyofu. Unaona? Sasa, kweli unamaanisha jambo hilo, ya kwamba unataka kuwa Mkristo wa namna hiyo? Unataka kuachilia ulimwengu wote uondoke, kila kitu kiondolewe kwako?

330 Kama kweli unamaanisha jambo hilo, humwonei aibu mtu yeyote katika kanisa hili. Huoni aibu kwa mtu yeyote kukuona ukisimama. La, bwana, huoni aibu. U—u—uliinua mkono wako kwa Mungu. Huonei aibu kitu chochote. Unakuja. Kitu pekee unachoonea aibu ni maisha yako. Unaona? Nawe unataka—unataka yanyoshwe. Unataka. Daima umetaka kushinda, ili kwamba ufanye mambo yaliyokuwa sawa.

331 Kama wewe ni mwaminifu jinsi hiyo, ninataka usimame uje hapa, usimame hapa madhabahuni, kana kwamba ulikuwa ukija kuombewa kama vile ulikuwa u mgonjwa. Ninataka kukuombea, na kukuwekea mikono. Kama unataka kuja hapa sasa kwa ajili ya jambo hilo, toka tu moja kwa moja. Nina hakika ya kwamba Baba wa Mbinguni ataninii . . . Njoo tu kwa utulivu na usimame moja kwa moja karibu na madhabahu hapa. Njoo kwa ajili ya kuwekwa wakfu, mtulivu uwezavyo.

332 "Ninayaweka wakfu maisha yangu, tangu usiku huu na kuendelea, Ndugu Branham. Sitadhania jambo lolote. Ninakuja sasa hivi. Ninakuja sasa hivi. Nime—nimemalizana nayo. Nina—ninamwahidi Mungu. Mimi, haidhuru iweje, mimi ni—mimi ni huru na dhambi sasa hivi. Mimi ni . . . Ninataka kuwa Mkristo halisi. Ninakuja kuyaweka wakfu maisha yangu." Hilo linanifanya nijisikie vizuri sana kuwaona mkifanya hivyo.

333 Sasa, hebu—hebu tu kwa dakika moja ama mbili zaidi sasa. Je! kuna mtu mwingine angetaka kusimama tu, na kusema, "Mimi, usiku wa leo, ninayaweka wakfu maisha yangu. Mimi . . . Mungu, mimi ni—nimechoshwa na haya. Daima nimetaka kuwa Mkristo halisi, halisi sana. Limeuchoma moyo wangu tangu nilipokuwa mvulana mdogo, ama msichana mdogo. Ni—ninataka ninii hasa . . . Si—siwezi kubahatisha namna hii, nikijua sina budi kufa." Hivi mbona usije, usimame tu hapa karibu na madhabahu kwa dakika moja, kwa ajili ya kuwekwa wakfu? Sasa, kuwekwa wakfu huko kunamaanisha kuwekwa wakfu kwa ajili ya jambo fulani, aliyewekwa wakfu kwa Kristo. Je! waweza kuja na kusimama karibu na madhabahu kwa ajili ya jambo hili, kwa dakika moja?

334 Wakristo ambao hawana tukio hili, msibahatishe juu ya jambo hili sasa. Unaona? Mti unajulikanaje? Kwa matunda unayozaa.

335 Sasa, tunakuja tu kwa uaminifu tujuavyo kuja. Baadaye kidogo, katika mmoja wa mikutano makanisani, mtajua ni kwa nini ninafanya jambo hili. Sina wakati wa kusema jambo hilo usiku wa leo, kuliingilia. Lakini mimi. . .mtafahamu ni kwa nini ninafanya jambo hili. Ninaamini Mungu analipa kanisa Lake wito Wake. Huo ni ninii. . .karibu ni wa mwisho tutakaopata. Mnaona? Ni jambo litakalotukia, nami sijui ni lini. Linaweza kukupata kabla ya asubuhi. Linaweza kunipata kabla ya asubuhi.

336 Lakini, ndugu, dada, je! tunaweza kuthubutu kubahatisha juu ya jambo lolote moja dogo, haidhuru tu ni lipi? "Aliye na hatia katika jambo lililo dogo sana ana hatia ya yote." Inakubidi uwe safi, umeoshwa katika Damu ya Mwana-Kondoo. Dhambi iliyo ndogo sana itakuzuia mara moja. Unaona? Kama Malaika wanaonekana wachafu mbele Zake, na sisi je?

337 Sasa, nitangojea tu dakika moja ama mbili zaidi, maana huenda kukawa na mtu mwingine. Tena, hatua moja mara kwa mara, ukija. Nataka uje ukiwa myofu sana sasa.

338 Sasa, hapana shaka yoyote, ila wengi wenu mnaosimama hapa madhabahuni mmekuwa na matukio ya mambo mbalimbali. Labda mmepiga makelele, mkalia, mkanena kwa lugha, mkacheza katika Roho, ninyi ndugu na dada. Hapana shaka mmefanya hivyo. Na hayo—hayo mambo ni sawa, sawa kabisa.

339 Lakini mnajua wakati Waebrania, mlango wa 6, "Mvua huinyeshea nchi mara nyingi, kuitayarisha, kuilima kwa ajili ambayo yalimwa. Bali miiba na magugu hukataliwa, ambayo mwisho wake ni kuteketezwa." Walijuaje tofauti yake? Roho yeye yule, Uhai ule ule, maji yale yale yaliyoinyea ngano yaliyanyea magugu pia. Nayo miiba, na michongoma, na ma— na magugu yalifurahi tu na kuburudika kwa mvua ile ile. Nao watu wanaweza kuketi kanisani, marafiki, na kupokea matukio ya namna ile ile.

340 Sasa, usidanganyike katika jambo hili, rafiki. Unaona? Unaweza kupokea tukio lile lile kwa Roho Mtakatifu yeye yule ambaye mtu anayeketi karibu nawe alimpokea, na ingali iwe si Huyo. "Jua huwaangazia wenye haki na wasio haki. Mvua huinyea miiba na ngano." Inatumwa kwa ajili ya ngano. Roho Mtakatifu hutumwa kanisani kwa ajili ya watakatifu waliowekwa wakfu, bali wale wanaoketi pale humfurahia. Hakika. "Lakini kwa matunda yao wanatambulikana."

"Je! tuyang'oe," kasema, "halafu?"

341 "La. Acha yakue pamoja. Na kwenye Siku ile, Malaika wataondoka na kuyakusanya magugu yote na mitambaazi, na watavichoma moto. Bali ngano itakusanywa ghalani. Kwa matunda yao mtawatambua."

342 Hiyo ndiyo sababu mnasimama hapa usiku wa leo, ni kwa ajili ya tunda, tunda la Roho. Sasa, kumbukeni.

343 "Ni kwa nini," mnasema, "Ndugu Branham?" Labda baadhi yenu ninyi wanawake mnaosimama hapa. Ninaona mna nywele fupi, "Ni kwa nini, Ndugu Branham, mimi ni Mkristo, na ni—ningali ninaonekana tu kana kwamba siwezi kufanya hivyo. Siwezi kuacha nywele zangu zikue. Hata hivyo ninajua ya kwamba Biblia inafundisha ya kwamba hiyo ni kweli. Agano Jipya linafundisha ya kwamba hilo ndilo jambo la kufanya. Siwezi kufanya jambo hilo kamwe. Inaonekana kana kwamba siwezi kushinda jambo hilo, mnaona, siwezi kufikia mahali hapo." Mnaona?

344 Ninaamini wewe ni mtu mzuri. Ninaamini wewe ni mwaminifu. Usingekuwa umesimama hapa kama mfano usiku wa leo. Unafanya jambo hilo. Na, hilo, hivyo ndivyo inavyokupasa kufanya. Ni Maandiko. Inakubidi kufanya hivyo. Unaona?

345 Baadhi yenu ndugu, Mungu ndiye tu anayejua moyo wako, kwamba unasimama hapa kwa sababu gani, mambo unayotaka kushinda. Sasa, u—unaweza kufanya hivyo, kama utalikubali tu namna hii. Na kusema, "Bwana, mimi si kitu sasa, na ninajitolea tu Kwako, nami huyu hapa ninakuja. Kwa neema yako nitafanya hivyo." Sasa, hu—huwezi kufanya hivyo bila ya Yeye. Hakuna kitu ulimwenguni unachoweza kufanya. Inakupasa kumwacha Yeye afanye hivyo. Unajiweka wakfu tu Kwake, na kuamini jambo hilo kwa moyo wako wote, ndipo Yeye atafanya jambo hilo. Atalifanya kwa ajili yako, unaona, kama tu utamchukua kwenye Neno Lake. Asingeweza kumfanya mmoja namna hiyo, wala asingemfanya mwingine namna hiyo. Atawafanya ninyi nyote hivyo. Mnaona? Atawafanya ninyi, kila mmoja, ipasavyo.

346 Ninawatakeni ninyi watu wote ambao ni Wakristo na mnaoishi juu ya mambo haya, ninawatakeni mwombe, ninawatakeni mwombe pamoja nami. Hasa sana ndugu wahudumu, kuomba pamoja nami. Ninataka kila mmoja wenu sasa, katika kilindi cha moyo wako . . . Unaona?

347 Unajua ya kwamba mvua imekunyeshea. Unasema, "Ndugu Branham, nilicheza katika Roho. Nilinena kwa lugha." Hiyo ni kweli. Lakini angalia, unaona, kuna jambo fulani lisilo sawa pale. Unaona? Unaona? Inakupasa kutoka kwenye gugu hili sasa, uwe ngano: mnyenyekevu, mtamu, ukiwa na Neno, mtiifu, unaona, mtiifu kwa Neno.

348 Sasa hebu tu mruhusu Roho Mtakatifu aingie, na hebu mruhusu Mungu akubadilishe usiku wa leo kutoka kwenye kile ulichokuwa, kufikia kile Yeye anachokutaka uwe, tunapoomba.

349 Baba yetu wa Mbinguni, ninatambua ya kwamba hapa kwenye madhabahu hii, ambayo, kanisa ni madhabahu, mahali ambapo watu wanakuja na kujiweka juu yake, wapate

kupokelewa kama sadaka ya kuteketeza kwa Bwana. Ninajua, Baba, usiku wa leo baadhi ya watu hawa wanaosimama hapa, na washiriki wa—wao waliomo kwenye makanisa ya hapa, nao wanasimama hapa kwenye madhabahu hii kwa ajili ya utakaso. Na hilo—hilo ni jambo kubwa kwao kufanya, kwa maana wanawashuhudia watu wanaposimama hapa, na mbele Zako, ya kwamba—ya kwamba kuna kasoro fulani maishani mwao.

350 Na kadiri ilivyonilazimu kuwakatakata maskini dada hawa wasichana usiku wa leo, Baba, juu ya ABC za—zao, na hapa wanaamka moja kwa moja kutoka kwenye kiti chao, wanatembea moja kwa moja kama mama wa heshima, wanasimama pale na kusema, "Basi, Mungu, kama nimekosea, nifinyange na kunifinyanga." Hawa hapa ndugu wanaosimama hapa, vivvyo hivyo. Hata hivyo wamesimama kutoka kwenye kiti chao na kuja moja kwa moja.

351 Ndani ya moyo wao kuna shauku. Na Baba, Shetani asingeweza kuweka shauku moyoni mwao kufanya mema. Angeweka shauku moyoni mwao kufanya mabaya. "Endelea. Usipande kwenda kule. Achana na hilo. Usiliamini." Hivyo ndivyo angesema.

352 Ndipo basi tunapambanua jambo hilo vipi? Kwa Neno. Kama nilivyosema, Mtakatifu Martin, Paulo, maaskofu wote wa kanisa la mwanzoni, na wazee, walipambanua mambo kwa Neno. Na sasa, usiku wa leo, wanapambanuliwa kwa Neno. "Na wanapohukumiwa, wanarudiwa, isije ikawapasa hukumu pamoja na ulimwengu."

353 Kwa hiyo wamekuja sasa, Bwana, kujitakasa, kujitenga na ulimwengu, ya kwamba hawataki uhusiano wowote na ulimwengu. Wanataka kujisalimisha kabisa Kwako, mpaka utu wao wote unaonyesha sura ya Kristo. Kwamba, wanapotembea, wanapozungumza, wanapovaa, wanapotenda, ni sura ya Kristo inayoonekana daima maishani mwao. Na, Baba wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba Wewe utawajalia jambo hilo.

354 Sasa, tukijua ya kwamba wakati umekaribia sana, kule Kuja kwa Bwana; na kuona uamsho huu mkuu kote katika Phoenix sasa hivi, miongoni mwa watu; na kuona nyakati ambazo tumepitia, katika ibada za uponyaji; na kuona jinsi nilivyopewa imani yao, ku—kusaidia kuwakomboa watu kutoka kwenye magonjwa yao na mateso; kuona Roho Wako akitenda kazi miongoni mwetu, Bwana, katika thibitisho ya kwamba Wewe ulikuwa pale, kwa jinsi ya mwili na kwa kisayansi pia.

355 Na halafu, usiku wa leo, kwa wito huu, ninawatoa Kwako, Bwana, katika maombi yangu. Kila mhudumu hapa ndani, Bwana, kila Mkristo anayetembea katika amri za Mungu, wanaomba pamoja nami, Bwana. Nasi tunakupa maombi yetu sasa, kwa niaba ya watu hawa. Jalia kila mmoja wao atakaswe,

tangu usiku huu na kuendelea, Bwana. Jalia nguvu za Yesu Kristo kwa unyenyekevu tu, sasa hivi, zipenye tu ndani ya mioyo yao, hivi kwamba, kwamba zitawafinyanga tu na—na kuwafanya tu tofauti, tangu usiku wa leo na kuendelea.

356 Jalia roho mtamu, mnyenyekevu, aliyepondeka aingie ndani yao, Bwana, katika kutubia mambo yaliyokosewa. Na jalia . . . jitihada kuu za—za neema ya Mungu zishuke juu yao, kuendeleza maisha yao katika njia iliyotakaswa kwa ajili Yako, Bwana. Wapokee, Baba. Tunawatoa Kwako sasa, wanapoyaweka wakfu maisha yao, katika Jina la Yesu Kristo.

357 Sasa, huku vichwa vyenu vimeinamishwa sasa, kwa kuwa mmekuwa mkiomba, ninaamini. Nawe huwezi kumwambia Mungu hata neno moja pasipo Yeye kulijua. Mtakatifu aliye dhaifu sana humfanya ibilisi atetemeke. Nanyi ni watoto Wake. Nanyi kabisa, kwa mioyo yenu yote, kila mmoja wenu, mmeyaweka maisha yenu kikamilifu mbele za Mungu, na kusema, "Mungu, nifinyange na unifanye aina ya Mkristo kama yule aliyezungumziwa habari zake hapa usiku wa leo. Kwa kuwa, ni—nimeyatoa maisha yangu Kwako. Ondoa tu mambo hayo yote katika maisha yangu, mambo yaliyo mabaya, Baba. Na jalia, usiku wa leo na kuendelea, ninaenda kufanya hivyo. Kwa neema Yako, nitakuishia Wewe kila siku, nikiangalia maisha yangu yalingane moja kwa moja na masharti ya Biblia"?

358 Kama umefanya jambo hilo moyoni mwako, naomba uinue mikono yako mbele za Mungu, useme, "Nimefanya jambo hili. Ninaamini kwa moyo wangu wote." Bwana akubariki. Bwana akubariki. Mungu akubariki.

359 Sasa, Baba, wao ni Wako. Wameinua mikono yao. Wamefanya utakaso wao. Na haidhuru zawadi hiyo ni ndogo jinsi gani, Wewe upo hapa kupokea zawadi iliyo ndogo zaidi. Nao wamejitoa Kwako, jinsi tu walivyokuwa. Wanataka kuwa washiriki wa huo Mwili mkuu, bila—bila waa, bila kunyanzi. Nao sasa wamewekwa wakfu Kwako, Baba. Ninaomba ya kwamba utawatenga na mambo ya ulimwengu mradi wangali hai. Kwa Jina la Yesu Kristo. Amina.

360 Sasa nendeni kwenye viti vyenu, mkishangilia, na mkiwa na furaha ya kwamba Kristo amechukua mlivyosema. Sasa, ninaamini . . .

361 Wanaposhuka kwenda chini, kuna mama anayeketi hapa katika kiti cha magurudumu, na mwanamume fulani, ninaamini, nao wanazungumza kwa mikono yao. Wao, hapana shaka wamekuja hapa wapate kuombewa. Je! ninyi nyote mwaweza kuinamisha vichwa vyenu nami nishuke niende nikawaombee?

362 Sasa, ndugu, ili mpate kuzungumza nao pale kwenye kiti cha magurudumu, na kile walicho. Unaona? Sasa, waambie tu jambo hili. Bwana Yesu Kristo anawapenda sana hata yuko tayari sasa kuwaponya. Kama kungekuwako na jambo lolote

ningeliweza kufanya mbali na kuomba, ningelilifanya. Lakini Yeye ameyajibu maombi yangu mara nyingi sana kwa ajili ya watu kama ninyi, ambao wanateseka, na amewaponya. Nimewapenda sana tangu niliposimama hapa.

363 Ninapomwangalia mama huyu, nami ninafikiri juu ya mama yangu ambaye ndiyo kwanza aende kuwa na Mungu siku chache zilizopita. Labda yeye ni mama wa mtu fulani. Nitamwombea. Ninawataka ninyi mwamini, dada na ndugu, ya kwamba Mungu atasikia maombi yetu, Naye atajibu. Na tangu saa ii hii, ninawatakeni mwamini ya kwamba kazi hiyo imekwisha.

364 Sasa, kwa wasikilizaji wengine hapa nje, je! kuna mtu mwingine aliyekuja kuombewa, watu wagonjwa ama kitu fulani, mtu wa kuombewa? Mama huyu hapa, mtu fulani huko. Vema. Ninyi njoni moja kwa moja kuyazunguka madhabahu hapa. Nitafurahia tu kufanya hivyo.

365 Sasa, ni wangapi wanaoweza kukumbuka hapa, muda mrefu uliopita, yapata miaka kumi na minne iliyopita, kule katika kanisa la Ndugu Outlaw? Je! yupo mtu anayekumbuka kanisa la Ndugu Outlaw, wakati nilipokuwa kule yapata miaka kumi na minne iliyopita? Ndugu Garcia na wale walioko kule kwenye kanisa hilo. Mnakumbuka jinsi ninavyowaita watu kuja huku?

366 Nimeuzunguka ulimwengu, wakati baada ya wakati, nikipambanua roho. Ninawaagiza kwa neno na utaratibu usiku wa leo. Je! mlipata kuona wakati wowote ambapo lilishindwa? [Kusanyiko linasema, "La."—Mh.] Hasha. Kwa maelfu ya nyakati, kila wakati lilikuwa kamilifu, sahihi kabisa. Sivyo? ["Hiyo ni kweli."] Sasa, wote wanaojua ya kwamba hiyo ni kweli, inueni mikono yenu, waliokuwa kwenye mikutano na kusikia. ["Amina."] Yeye alisema nini? "Anayosema yakitimia, basi msikilizeni."

367 Sasa, maono hayawaponyi watu. Maono yanathibitisha tu Uwepo wa Mungu. Mnaona? Sasa, ninafikiri ya kwamba kweli tunajua jambo hilo sasa. Lakini vile nilivyofanya wakati huo ilikuwa ni kuomba tu.

368 Kulikuwako na mama mmoja hapa aliyekuwa mahali fulani hapa Phoenix. Jina lake lilikuwa ni Dada Hattie Waldrop, ninaamini ndivyo lilivyokuwa. Ninaamini ndivyo lilivyokuwa. Ama, naam, alikuwa na kansa. Mumewe alikuwa ni fundi bomba. Na kwa kawaida hao huhudhuria mikutano. Sijui kama yeye yupo hapa usiku wa leo ama hayupo.

369 Ninakumbuka ya kwamba alikuwa mkutanoni. Na—nao walisema alikufa; na alionekana hivyo, mstarini. Ninakumbuka juu ya kansa moyoni, naye daktari hapa alituma eksirei na kadhalika, kuonyesha. Hiyo imekuwa ni kama miaka kumi na minne iliyopita. Anaishi sasa.

370 Ninakumbuka nikimwita, nikimwombea mvulana mdogo, kilema, mwenye nywele nyekundu. Bwana alimponya, alimfanya

mzima. Mambo mengi sana tu, mengi kweli, ni mengi sana tu, hayahesabiki. Nitaninii . . .

371 Ninasema jambo hili, kwa—kwa weupe wa moyo wa Kikristo. Nadhani, kama ningeweza kuandika kila jambo lililotukia ambalo nimemwona Kristo akifanya tangu nilipokuwa mhudumu, nisingelundika wingi wa vitabu namna *hiyo* kwenda juu. Nina ushahidi wa maelezo ya madaktari, juu ya watu watano waliotangazwa kwamba wamekufa, wakalazwa chini wamekufa, nao wakafufuka tena, kwa maombi. Mnaona? Wengi waliodai ya kwamba walifufuka, nami—nami nisingeweza kusema hilo. Nisingelisema hilo isipokuwa pawe na njia ya kulithibitisha, mnaona, kujua jambo hilo. Lakini niliwaona basi, baada ya kufa kwa masaa kadhaa, siku kadhaa.

372 Vema, maskini yule mtoto mchanga wa Kimeksiko hapa kwenye jiji la Meksiko, alikuwa amekufa. Kwa, vema, alikufa asubuhi hiyo saa tatu, na hii ilikuwa ni saa nne na kitu usiku huo. Daktari alitia sahihi maelezo hayo, "Mtoto mchanga, mtoto huyo mchanga alikufa kwa nimonia, na amekuwa mfu wakati huo wote." Na akisimama huko nje kwenye mvua, maskini mama huyo msichana wa Kimeksiko. Kamwe sikufanya jambo lolote ila kuweka tu mikono yangu juu ya mtoto huyo. Niliona ono. Nikaweka mikono yangu juu ya mtoto huyo. Alianza kurusha miguu na kulia. Nao Wafanyabiashara Wakristo waliandika makala hiyo si muda mrefu uliopita, ama kitu fulani kuhusu jambo hilo katika *Sauti* ya Wafanyabiashara, kuhusu kufufuliwa kwa wafu. Sasa, inawezekana. Lakini vipi kama . . .

373 Hebu niwaambie kitu. Hebu niwaambie wafuasi wa kanisa hili hapa, na nitalisema kwa wafuasi wowote wa kanisa. Hebu liwekeni kanisa hili wakfu kwa Mungu, na wafuasi wake wote, mnaona, liwekeni wakfu kwa Mungu, kila mmoja wenu, kwa maisha matakatifu mbele za Mungu, angalieni yatakayotukia. Wakati kanisa hilo linapojifunga, na kuanza kuomba, mnaona, maombi ya watu hao yanaanza kwenda juu mbele za Mungu, Yeye hatayakataa. Hiyo ni kweli. Sasa, mimi ni mmoja tu, ambapo kutakuwako na wengi wenu hapa mkiomba. Na uponyaji wa Kiungu hauko na mtu fulani yeyote yule. Ni mioyo minyenyekevu inayomwomba Mungu, na ni watu waaminifu wanaoupokea.

374 Ninatambua ya kwamba kuna karama zinazotumwa kwa Kanisa, lililo na imani. Nami ni—ninatambua ya kwamba huduma yangu ya kuyazuru mataifa, na—na kuchukua tu, kuwaleta tu watu wachache hapa, na kuonyesha maono, na kuyachambua. Na wale wanaopitia kwenye mistari ya maombi ya watu wengine, na kadhalika, wanaingia. Ndipo ingenibidi kukoma, labda kuna jambo fulani nyuma ya maisha ya mtu huyo. Na wengi wenu hapa mmeona jambo hilo moja kwa moja jukwaani: dhambi inatajwa, siri za mioyo yao, na kadhalika, na kuambiwa kinachowazuia kuponywa.

375 Lakini kupitia kwa hao, kwa kupewa tu hao wachache. Maana, wachache tu, ndipo basi nguvu zangu zinakwisha. Unaona? Na ndipo mnafahamu jambo hilo? Ni la Kimaandiko, na jinsi lilivyo. Pia kumekuwako na akina mama wengi wenye mtoto mchanga huko nje, hata siwafikii kwa maombi, mnaona, wagonjwa wengi nisiowafikia kwa maombi. Nafikiri inajulikana vizuri sasa ya kwamba kila mtu anapaswa kujua, ya kwamba nimewaambia kweli, mnaona, ya kwamba ni kweli. Nami nitawaombea tu wagonjwa, na kumwomba Mungu awaponye. Nami ninaamini ya kwamba kila mtu tutakayemwombea atapona.

376 Sasa, kama kuna jambo lolote maishani mwenu, watu wanaosimama hapa, hebu niwaulizeni jambo hili. Kama wewe si Mkristo, kuwa Mkristo. Wewe utoe moyo wako kwa Kristo, ukiwa umesimama papo hapo ulipo. Kama hujajazwa na Roho Mtakatifu, usi—usiache kuomba mpaka Mungu amekujaza kwa Roho Mtakatifu. Kama unafanya jambo lolote baya, katika Mkristo, acha kulifanya. Acha kulifanya. Yachunguze maisha yako. Mwishie Kristo. Nitaomba na kumsihi Mungu.

377 Sasa, asubuhi moja kwenye kiamshakinywa kimoja, ama usiku fulani, ninataka kuwaambia jambo fulani lililotukia ninii—ninii tu. . . Niliondoka hudumani na kungojea, nikarudi kuomba na kufunga, nione kwamba ilikuwa ni kitu gani. Na jambo fulani ambalo daima nimelitamani; lilitukia. Kwa hiyo mimi. . .

378 Si kitu chochote, sasa, cha ajabu-ajabu. Siuendei upuuzi huo. Ninataka. . . Inapaswa kuwa ni BWANA ASEMA HIVI, kwa Neno. Mnaona? Inapaswa, tuna mengi sana ya haya hapa, kugusa, kuhisi, na kila kitu kama hicho sasa, ushirikina na kadhalika. Hebu na tuondoke kwenye upuuzi wa namna hiyo. Hebu na tumrudie Mungu moja kwa moja. Tunamtaka Roho Mtakatifu.

379 Ninaamini ya kwamba Mungu huwatuma watu wakawaombee wagonjwa. Nami ni mmoja wa walio wanyenyekevu. Mimi ni mmoja wa wale wadogo sana ambao Yeye aliwatuma. Nami ni—ninataka kuyatoa maombi yangu kwa ajili yenu usiku huu, mpate kuponywa. Mnaamini. Nami ninawataka ndugu hawa hapa, na dada, kote jengoni, kujiunga pamoja nami katika maombi. Na kuacha tu. . .

380 Ninaamini tunaanzia moja kwa moja hapa. Hebu mtu fulani aje moja kwa moja hapa mimbarani. Halafu hebu waondoke, ama warudi nyuma, jinsi walivyofanya. Hilo litakuwa ni jambo zuri. Mtu fulani, Billy, baadhi yenu nisaidieni, waleteni tu, tuleteeni.

381 Papa hapa, mama huyu papa hapa. Haikubidi kuanza na mtu yeyote yule. Siwezi tu. . . Ninahofu kuwaacha. . . Kama wangewaacha washuke waje huku, je! wanaweza kuja namna

hiyo, ndugu? Vema. Sasa tutaninii tu. . . Sasa tumechelewa tu kidogo, bali ninyi nyote mtanivumilia kwa dakika moja tu, kuomba.

382 Ninamjua dada huyu hapa. Ni—ninaamini yeye ni mfuasi wa kanisa la Ndugu Outlaw. Anaendeleaje? Sawa. Na inasema. . . Loo, siwezi kukumbuka jina lako. Lakini. . . [Dada anasema, "Bagby."—Mh.] Bagby, Dada Bagby. Ninapaswa kukufahamu. Umekuwa mwema kwangu, Dada Bagby. Na hivi haikuwa ninii. . . Wewe siye ambaye Ndugu Outlaw alinipeleka kwake, kumwombea, hospitalini, wakati nilipokuja hapa kwa mara ya kwanza, miaka kadhaa iliyopita? ["Ndiyo."] Ilikuwa ni kitu kama. . . Ulikuwa na nini, kisukari ama moyo? ["TB kooni."] TB ya kooni. Naye angali anaishi kwa ajili ya utukufu wa Mungu. ["Hiyo ni kweli."] Vema, hilo ni sawa kabisa.

383 Sasa Yeye yungali ni Mungu yeye yule usiku wa leo, kama tu vile alivyokuwa. Huenda sisi tumebadilika, bali Yeye hajabadilika. Sasa, hata shida yako iwe nini, Yeye ataiondoa, kama ukiamini. Je! utaamini?

Ninaomba Kanisa liniombee.

384 Baba wa Mbinguni, ninapoweka mikono yangu juu ya dada huyu, katika Jina la Yesu Kristo, Mungu na amponye. Ninatamka baraka hii kwa ajili ya utukufu wa Mungu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina. Sasa, amini, Dada Bagby.

385 Je! unaamini ya kwamba Mungu atakuponya kama tukikuombea, nawe utakuwa mzima? Nawe ni Mkristo, utampa Mungu shukrani zote na sifa. Lakini tunapokuombea, sasa, utaenda nyumbani upate kupona. Hilo linatatua jambo hilo milele. Hakuna kuwazia juu yake tena.

386 Baba yetu wa Mbinguni, pamoja na kanisa hili, ambapo wengi wao ndio kwanza wayaweke maisha yao wakfu tena. Baba, ninaomba ya kwamba utamponya dada yetu, katika Jina la Yesu Kristo.

387 Sasa, si maombi yangu tu, bali hebu angalia kila mahali. Unyofu wa kilindi! Sisi hatuninii. . . Kweli tunamaanisha jambo hili kutoka moyoni mwetu. Utapona.

Utaamini jambo lile lile, sivyo?

388 Baba yetu wa Mbinguni, kwa unyenyekevu wa Roho. . . Na, Mungu, samehe mioyo yetu isiyo minyofu. Tufanye safi, Bwana, tunapoweka mikono juu ya wagonjwa, kwa sababu ni—ni kutamkwa kwa jambo fulani ambalo Mungu aliagiza lifanywe. Basi wasaidie tu maskini watu hawa, Baba. Ninaweka mikono juu ya dada, katika Jina la Yesu, na kuomba ninii yake. . . Mungu ambariki.

389 [Dada fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Hakika. Ninatumaini. . . Mungu akubariki, dada. Hivi waweza kwa dakika moja. . . Mama huyu anakiri kwa uaminifu. Alisema

ana roho fulani juu yake, ya hasira kali. Nasi tunatambua ya kwamba hilo si—hilo si jambo zuri. Lakini, dada, si wewe peke yako, bali kuna wengi wetu, unaona. Lakini labda baadhi yao huenda wasiwe waaminifu jinsi hiyo kukiri hilo. "Lakini yeye atakayekiri dhambi zake . . . Yeye atakayezificha dhambi zake hatafanikiwa. Lakini yeye atakayekiri dhambi zake atapata rehema." Mnajua hilo.

390 Kwa hiyo ninaomba, Baba wa Mbinguni, kwa kuweka mikono juu ya dada, ya kwamba hasira hii itamwondoka. Jalia isimsumbue tena, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Ubarikiwe, dada.

391 Ndugu yangu, unaamini ataninii—atatimiza haja hiyo? Loo! [Ndugu huyo anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Mungu akubariki, ndugu. Labda hiyo, unaona, kuwa na wasiwasi, huenda kukasababisha moyo kuruka namna hiyo.

392 Baba yetu wa Mbinguni, tukitambua ya kwamba hatujui ni wakati gani moyo wetu utakaposimama, huenda ukasimama dakika yoyote. Na ndugu huyu ana ugonjwa wa moyo, pamoja na hasira inayomfanya kushikwa na ghadhabu kali. Loo, ibilisi huyo angetaka kumwingiza kaburini mapema. Bali mimi, kama mtumishi Wako, pamoja na watumishi hawa wengine wote usiku wa leo, tunaomba ya kwamba, katika Jina la Yesu Kristo, ya kwamba hasira hiyo itamwacha, na moyo utakuwa mzima, naye atakuwa mwaminifu kwa Kristo siku zote za maisha yake, na atakuwa na afya apate kumtumikia. Katika Jina la Yesu. Amina.

Ubarikiwe, ndugu, ninaamini imekwisha kabisa. Umeponywa.

U hali gani? Unaamini ya kwamba Yeye atakupa ombi lako?

393 Baba yetu wa Mbinguni, tunamleta ndugu yetu Kwako, chini ya Jina la Bwana Yesu, tunamleta, tuseme, chini ya msalaba, na kumwelekeza juu. Aangalie majeraha hayo pale. Aangalie hiyo Damu inapotiririka kutoka ubavuni Mwake na usoni Mwake, Mwana wa Mungu, akifa, tupate kusafishwa na dhambi zetu zote na magonjwa. Mjalie ndugu yetu. Katika Jina la Yesu, ninaomba ombi hili. Amina.

394 Ninaamini imekwisha. Sivyo, ndugu? Nenda tu nyumbani. [Ndugu huyo anasema, "Amina."—Mh.]

395 U hali gani, ndugu? Unaamini sasa huu utakuwa ndio ule usiku? Yote yatakwisha tangu usiku wa leo, nawe utakuwa mzima. [Huyo ndugu anasema, "Amina."—Mh.]

396 Baba yetu wa Mbinguni, ninapoushika mkono wa ndugu yetu, tangu usiku huu na kuendelea jalia haja yake itimizwe, apate kuwa mzima, na akuishie siku zote za maisha yake. Katika Jina la Yesu. Amina.

Ninaamini itatendeka . . . Utakuwa mzima.

397 U hali gani, ndugu? Huu ndio wakati ambapo yote yamekwisha. Fanya uamuzi wako sasa. [Ndugu huyo anasema, "Amina."—Mh.]

398 Baba yetu wa Mbinguni, kama vile ndugu alivyosema, "Amina," huu ndio wakati ambapo uamuzi unafanywa, papa hapa katika Uwepo wa Kristo. Jalia uishe, tangu usiku huu na kuendelea. Katika Jina la Yesu Kristo, uponywe.

399 [Huyo ndugu anasema, "Asante Bwana."—Mh.] Ubarikiwe, ndugu yangu. Amini yote yamekwisha sasa. ["Amina."]

400 U hali gani, dada? [Huyo dada anasema, "Ninataka umwombee mume wangu. Amekuwa kilema kwa muda wa miaka ishirini."—Mh.] Loo, waweza kunipa leso yako iambatane na hili? Hiyo ni sawa. Hiyo ni sawa. Kitu fulani chochote kile, ishara ndogo. Huenda nikasema, udongo, lakini ninawazia ya kwamba mavazi waliyovaa zamani za kale. Na Yesu je? Yeye alikuwa na vazi moja. Labda ilimbidi kulala nalo, kuishi nalo, lakini angalia kile lilichofunika. Vema.

401 Baba yetu wa Mbinguni, mume wake wa thamani amelala, amelemaa. Na huyu hapa mwenziwe amesimama hapa usiku wa leo, ameshika kitambaa kidogo mkononi mwake. Naye amelemaa. Ninaomba, Baba, ya kwamba utamrehemu. Na kwamba ombi la kanisa hili lililokusanyika pamoja hapa, hawa wanaosafiri hapa Phoenix, na sehemu mbalimbali za nchi ambazo zimewakilishwa hapa usiku wa leo, maombi yetu yatasikiwa. Na wakati kitambaa hiki kitakapowekwa juu ya mtu huyu, jalia nguvu za Mungu zimrejeshe kwenye maisha ya kawaida tena. Katika Jina la Yesu. Amina.

Sasa, limeombwa, sasa na litendeke. Amini hilo, dada.

402 U hali gani, dada? Unataka kuchukua leso yako? Ulikuwa . . . Haja yako sasa, labda wewe ni mgonjwa sana. Je! unataka kusema shida yako, ama ninii tu . . . [Huyo dada anasema, "Nimekuwa na yabisi kavu."—Mh.] Yabisi kavu. Hiyo . . . ["Miaka ishirini na kitu."] Miaka ishirini na kitu.

403 Yupo mtu anayeketi moja kwa moja nyuma yangu, jina lake ni Ndugu Ed Hooper. Alikuwa mahututi kwa huo, hapa Phoenix wakati mmoja, iliwabidi kuweka mikono yake kwenye mito. Sivyo, Ndugu Ed? Naye alikuwa akifa, karibu na kufa, kwa huo, alasiri hiyo, ama jinsi ninavyoelewa na hadithi hiyo. Naye alimwambia mke wake alidhani anaaga dunia wakati huo. Ndipo aliangalia na kumwona Kristo msalabani, ama kitu kama hicho, ameinamisha kichwa mbele, ama kitu kama hicho. Naye aliponywa kabisa, hata angeweza . . . Huyo pale ameketi, papa hapa sasa, ameketi pale nyuma. Naam. Ndugu Hooper, anataka tu kukuona. Yule, inua mkono wako. Haya basi.

Na tuombe.

404 Baba yetu wa Mbinguni, mtu huyu aliyepo anatufanya tujue ya kwamba Wewe ndiwe Mponyaji. Tunaweka mikono yetu juu ya dada. Ombi hili dogo, nyenyekevu lililowekwa wakfu tunaliomba kwa ajili ya uponyaji wake, Baba. Katika Jina la Bwana Yesu, kwa ajili ya utukufu Wake. Amina. Amina.

Nenda ukiamini. Hii ni . . . itakwisha basi. Ulikuwa uninii . . .

405 Hatujasikia? [Mtu fulani anasema, “Hiyo ni kweli.”—Mh.] Mungu awabariki.

406 U hali gani, dada? [Huyo dada anasema, “Nina kisukari, daktari ananiambia, na yabisi kavu. Nimekuwa mgonjwa tangu mume wangu alipokufa miaka mitatu iliyopita.”—Mh.] Dada yetu anaugua, tangu mumewe alipokufa miaka mitatu iliyopita, ana kisukari na yabisi kavu. Naye anaamini ya kwamba Mungu atamponya. Tunaamini jambo lile lile.

407 Baba wa Mbinguni, huku mikono imewekwa juu yake sasa, jalia arudi kanisani pamoja na wengine wengi, akimshukuru tu Mungu kwamba yote yamekwisha na yameondoka. Tunaomba jambo hili liwe hivyo, Baba, katika ombi letu nyenyekevu, katika Jina la Yesu. Amina.

Mungu akubariki, dada yangu. Amini sasa.

408 U hali gani, dada? Unaamini ya kwamba usiku wa leo utakuwa ndio mwisho wake, nawe unaweza kumkubali sasa kama Mponyaji wako? [Huyo dada anasema, “Ndiyo, bwana, ninaamini.”—Mh.]

409 Loo, Mungu wa thamani! “Ombi la imani litamwokoa mgonjwa, Naye Mungu atawafufua.” Tunawazia juu ya Bwana wetu, jinsi alivyosafiri hapa duniani na kuwahudumia wagonjwa, na mambo mengi aliyofanya. Sasa ninamwombea dada yetu, katika Jina la Yesu Kristo. Katika agizo tulilopewa kama wahudumu, tunaomba ombi hili kwa ajili ya uponyaji wake. Amina.

410 Amini tu yote yametendeka sasa. Imani yote uliyo nayo, iweke moja kwa moja pamoja nayo. Itatendeka.

411 U hali gani, ndugu? Juu ya msingi wa Neno Lake, ingekwisha papa hapa. [Ndugu huyo anasema, “Bwana asifiwe.”—Mh.]

412 Baba wa Mbinguni, jalia ombi hili la ndugu yetu. Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe. Amina.

413 [Ndugu huyo anasema, “Bwana ashukuriwe. Amina. Bwana ashukuriwe.”—Mh.] Ubarikiwe, ndugu yangu . . .? . . .

414 U hali gani, dada? Uko tayari sasa, na tayari kupokea uponyaji Wake? [Huyo dada anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Nasi tunapoomba, mnaona, kwa jambo hilo, hakuna kitu kitakachomzuia kuimwaga Roho Yake? [“Labda.”]

415 Baba yetu wa Mbinguni, ninapoweka mikono yangu juu ya dada yetu, nikikuona ukiwaponya watu hawa, ninaomba na kuamini kwa moyo wangu wote ya kwamba utampa ombi lake. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

[Huyo dada anasema, "Asante, Yesu."—Mh.] Mungu akubariki, dada.

416 Mnajua, ninataka tu kusema jambo hili wakati wakija. Kamwe nisingeweza kufahamu ni kwa nini mimi. . .Kabla tu hata sijakuwa mpentekoste, nilizoea kwenda na kuwaombea watu. Hao, wengepona tu. Sijui. Hakuna kitu kingalinibidi kufanya juu ya jambo hilo. Ni ninii tu—ni kumwamini Yeye tu. Nami ninaomba tu, na muda si muda mnajua, watu wangepona.

417 Hivyo ndivyo mtu yeyote anavyofanya. Tunaomba tu na kuamini. Wanapona tu. Hivyo tu. Unaona? Ni wangapi wameponywa kwa uponyaji wa Kiungu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Naam. Mnaona?

418 Loo, mnaona, u—unaweza kujua uko miongoni mwa wapentekoste na watu wa Full Gospel. Hiyo mikono, wanaamini hilo. Mnaona? Hivi hamwoni ni kwa nini Bwana ana juhudi sana kwenu? Si kujaribu kuwaudhi, lakini ni kujaribu, mwajua, kutufikisha mahali hapo "bila waa wala kunyanzi." Ninatumaini hamnikasirikii kwa kuleta maneno kama hayo kutoka katika Biblia. Ni—ninafanya hivyo kwa nia njema kwa Mungu.

419 Hii ndiyo ile saa ya jambo hili kutukia kwako. Sivyo, dada? Sasa, halina budi kutukia, unaona, maana Yeye aliliahidi jambo hilo. Amina? [Huyo dada anasema, "Amina."—Mh.]

420 Baba yetu wa Mbinguni, mbariki dada yetu ninapoweka mikono yangu juu yake. Na kwa imani, kila Mkristo hapa ndani wanaweka mikono yao juu yake. Kanisa hili linaomba, tunaomba kwa ajili ya ugonjwa huu na mateso yamwondoke. Katika Jina la Yesu. Amina.

Ni—ni yale Yeye aliyoahidi.

U hali gani, dada? Unaamini usiku wa leo ndio usiku kwa huo.

421 Baba yetu wa Mbinguni, katika Jina la Bwana Yesu, jalia huu uwe ndio mguso wa kumalizia saa hii, kwamba dada ataponywa. Katika Jina la Yesu. Amina.

Ubarikiwe, dada yangu. Itakwisha, tangu usiku wa leo.

422 U hali gani, dada? Hii ndiyo saa ya uponyaji wako? Vema, bwana.

423 Baba yetu wa Mbinguni, ninamleta dada yetu mbele Zako, katika Jina la Bwana Yesu, na kuomba ombi hili kwa niaba yake, ya kwamba yeye ataponywa katika Jina la Yesu. Amina.

424 Sasa, unaona, si maombi yangu pekee. Kila mtu humu ndani anaomba, unaona, wote katika wakati mmoja. Nasi tunajua ya kwamba Mungu yupo. Tunajua ya kwamba Yeye—Yeye hana budi kuwepo. Unaona? Aliahidi hilo. Nenda zako, ukiamini.

U hali gani, dada? Hii ndiyo saa yake, sivyo ya kuponywa?

425 Baba yetu wa Mbinguni, jalia litatuliwe kwa ajili yake, tangu usiku wa leo na kuendelea. Jalia aondoke kwenye kanisa hili usiku wa leo mwenye furaha, akishangilia, akijua ya kwamba imekwisha. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Ubarikiwe, dada.

426 U hali gani, dada? Huu ndio usiku wa kuponywa kwako, sivyo? Huu ndio wakati, sasa hivi, mbele ya Biblia hii na kanisa, na Kristo.

427 Baba wa Mbinguni, miongoni mwa wahudumu, miongoni mwa walei, waaminio wa kawaida, watakatifu wote wa Mungu, Malaika, na Roho Mtakatifu, katika agizo la Yesu Kristo, ya kwamba, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Kwa hiyo tunadai hilo, litimie, kwa ajili ya dada yetu usiku wa leo, uponyaji wake, katika Jina la Yesu. Amina.

Mungu akubariki, dada yangu.

428 Tutafanya jambo lilo hilo kwa ajili yako, ndugu. Utaamini jambo hilo? [Ndugu huyo anasema, "Ninaamini."—Mh.]

429 Baba yetu wa Mbinguni, yeye alisema anaamini. Kwa hiyo halina budi kutimia, Baba. Hivyo ndivyo ulivyosema. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Naye anaamini. Kwa hiyo tunakushukuru kwa ajili ya uponyaji wake, Baba, katika Jina la Yesu. Amina.

Hilo ni jambo jema. Unajua jinsi ya kulikubali na kuliamini.

430 U hali gani, ndugu? Huu utakuwa ndio usiku wa kuponywa. Acha tu ukae hapa na nenda zako uuache.

431 Baba yetu wa Mbinguni, tunamleta ndugu yetu kwako, katika Jina la Yesu, kwa ajili ya uponyaji wake. Atauacha papa hapa, Bwana. Naye adui itambidi kumwacha. Atawekwa huru tena, katika Jina la Yesu. Amina. Na iwe hivyo.

432 U hali gani? Je! Unaamini Yesu atakuponya hapa usiku wa leo?

433 Baba yetu wa Mbinguni, wakati mtoto huyu anapokuja kupokea uponyaji wake, sisi, kanisa, tunaomba ombi letu, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya uponyaji wake. Amina.

Mnaona? Jambo ndilo hilo. Yote yamekwishwa. Ubarikiwe, dada.

Yote yatakwisha, tangu usiku wa leo na kuendelea, sivyo?

434 Baba yetu wa Mbinguni, watu wanaamini. Wanaamini; wasingekuwa wakitembea kuvuka jukwaa hapa. Wao ni wagonjwa. Wanajua la kufanya. Wamefunzwa. Wanajua ya kwamba hii ndiyo saa ambayo wanafanya uamuzi wao wa mwisho. Nao wanakuja kwa ajili ya thibitisho hilo. “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Nami ninaweka mikono yangu juu yake, katika Jina la Yesu. Hivyo ataponywa. Amina.

435 Mungu akubariki, dada. [Dada anasema, “Ndugu Branham, isingalikuwa ni kwa ajili yako, miaka kumi na mitano iliyopita, ningalikuwa nimekufa.”—Mh.] Hiyo ni . . . [“Hiyo ni kweli. Kwenye ibada ya Ndugu Reed huko Jonesboro, Arkansas.”] Jonesboro, Arkansas. [“Mungu asifiwe!”] Jamani, miaka mingi iliyopita!

436 Shida yako ilikuwa ni nini, dada? [“Vema, nilikuwa na tezi. Kama unaninii . . . Sijui kama unakumbuka, ama hukumbuki.”—Mh.] Sikumbuki. [“Lakini nilikuwa na tezi. Ilikuwa na ninii . . . Ilikuwa *hivi*, na ilikuwa ikiathiri moyo wangu. Na asubuhi hiyo . . . Karibu watu wangu wote ni Mashahidi wa Yehova. Asubuhi hiyo, nilisema, ‘Yeye ni nabii tu wa ibilisi.’ Lakini nilitoka nikaenda shambani kwangu. Mungu akasema nami. Akasema, ‘Catherine, ukienda kwa Ndugu Branham usiku wa leo, utaponywa.’ Ndipo nikarudi ndani ya nyumba na kuwaambia hao wote. Nikasema, ‘Kama nikienda usiku wa leo, Mungu alisema nami, “nitaponywa.”’ ‘Nasi tulikuwa tukienda vivi hivi tu, kumfurahisha.’ Wakaambatana nami. Karibu watu wangu wote sasa ni Wapentekoste.”] Bwana asifiwe!

437 Mngeweza kusikia ushuhuda huo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ngoja sasa, hebu kidogo tu, dada. Nitaurudia.

438 Huko Jonesboro, Arkansas, imekuwa muda, yapata miaka kumi na minne, kumi na mitano iliyopita, alikuwa na tezi kubwa iliyoning’inia nje, shingoni mwake. Naye alikuwa ni Shahidi wa Yehova. Na asubuhi hiyo, wakati amekwisha kusikia kuhusu ibada yetu kule kwa ajili ya Bwana, yeye alisema nilikuwa “nabii wa ibilisi.” Ndipo akaenda shambani kuomba, naye Bwana akasema naye, na kusema, “Panda uende kule na” yeye “angeponywa.” Ndipo Bwana akamponya. Hana tezi. Na watu wake, ambao walikuwa Mashahidi wa Yehova, karibu wote ni Wapentekoste usiku wa leo.

439 Sasa, kama Yeye anaweza kuifanya shingo ya mwanamke huyo mzuri wa Kikristo iwe laini namna hiyo, Yeye anaweza kukuponya. Sivyo? Hakika anaweza.

440 Baba yetu wa Mbinguni, huku mikono imewekwa juu ya ndugu yetu, tunaomba kwa ajili ya uponyaji wake, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mungu akubariki.

Yeye ni yeye yule kwako kama vile angekuwa kwake. Hiyo ni kweli?

441 Baba yetu wa Mbinguni, maombi madogo rahisi pamoja na imani rahisi! Loo, nina furaha sana Bwana, Wewe unalifanya rahisi, kusudi nipate kulielewa, kukukubali tu. Na, Baba, ninaomba ya kwamba Wewe utamponya, na kumfanya mzima, katika Jina la Yesu. Amina.

442 U hali gani, dada? [Huyo dada anasema, "Ndugu Branham, nimefanyiwa upasuaji wa kifua kikuu. Na mbavu zangu sita zilitolewa, katika utumbo. Kapona vema. Na—na inanipa shida nyingi sana. Siwezi kutumia mkono wangu vizuri sana, wajua."—Mh.] Naam, mama. ["Huchoka."] Ninaona jinsi unavyopumua, pia. Nakisia ninii . . . ["Naam. Siwezi kupumua vizuri."] Hilo ni jambo baya sana. ["Siwezi kupumua vizuri. Na mapafu yangu hukunjamana, wajua, ubavuni mwangu."] Loo, naam, jamani! Hilo linasababisha uchungu basi, nadhani. Ninii yake . . . Jamani! ["Naam. Naam. Ndipo inausonga moyo wangu."]

443 Hakuna sababu yake kuteseka tena. Sivyo? [Kusanyiko linasema, "La."—Mh.] Mnaona? Madaktari labda wamemfanyia upasuaji, nao wametoa mbavu kutoka kwenye pafu lake, na labda wakampa matibabu ya numothoraksi, nayo yalikunjamanisha pafu lake. Na—na mama huyu anateseka. Nawe umekuja, ukiamini ya kwamba Kristo atakuponya, nawe unataka kutumia maisha yako yote kwa ajili Yake katika huduma, kumtumikia Yeye. Basi, Wakristo, nafikiri tuna haki ya kumleta bibi huyu mbele za Kristo, Naye atamponya.

Na tuombe, sisi sote.

444 Baba yetu wa Mbinguni, dada yetu anakuja katika ibada nyenyekevu usiku wa leo, akijua ya kwamba daktari wake amefanya yote angaliweza kufanya. Alijaribu sana, bali ingali haiponi. Lakini Wewe ni mponyaji. Ja—jalia apone, Baba. Tunamkabidhi Kwako, ya kwamba utamponya, katika Jina la Yesu. Amina.

445 Ubarikiwe, dada. Uponywe sasa. Ninaamini itapona, nawe utakuwa mzima.

446 U hali gani, dada? Unaamini ya kwamba atakuponya usiku wa leo? [Huyo dada anasema, "Sijui la kufanya, kwa kuwa nina . . . ? . . . matubwitubwi."—Mh.] Vema. Yeye atakuponya, haidhuru, kama tu ukimwamini. Utamwamini? ["Ndiyo."] Vema. Na tuombe.

447 Baba yetu wa Mbinguni, bibi huyu anakuja, akiamini. Yeye alisema hata hajui ana shida gani. Lakini Yeye anajua. Chochote kile, Bwana, anataka kukiondosha. Sisi . . . Mama huyu anajua ni cha adui. Ninaomba ya kwamba Wewe utamjalia haja yake, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Ubarikiwe, dada. Nenda zako, ukiamini kwa moyo wako wote.

448 U hali gani, dada? Unaamini usiku wa leo utakuwa ndio wakati wa kuamua?

449 Nilikuwa nikiwazia, yule mama kutoka Arkansas ambaye ndiyo kwanza ashuhudie. Ninakumbuka, njiani, kamwe sitalisahau kule, mama aliyekuwa ameshika leso. Nilifikiri alikuwa akilia. Na wakati alipoiondoa, hiyo leso, hakuwa na pua. Kansa ilikuwa imekula ikaimaliza pua yake. Na mwanawe alikuwa ni mwangamizi huko Texarkana. Nami ni—nikamwombea.

450 Kesho yake tu asubuhi, mwanamke wa kupendeza amesimama pale, akiangalia, alionekana mwenye umri mdogo sana, na akiniangalia. Akasema, "Hivi hunikumbuki?"

Nikasema, "Siamini ninakukumbuka."

451 Naye mvulana huyo kwa namna fulani akaanza kulia na kuangalia. Ilikuwa ni mama huyo. Alikuwa na pua mpya. Ilikua ikarudi usoni mwake. Ninajua hilo linasikika si jambo la kweli. Nami ni—nisingeninii—nisingetaka kusema jambo lisilokuwa sahihi. Kwa hiyo, hapo, hatupaswi kufanya hivyo. Inatupasa tuwe waaminifu kabisa tunaposema mambo haya. Lakini nilimwangalia mama huyo aliyekuwa amesimama hapo bila pua. Halafu majuma machache baadaye, nikakutana naye tena, alikuwa na pua. Na ili—ilininii tu. . . Alisema hiyo kansa iliacha tu kula. Na baada ya muda kidogo ilianza tu kama kitu kilichokuwa kikikua tena, na hapo akawa na pua tena. Mnaona? Ni ajabu sana kuona jinsi Yeye aliweza kufanya jambo hilo.

452 Sasa, Yeye ambaye angeweza kufanya jambo hilo, anaweza kukuponya. Je! Yeye asingeweza kukuponya, dada? Sio swali, nguvu Zake za kufanya hivyo. Ni kuwa tayari kufanya. Nami ningetaka kukwambia hivi, dada, kama mwanadamu, ya kwamba sote wawili itatubidi kusimama kama hivi katika Uwepo Wake siku moja. Yeye tayari amefanya hivyo, kama tu Yeye angekufanya uamini hilo. Na kuna tendo dogo kama kuwa Mkristo, kubatizwa na kadhalika, namna hiyo. Wewe amini ninapokuombea, utapona, dada.

Sasa, kanisa lote na liombe pamoja nami tunapoomba.

453 Baba yetu wa Mbinguni, msichana huyu mdogo anayesimama hapa, na katika Uwepo wa Mungu. Ninaweka mikono yangu juu yake, na kuomba uponyaji wake, katika Jina la Mwokozi wetu, Yesu Kristo. Amina.

Mungu akubariki, dada. Na litendeke tangu sasa na kuendelea.

454 [Huyo dada anasema, "Ndugu Branham, nimekuja hapa kumwakilisha mama yangu ambaye ana watoto wa macho katika macho yote mawili."—Mh.] Naam. Loo, sawa. ["Yeye ana umri wa miaka tisini na mitano."] Tisini na mitano. Hili ni jambo

zuri, kuja kumwakilisha mama yake mwenye umri wa miaka tisini na mitano aliye na watoto wa macho.

455 Baba yetu wa Mbinguni, wakati akisimama kumwakilisha, alisema, kwa niaba ya mama yake, mwenye umri mkubwa, aliye na watoto wa macho, tunamwombea mama yake. Ee Mungu, kanisa hili tunatoa ombi letu kwa ajili ya uponyaji wa mama yake, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Usitilie shaka. Amini tu.

456 Dada, mpenzi, itakuwa ni mw-. . .Je! unaweza kuamini ya kwamba itakwisha usiku wa leo? [Huyo dada anasema, "Amina."—Mh.]

457 Baba yetu wa Mbinguni, huku mikono imewekwa juu yake, kwa ajili ya kazi iliyomalizika kukamilika, jalia iwe hivyo ndani yake sasa. Katika Jina la Yesu ninaomba. Amina.

Mungu akubariki, dada.

Ndugu yangu, unaamini sasa kwa moyo wako wote?

458 Baba Mungu, tunamleta mvulana huyu kwako hapa, tukiweka mikono yetu juu yake, katika Jina la Bwana Yesu. Jalia kazi ya Kristo iliyomalizika pale Kalvari imalizike ndani yake, kwa kumponya. Amina.

Ubarikiwe, ndugu. Na iishe, usiku wa leo.

459 U hali gani, dada? Tutaamini ya kwamba itakwisha usiku wa leo. [Huyo dada anasema, "Ninaamini, pia na mimi."—Mh.] Mungu ataimalizia papa hapa.

460 Baba yetu wa Mbinguni, ninii tu. . .Imeandikwa, sasa itanenwa, kisha haina budi kutendwa. Jalia iwe hivyo katika mwili wa dada yetu. Katika Jina la Yesu Kristo tunaomba hilo. Amina. Amina.

Tunaamini jambo hilo sasa kwa moyo wetu wote. Atakuwa mzima.

461 Shingo iliyovunjika? [Dada huyo anasema, "La. Ilikuwa ni kurushwa vibaya."—Mh.] Kurushwa vibaya. ["Na ishara hapa. Ninaibeba."] Loo! Naam. A-ha. ["Kuna maumivu wakati wote! . . .?. . . "] Jamani! Maumivu! Vema, dada . . .

462 Sasa, kila mmoja wetu hapa, Wakristo, sisi sote, tunawazia tu jinsi tungalisikia, tukishikwa na hayo. Sasa, vipi kama ilikuwa ni kinyume chake, mama huyo alikuwa akiniombea? Ama vipi kama alikuwa akikuombea? Sasa, jinsi alivyo katika maumivu wakati wote! Sasa, jinsi ambavyo ungetaka mtu awe mwaminifu kweli kweli, mnyofu, na bidii kweli kuhusu jambo hili kwa dhati! Kama ingalikuwa ni mimi, ningefanya hivyo. Na sasa watendee wengine jinsi ungetaka wakutendee wewe. Sasa, kila mmoja wenu na ashikilie tu imani hii, na kama kanisa halisi, useme, kama tunavyosema, useme, "Baba Mungu, ondoa maumivu haya kutoka kwa dada yetu sasa."

463 Baba yetu wa Mbinguni, jalia arudi, akileta kipande hiki kilichozungushiwa shingo yake, akijua haimpasi kukivaa tena, ya kwamba yamemalizwa na Yesu Kristo, wakati kanisa likisihi na kuomba baraka hii. Wajibu Wakristo hawa, Bwana. Wameyaweka wakfu maisha yao Kwako. Katika Jina la Yesu, naomba aponywe. Amina.

464 Hebu na yaishe tu, yakome. Hayatauma tena, na utapona.

Ndugu, naomba iishe sasa. Itatuliwe milele.

465 Baba wa Mbinguni, katika Jina la Bwana Yesu, jalia uponyaji wa ndugu yetu. Tunaomba hili kwa ajili ya utukufu wa Mungu, katika Jina la Yesu. Amina.

Ubarikiwe, ndugu yangu.

Yaishe, tangu sasa na kuendelea.

466 Bwana, maskini mwanamke huyu anayesimama hapa usiku wa leo, jalia kazi ya Bwana Yesu ifanywe ndani ya mwili wake, kwa kuwa kwa mapigo Yake sisi tuliponywa. Tunaomba baraka hii, katika Jina la Yesu. Amina.

Imekwisha sasa.

467 U hali gani? Je! unaamini Yesu atakufanya mzima usiku wa leo? [Huyo dada anasema, "Kushikwa na pumu, na zaidi ya hayo nina uvimbe."—Mh.] Pumu, jamani, hicho ni kitu kichoyo cha kale. Sivyo? Hakika.

468 Ndugu Williams hapa, ndugu, mfanyabiashara Mkristo. Yeye. . . Naam, ni mfanyabiashara. Naam. Yeye alikuwa na ninii. . . Mayo ndiyo kwanza wamkatie tamaa, kwa pumu, wakasema kamwe hataongezeka uzito tena, wala chochote kile. Yeye alikuja kule, imekuwa ni karibu sana mwaka mmoja uliopita, ninaamini, huko maskanini usiku mmoja. Nami nilitoka, nikamwombea, naye Bwana akamponya. Nadhani ameongezeka. Aliketi. . . Walisema asingeongezeka uzito tena, asingeweza kamwe kuongezeka uzito tena. Naye ameongezea thelathini, ratili thelathini na mbili, tangu wakati huo.

469 [Mama mmoja anasema, "Ndugu Branham, kuna msichana mdogo, msichana wetu, mwenye umri wa miaka kumi na saba, aliponywa kwenye mkutano wako wakati ulipokuwa Phoenix, yapata miaka kumi, kumi na mmoja iliyopita. Binti yetu aliye mdogo sana aliponywa ghafla katika ibada. Alikuwa na pumu; karibu tumpoteze. Alikuwa na nimonia, mara kumi na nne."—Mh.]

Unasikia jambo hilo, mpenzi?

470 [Mama huyo anasema, "Mungu ghafla. . . "—Mh.] Je! Mama huyo. . . Yeye yupo hapa sasa? ["Yuko moja kwa moja *pale*, wa—wa tatu kutoka mwisho, safu ya pili sasa."] Kijana msichana hapa pamoja na. . . Loo, naam. Ninaona jambo hili. ["Tuli. . . "]

Endelea. ["Tulishuhudia, kutoka pwani hadi pwani, kumhusu yeye—kuhusu uponyaji wake."] Je! . . .

471 Mnasikia jambo hilo? Sasa angalieni. Yesu alimponya huyo wakati alipokuwa labda ni mdogo kuliko ulivyo wewe. [Huyo mama anasema, "Naam, alikuwa ni msichana mdogo."—Mh.] Mdogo, naye alikuwa na nimonia, na kila kitu, akiugua sana. Na hebu angalia, Yesu anapenda, Yeye anakupenda. Naye . . . Angalia jinsi—jinsi anavyoonekana, mzuri, unaona, na mzima. Sasa, utakuwa hivyo, pia.

Hebu tuombe sasa.

472 Baba wa Mbinguni, tukiweka mikono yetu juu ya msichana huyu mdogo, tunaomba ya kwamba pumu hiyo imwache, naye atakuwa mzima, kwa Yesu Kristo Bwana wetu. Amina.

473 Ubarikiwe. Sasa nenda zako, nawe utapona, na utakuwa mzima, na ushuhudie kama yule mama alivyofanya kwa ajili ya msichana wake mdogo.

U hali gani, dada? Unaamini Bwana Yesu atakuponya?

474 Baba yetu wa Mbinguni, tunaomba ya kwamba utamponya msichana huyu mdogo, pia. Jalia ushuhuda wake uwe kama tu vile yule dada alivyosema sasa hivi. Kutoka pwani hadi pwani na jalia amsifu Mungu kwa wema aliouonyesha. Amina.

Ubarikiwe, dada.

U hali gani, dada? Huu ndio wakati wa kuponywa kwako sasa?

475 Baba yetu wa Mbinguni, mama huyu anapokuja, akiamini kwa unyofu ya kwamba hii itakuwa ndiyo saa ya ukombozi wake, jalia iwe hivyo, Baba, tunapoomba, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

476 Ubarikiwe, dada. Na iishe, tangu sasa na kuendelea, hakuna kuwazia tena juu ya jambo hilo. Unaamini pia, dada.

477 Ninajua hilo linasikika la kifidhuli, kusema, "Hakuna kuwazia jambo hilo tena." Lakini si—silimaanishi namna hiyo. Ninamaanisha, ya kwamba, ninii tu, ni kazi iliyomalizika. Tayari imefanywa. Unaona? Kama tu . . .

478 [Dada mmoja anasema, "Nina ninii—nina uvimbe! . . .?. . ."—Mh.] Kweli. Nawe unaamini ya kwamba atauponya? ["Hakika ninaamini."]

479 Baba yetu wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamponya dada yetu na kumpa afya. Tunaweka mikono juu yake, katika Jina la Yesu, tukiombea uponyaji wake. Amina.

Hebu liishe niani mwako, litatuliwe, na itakuwa ni sawa.

480 U hali gani, mwanangu? [Ndugu anasema, "Nina-. . .?. . . tu—tumboni mwangu."—Mh.] Ati tumboni mwako? Unaamini Yesu atakufanya mzima, mwanangu?

481 Ni mwanao? Unaamini ya kwamba atafanya jambo hilo, dada? Ninajua. Inasikika . . . Vema, unaujua huo ushuhuda, vile sisi . . . vile Bwana amefanya katika Kanisa Lake katika siku za mwisho, zaidi ya vile maskini ndugu yetu mdogo alio nao wakati huu. Yeye ni Mungu, Ambaye anaweza kuumba. Anaweza. Ambapo kama . . .

482 Angalia. Kama shina la ngano linachipuka, na bonge la udongo liliangukie na—na kuitia dosari ngano hiyo, na kuifanya igeuke upande mwingine, basi hiyo ngano haikui vizuri. Lakini ondoa sababu hiyo, ndipo ngano itakua vizuri. Mnaona?

483 Vema, Shetani alifanya jambo baya hapa. Lakini kama maombi ya imani yanaweza kumtoa, basi itakua vizuri. Unaamini hilo, sivyo?

Sasa hebu na tumwombee mvulana huyu wa thamani hapa.

484 Baba wa Mbinguni, jalia nguvu za Mungu, zilizo rahisi lakini hata hivyo zina nguvu, zimponye ndugu yetu mdogo. Jalia kuweko na badiliko katika mvulana huyu hivi kwamba, mama huyu atafurahi sana juu yake, masaa machache yafuatayo. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

485 Mungu akubariki, ndugu yangu. Mwamini Yeye. Mungu akubariki. Mvulana mzuri sana. Mungu akubariki.

486 [Ndugu mmoja anasema, "Nina presha ya kupanda."—Mh.] Presha ya kupanda.

487 Baba wa Mbinguni, ndugu yetu anakiri kwamba ana presha ya kupanda. Ninaomba ya kwamba Wewe utamponya, Bwana. Jalia imwache usiku wa leo. Jalia, wakati atakapofanyiwa uchunguzi mwingine, ama chochote kile, daktari aseme, "Mbona, umeninii, umerudia hali ya kawaida tena." Chini kwenye moyo wake atashukuru, Bwana. Ninaomba katika Jina la Yesu. Amina.

488 [Ndugu anasema, "Baba yangu ni mgonjwa sana. Kama ungeombea leso hiyo, nitampelekea."—Mh.] Nitafurahia kufanya jambo hilo, ndugu yangu.

489 Baba wa Mbinguni, baba ya—yake, wa hapa duniani, ni mgonjwa. Yeye ana leso hapa. [Huyo ndugu anasema, "Ndiyo."—Mh.] Anataka kuiweka juu ya baba yake. ["Utukufu kwa Mungu! Asante, Yesu."] Ee Mungu, ninaomba ya kwamba Wewe utaiheshimu imani ya mwanawe. ["Utukufu kwa Mungu. Ndiyo, Bwana."] Na utamponya baba yake, katika Jina la Yesu. ["Ndiyo. Amina. Asante, Yesu."] Amina. ["Mungu asifiwe!"]

490 Mungu akubariki, ndugu yangu. Mungu na akujalie kila kitu, nami ninaamini atakujalia.

491 Dada, itakwisha sasa, sivyo? Tangu sasa na kuendelea, itaondoka. [Huyo dada anasema, "Ndiyo."—Mh.]

492 Baba yetu wa Mbinguni, wakati sisi, kanisa Lako, tunapomwombea dada yetu katika hali yake, jalia nguvu za Mungu zimponye na kumpa afya, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Ubarikiwe sasa, dada. "Ombeni nanyi mtapewa."

493 U hali gani, dada? Je! Yeye atakuponya tangu usiku wa leo? [Huyo dada anasema, "Ndiyo."—Mh.]

494 Baba yetu wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamponya dada yetu, ukimfanya mzima. [Huyo dada anasema, "Ndiyo."—Mh.] Anakuja na kusema anaamini ya kwamba itakuwa hivyo. Na iwe, basi, Baba. Ninaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Mungu akubariki, dada.

U hali gani, dada? Hii ndiyo saa yako ya ukombozi.

495 Baba yetu wa Mbinguni, watu hawa wanyenyekevu wanatembea jukwaani, wakiamini ya kwamba Wewe utayaponya magonjwa yao. Wamesikia mambo mengi sana yakisemwa. "Na imani chanzo chake ni kusikia," kusikia shuhuda. Ambapo, "Tunashinda kwa Damu ya Mwana-Kondoo na ushuhuda wetu." Ninaomba ya kwamba utamponya dada yetu na kumfanya mzima, katika Jina la Yesu. Amina.

Mungu akubariki, dada, uache papo hapo.

496 Ndugu, mpendwa, na hii itakuwa ndiyo saa ambapo huo utakapokwisha. Hiyo ni kweli?

497 Baba yetu wa Mbinguni, ninamleta Kwako, pamoja na kanisa hili, maombi yao, ya wahudumu hawa wote waaminifu, na mashemasi, na wazee, na washiriki walei, wote. Roho Mtakatifu katikati yetu, akishuhudia Neno Lake. "Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa; watapata afya." Uliahidi jambo hilo, Baba. Sasa yaponye macho yake na umpe afya, katika Jina la Yesu. Amina.

Ubarikiwe, ndugu yangu. Na uishe, tangu sasa na kuendelea.

498 U hali gani, dada? Je! unaamini ya kwamba itakwisha tangu sasa na kuendelea? [Huyo dada anasema, "Ndiyo, bwana."—Mh.]

499 Baba yetu wa Mbinguni, jalia iishe kwa ajili ya dada yetu, tangu usiku huu na kuendelea. Jalia aponywe kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Amina.

Ubarikiwe, dada. Amini sasa kwa moyo wako wote, amini imekwisha.

500 U hali gani? Mtoto mchanga? [Huyo dada anasema, "Naam. Ana mzio ambao umesababisha kushikwa na fadhaa."—Mh.] Loo, jamani! Loo, jamani! Hilo ni baya sana. Wewe ni msichana mdogo mzuri sana. Yesu atakuponya sasa.

501 Sasa, Baba wa Mbinguni, huku nimeweka mikono yangu juu ya mtoto huyu mdogo, nikihisi ndani ya moyo wangu, "Vipi kama ingelikuwa ni Sara, binti yangu?" Ni binti wa mtu

fulani. Ninaomba, Baba, ya kwamba Wewe utamponya maskini msichana huyo kutokana na mzio huu. Na jalia magonjwa haya yamwache. Jalia apone, katika Jina la Yesu. Amina.

502 Sasa utapona, kipenzi, na uwe mzima. Amini hilo, dada.

503 U hali gani, ndugu? Utapona, tangu usiku wa leo. Hiyo ni kweli, bwana? [Huyo ndugu anasema, "Amina."—Mh.]

504 Baba, Mungu, ninaomba ya kwamba, katika Jina la Yesu, ya kwamba utamponya ndugu yetu, umpe afya. Jalia iishe sasa hivi, maishani mwake, kila kitu kiishe; kusudi apate imani, imani isiyoshuku, moyoni mwake. Atakuwa mzima, katika Jina la Yesu. Amina.

505 Ubarikiwe, ndugu yangu. [Huyo ndugu anasema, "Ndugu Branham, ningetaka *hiyo* iombewe, kwa ajili ya mama yangu. Ana umri wa miaka themanini na mitatu. Anasumbuliwa na pumu na ugonjwa wa moyo."—Mh.] Mbona, nakutakia la heri!

506 Baba wa Mbinguni, mama yake, umri wa miaka themanini na mitatu, na ana ugonjwa wa moyo na pumu. Tujalie, Bwana, ya kwamba wakati ishara hii ndogo itakapowekwa juu yake, jalia apate afya, katika Jina la Yesu. Amina.

Mungu akubariki, ndugu, na mama yako, pia.

507 Na iishe, tangu sasa hivi na kuendelea, dada. Hebu tu hilo liwe ni la wakati uliopita. Huu unaokuja hapa ni wakati ujao.

508 Baba wa Mbinguni, katika Jina la Yesu Kristo, mponye huyu, dada yetu. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Umetoweka sasa. Amini tu.

U hali gani, ndugu? Itakwisha, tangu sasa na kuendelea.

509 Baba yetu wa Mbinguni, ninamwombea ndugu yetu, ya kwamba utauponya mwili wake na umpe afya. Jalia iishe, tangu saa hii na kuendelea, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Ubarikiwe, ndugu.

510 [Ndugu mmoja anasema, "Tunamjua mama mmoja. Amepoteza nguvu zake za kuona katika jicho moja, na anabaki na lingine."—Mh.] Loo, jamani! ["Nasi tungetaka kuninii . . ."] Liombewe. Mbona, ningefurahi kufanya hivyo, ndugu. Ninyi aminini pamoja nami sasa, ya kwamba atapona.

511 Baba yetu wa Mbinguni, mama huyo wa kupendeza mahali fulani, anayengojea leso hii iwekwe juu yake. Tunampelekea kwa ajili ya uponyaji wake, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Amina.

Mungu akubariki.

512 Sasa, yupo mama mmoja anayeketi hapa ambaye hawezi kusimama, na mwingine *hapa*, na mwanamume, pia. Nitashuka niende nikawaombee. Sasa, ninyi nyote ombeni pamoja nami. Mtaomba? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

513 [Ndugu Branham anaondoka mimbarani, kuwaombea wale wasioweza kusimama. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

514 [Ndugu fulani anasema, "Bonge alilokuwa nalo ziwani mwake limetoweka, na maumivu yamekwisha."—Mh.] Loo, Mungu asifiwe! [Kusanyiko linashangilia.] Hilo si ni la ajabu? [Kusanyiko linashangilia.]

> Ninampenda, ninampenda,
> Kwani alinipenda kwanza,
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

515 [Dada fulani anasema, "Ndugu Branham, mimi niko karibu na kujifungua mwanangu. Nimerudishwa nyumbani, kurudishwa nyumbani, nikafe kwa kansa. Naye Dada Waldorf alikuja nyumbani. Akaniombea. Akanizungumzia, naye akaniambia niamini kwa ajili ya uponyaji. Nami nimeombewa tayari, nami ninaamini kwa ajili ya uponyaji wangu."—Mh.] Mungu akubariki. ["Lakini mimi si mzima, kwa hiyo je! waweza kuniombea?"] Hakika nitakuombea.

516 Baba wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamponya dada yetu na kumpa afya. Katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba ya kwamba huu utaponywa kabisa, kwa ajili ya mimba hii. Amina.

Mungu akubariki, dada. Nenda na uwe mzima wa afya sasa. Udai uponyaji wako.

517 Mnaona jinsi lilivyo rahisi? Sasa, niambieni ni kitu gani kilichopitia hapa, kuondoa bonge hilo na kumwondolea maumivu mwanamke huyu ambaye hata asingeusikia Ujumbe? Mnaona? Naam. Yeye yuko kule akimsifu Mungu. Kama mwanamke ambaye ni kiziwi, bubu na kipofu pia, anaweza kumsifu Mungu kwa kumwondolea kansa, hakika sisi, tulio na afya kama tulivyo usiku wa leo, tungeweza kumsifu Mungu kwa ajili ya jambo hilo. Sivyo? Naam. Hebu kwa namna fulani tupeane mikono mmoja kwa mwingine tunapoimba.

> Nampe-. . .

518 [Ndugu Branham anapeana mikono—Mh.] Ibada iko wapi, kesho? Imetangazwa? [Ndugu mmoja anasema, "Mahali pale pale. Tempe."] Tempe, Arizona.

[Dada fulani anasema, "Ombea *hiyo*. Ninataka kumwekea yeye hiyo! . . .? . . . "—Mh.]

519 Katika Jina la Bwana Yesu, jalia ya kwamba yeyote atakayewekewa hii, naomba waponywe kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

520 Si Yeye ni wa ajabu? Na—nawaambia jambo hili, ninalipenda tu jinsi Hii. Ni—ninampenda Mungu. Ninampenda kwa moyo wangu wote. Yeye ni Mwokozi wangu.

521 Sasa, kesho usiku, nafikiri ibada ifuatayo iko huko Tempe, Arizona, pamoja na Ndugu . . . Jina Lake ni nani? Ati nini? [Ndugu mmoja anasema, "Groomer."—Mh.] Groomer. Groomer, Ndugu Groomer, huko kwenye Assembly of God. Sivyo? Assembly of God huko Tempe. Full Gospel. Naam. Imetangazwa, nafikiri. Vema.

522 Sasa, mnampenda vizuri sana? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Amina. Ni wa ajabu kabisa!

Sasa, ninamkabidhi ndugu ibada, mchungaji.

Mtu fulani, hebu ngojeni, mtu fulani wa kuombewa? Hebu kidogo.

523 Endelea. [Ndugu mmoja anasema, "Mke wangu amekuwa mgonjwa miaka miwili. Ninataka umwombee."—Mh.] Mbona, ningefurahi kumwombea, ndugu yangu wa thamani.

524 Sasa, kwa ajili ya mke wake aliye mgonjwa, amekuwa mgonjwa kwa muda wa miaka miwili. Sasa hebu tu na tumwamini Baba. Najua ulimwengu ungeweza kupuuza jambo hili na kusema, "Siamini jambo hilo." Vipi kuhusu huyo mama aliyetoa ushuhuda dakika chache zilizopita, ambaye alikuwa na hiyo tezi shingoni mwake pale juu? Vipi kuhusu jambo hilo? Mnaona? Hawa watu ambao wananinii . . . Msichana mdogo hapa, ni kijana mwanamke sasa, kulikuwa na hiyo pumu na kila kitu katika afya yake. Angalieni yote tunayojua kwamba ni kweli. Mnaona? Yeye ataninii . . . Yeye . . . Mungu, kwa mkewe, pia.

Na tuombe.

525 Bwana Yesu, mke mgonjwa. Ninaomba ya kwamba kitambaa hiki, kikiwekwa juu yake, kitakuwa ni ishara ya mkutano huu usiku wa leo na Neno la Mungu. Na jalia aponywe kwa ajili ya utukufu Wako. Amina.

526 Mungu akubariki, ndugu. [Huyo ndugu anasema, "Ndugu Branham, nitakwambia jambo hili. Miaka kumi na mitatu iliyopita, ulikuwa hapa Phoenix. Nilikuwa nimeketi nyuma kwenye kusanyiko. Mungu akaniambia kama ningepanda kule juu na kushika upindo wa nguo yako, ningeponywa. Ibilisi akasema, 'Usiende. Utamruka mtu mwingine.' Ndipo ukasimama na kusema, 'Yupo mtu humu jengoni, wangalikuja na kuigusa, wangekuwa wameponywa.' Niligeuka, nikamwambia ndugu mwenye umri mkubwa, nikasema, 'Mimi ndimi jamaa huyo'"—Mh.] La, la.

Namtakia heri. Na tuombe.

527 Baba wa Mbinguni! Sasa kwa Mungu, ninaomba ya kwamba utatujalia jambo hili! . . . ? . . . Tujalie. Na utujalie jambo hili, Baba, katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Amina.

528 Amelitimiza sasa. Alilitimiza, baada ya miaka kumi na mitatu. "Wale wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya." Ni sawa, ndugu. Loo, ni ajabu sana.

529 Vema, tuonane kesho usiku, karibu ninyi nyote. Kama nikininii . . . Mchungaji hapa sasa, ndugu.

KUDHANIA SWA62-0117
(Presuming)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumatano jioni, tarehe 17 Januari, 1962, katika Gospel Echoes huko Phoenix, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org